# MASUALA IBUKA KATIKA VIPINDI VYA WATOTO: TATHMINI YA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS*

**STEPHEN ODIWUOR OPONDO**

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**OKTOBA, 2025**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa minajili ya kutosheleza shahada yoyote.

Sahihi ………………………………………… Tarehe 07/10/2025……………

Stephen Odiwuor Opondo
AM12/63221/22

**Idhini**

Tansnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu Cha Chuka.

Sahihi ………………………………………… Tarehe 07/10/2025……………

Dkt. Mary Kanyua
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi ………………………………………… Tarehe 07/10/2025……………

Dkt. Onesmus Ntiba
Chuo Kikuu cha Chuka

CHUKA UNIVERSITY
RECEIVED
08 OCT 2025
P.O. Box 109 - 60400, CHUKA
DIRECTOR BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES AND RESEARCH

**HATIMILIKI**

©2025

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kurudufisha, kuhifadhi kwa njia ya kielektroniki au kutoa vipengele fulani kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

## TABARUKU

Kazi hii namtabarukia babangu mpendwa, Maurice Opondo na marehemu mama yangu Benter Adhiambo.

## SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima, nguvu na hekima iliyoniwezesha kukamilisha kazi hii ya utafiti. Ninawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu, Dkt. Mary Kanyua na Dkt. Onesmus Ntiba, kwa mwongozo dhabiti, ushauri wa kitaaluma, na uvumilivu wao wao katika hatua zote za utafiti huu.

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa wahadhiri wangu. Hawa ni, Dkt. Mary Kanyua, Dkt. Onesmus Ntiba, Dkt. Shadrack Kirimi, Bw. Enock Matundura, Dkt. Allan Mugambi na Dkt. Dorcas Musyimi. Mchango wao muhimu ulinilea na kunikuza kitaaluma.

Pia, ninawashukuru wale wote waliotoa maoni ya kujenga na ukosoaji wa kitaaluma katika kazi hii, hasa Bw. Sammy Liana na Bi. Linet Wanjala. Maoni yenu yameimarisha ubora wa utafiti huu.

Shukrani za pekee zimwendee ndugu yangu mpendwa, Vincent Ochieng kwa ufadhili na msaada wake wa kifedha uliokuwa nguzo muhimu ya mafanikio yangu. Pia, dada zangu wapendwa, Judith Akinyi na Dorothy Auma wapokee shukrani zangu za dhati kwa ufadhili wao wa kifedha, ushirikiano wao na maneno yao ya kunitia moyo nyakati zote. Pia nawapongeza ndugu zangu Peter Odhiambo na Fredrick Omondi kwa kunihimiza wakati wote wa utafiti huu.

Sitakuwa mwenye shukrani iwapo sitawataja wapwa wangu wapendwa, Vitalis Barrack na Liz Brenda, ambao kwa kuwa mashabiki wa vipindi vya *Ubongo Kids*, walinichochea kukuza shauku ya kuvifanyia utafiti vipindi hivi. Kwa wote ambao majina yenu hayakutajwa hapa, nawaomba radhi. Mchango wenu haukupuuzwa. Mungu awabariki nyote kwa moyo wenu wa upendo na msaada.

## IKISIRI

Utafiti huu ni wa kifasihi na ulilenga kuchanganua masuala ibuka katika vipindi vya watoto kwenye televisheni, kwa kuangazia vikatuni vya *Ubongo Kids*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Elimu Burudani ambayo iliwekewa msingi na Miguel Sabido (2003). Elimu Burudani ni nadharia iliyofumwa kwa lengo la kuelimisha na kubadilisha mitazamo ya jamii kupitia burudani. Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuelewa jinsi vikatuni vya *Ubongo Kids* vinavyoeleza hali halisi kuhusu maisha ya watu na jinsi watazamaji wanaweza kuchochewa kujenga maana fulani kwa kulinganisha matukio katika kipindi na maisha yao. Sampuli ya utafiti ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji kimaksudi. Ukusanyaji wa data ulitumia mbinu ya kiwango kifu. Hatimaye, mtafiti aliteua video 20 zilizolingana na malengo ya utafiti. Data ilikusanywa kwa kutazama visa, kauli na matendo kwenye vipindi vilivyoashiria masuala ibuka na kunukuliwa ili kurahisisha uchunguzi kuhusiana na masuala ibuka. Uchanganuzi pamoja na uwasilishaji wa data ulifanyika kwa njia ya maelezo. Utafiti ulibaini kuwa masuala ibuka katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* huwasilishwa kwa njia rahisi, yakilenga kuelimisha watoto kuhusu changamoto za sasa. Masuala yanayojitokeza kwenye vipindi hivi ni mabadiliko ya tabianchi, usafi wa mazingira, umuhimu wa lishe bora, elimu, ulinzi wa watoto, usawa wa kijinsia na matumizi salama ya teknolojia. Mafunzo yanayotolewa yanahamasisha watoto kuwa raia wanaowajibika na wanaofikiria kimkakati katika kukabiliana na matatizo ya kijamii. Utafiti huu unatarajiwa kuwafaidi walimu, wakuza mitalaa, waundaji sera, jamii na watafiti wengine kwa kuonyesha ufaafu wa vipindi vya watoto kama kiungo muhimu cha elimu kando na kuburudisha. Kwa kuchambua maudhui, uhusika, na mbinu katika kazi za kifasihi, walimu, wakuza mitalaa na watafiti wengine wataweza kuboresha maudhui ili yaambatane na masuala yanayoikumba jamii kwa sasa kwa njia inayovutia.

## ABSTRACT

This study is literary in nature and aimed to analyze emerging issues in children's television programs, with a focus on the *Ubongo Kids* cartoons. The study was guided by the theory of Entertainment-Education, which was founded by Miguel Sabido (2003). Entertainment-Education is a theory crafted with the aim to educate and change societal attitudes through entertainment. This theory helped the researcher understand how *Ubongo Kids* cartoons depict real-life situations and how viewers can be motivated to construct certain meanings by relating events in the episodes to their own lives. The sample for the study was obtained using purposive sampling. Data collection employed saturation point method. Ultimately, the researcher selected 20 videos that aligned with the research objectives. Data was gathered by observing scenes, statements, and actions in the episodes that highlighted emerging issues, which were then transcribed to facilitate deeper analysis. Data analysis and presentation were carried out descriptively. The study found that emerging issues in *Ubongo Kids* cartoon episodes are presented in a simple and understandable way, aiming to educate children on current challenges. The emerging issues presented in these programs include climate change, environmental cleanliness, the importance of proper nutrition, education, child protection, gender equality, and the safe use of technology. The themes delivered encourage children to be responsible and strategic thinkers in addressing social problems. This study is expected to benefit teachers, curriculum developers, policy makers, the society and other researchers by demonstrating the effectiveness of children's programs as an essential tool for education beyond just entertainment. By analyzing content, character portrayal, and techniques in literary works, teachers, curriculum developers and researchers can enhance content to align with contemporary societal challenges in an engaging manner.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** .......... **ii**
**HATIMILIKI** .......... **iii**
**TABARUKU** .......... **iv**
**SHUKRANI** .......... **v**
**IKISIRI** .......... **vi**
**ABSTRACT** .......... **vii**
**YALIYOMO** .......... **viii**
**VIAMBATISHO** .......... **xii**
**ORODHA YA VIELELEZO** .......... **xiii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Usuli wa Mada .......... 1
1.2 Suala la Utafiti .......... 4
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 5
1.4 Maswali ya Utafiti .......... 5
1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 5
1.6 Upeo wa Utafiti .......... 6
1.7 Maelezo ya istilahi .......... 7

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI** .......... **8**
2.1 Utangulizi .......... 8
2.2 Dhana ya Vikatuni .......... 8
2.3 Masuala Ibuka .......... 9
2.3.1 Masuala Ibuka Katika Fasihi .......... 9
2.3.2 Masuala Ibuka Katika Vikatuni .......... 12
2.4 Mbinu Katika Kazi Za Fasihi .......... 14
2.5 Usawiri wa Wahusika Katika Kazi za Kubuni .......... 19
2.6 Kiunzi Cha Nadharia .......... 23

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** .......... **27**
3.1 Utangulizi .......... 27
3.2 Muundo wa Utafiti .......... 27

3.3 Eneo La Utafiti ........ 27
3.4 Uteuzi wa Sampuli ........ 27
3.5 Ukusanyaji wa Data ........ 28
3.5.1 Zana za Utafiti ........ 28
3.6 Uchanganuzi wa Data ........ 29
3.7 Uwasilishaji wa Data ........ 29
3.8 Maadili ya Utafiti ........ 29

**SURA YA NNE: MASUALA IBUKA YANAYOWASILISHWA KATIKA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS* ........ 31**
4.1 Utangulizi ........ 31
4.2 Mabadiliko ya Tabianchi ........ 31
4.2.1 Chanzo cha Mabadiliko ya Tabianchi ........ 31
4.2.2 Madhara ya Mabadiliko ya Tabianchi ........ 33
4.2.2.1 Ongezeko la Joto Ulimwenguni ........ 33
4.2.2.2 Kukosekana kwa Vyakula ........ 34
4.2.2.3 Kuyeyuka kwa barafu Kaskazini mwa Dunia na Kuzuka kwa Moto wa Porini ........ 35
4.2.2.4 Uchafuzi wa Mto, Hatari ya Magonjwa na Vifo vya Wanyama ........ 36
4.2.3 Jinsi ya Kuzuia Mabadiliko ya Tabianchi ........ 38
4.3 Afya na Usafi ........ 39
4.3.1 Usafi wa Mazingira ........ 39
4.3.2 Umuhimu wa Lishe Bora na Mazoezi ........ 42
4.4 Elimu ........ 43
4.4.1 Mtaala wa Umilisi ........ 44
4.4.1.1 Umilisi wa Teknolojia ........ 44
4.4.1.2 Umilisi wa Hisabati ........ 46
4.4.1.3 Umilisi wa Sayansi ........ 47
4.5 Masuala ya Kijamii ........ 48
4.5.1 Ulinzi wa Watoto ........ 48
4.5.2 Usawa wa Kijinsia ........ 50
4.6 Maarifa ya Kidijitali ........ 53
4.6.1 Usalama Mtandaoni ........ 54

**SURA YA TANO: MBINU ZINAZOTUMIWA KUWASILISHA MASUALA IBUKA KATIKA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS*...........55**

5.1 Utangulizi ....................................................................................... 55

5.2 Uchambuzi wa Mbinu za Kifasihi ....................................................... 55

5.2.1 Maelezo ya Picha na Michoro ya Rangi ............................................ 55

5.2.2 Vichekesho ..................................................................................... 59

5.2.3 Mazungumzo .................................................................................. 61

5.2.4 Matumizi ya Lugha sahili .................................................................. 62

5.2.5 Nyimbo ........................................................................................... 63

5.2.5.1 Wimbo unoambatana na Shughuli za Usafi na Uhifadhi wa Mazingira ............................................................................... 64

5.2.5.2 Wimbo unaofanikisha Shughuli za Mabadiliko ya Tabianchi ............. 65

5.2.5.3 Wimbo wa Shughuli za Usalama Mtandaoni ...................................... 66

5.2.5.4 Wimbo Unaoambatana na Shughuli za Usawa wa Kijinsia ................. 67

5.2.5.5 Nyimbo zinazoambata na Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati . 69

5.2.5.6 Wimbo unoambatana na Haki za Watoto ............................................ 71

5.2.6 Matumizi ya Taswira na Mazingira Yanayofahamika kwa watazamaji ...... 72

**SURA YA SITA: JINSI USAWIRI WA WAHUSIKA UNAVYOFANIKISHA UWASHILISHAJI WA MASUALA IBUKA KATIKA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS* ..........................................74**

6.1 Utangulizi ....................................................................................... 74

6.2 Uchunguzi wa Wahusika ..................................................................... 74

6.2.1. Ngedere .......................................................................................... 74

6.2.2 Mzee Kigo ....................................................................................... 75

6.2.3 Mama Ndege ..................................................................................... 76

6.2.4 Koba ................................................................................................ 78

6.2.5 Kibena ............................................................................................. 78

6.2.6 Kiduchu ........................................................................................... 79

6.2.7 Baraka ............................................................................................. 79

6.2.8 Uncle T ............................................................................................ 80

**SURA YA SABA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO............81**

7.1 Muhtasari wa utafiti ........................................................................... 81

7.2 Hitimisho .......................................................................................... 81

7.3 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadaye ................................................................. 82
**MAREJELEO ........................................................................................................ 84**

**VIAMBATISHO**

Kiambatisho 1: Orodha ya Ukaguzi ........................................................................ 95
Kiambatisho 2: Kibali cha Utafiti kutoka kwa Chuo Kikuu cha Chuka ..................... 96
Kiambatisho 3: Kibali cha Utafiti ............................................................................. 97

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo cha #1, Umuhimu wa Lishe Bora ................................................................56
Kielelezo cha #2, Usafirishaji wa faili Mtandaoni.......................................................57
Kielelezo cha #3, Mabadiliko ya Tabianchi ................................................................58
Kielelezo cha #4, Usafi wa Mazingira.........................................................................59

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Vipindi vya watoto, hasa vikatuni, vina ushawishi mkubwa kwa watoto. Ila vipindi hivi vimebadilika kwa kiasi kikubwa baada ya kuanzishwa kwa kituo cha kwanza cha kupeperusha vipindi vya watoto. Karibu nusu karne imepita tangu kuanzishwa kwa kituo cha kwanza cha televisheni cha watoto, *Nickelodeon* cha Marekani, ambacho kilizinduliwa Aprili 1979 (Imaizumi, 2009). Kwa kauli mbiu yake ya "Watoto kwanza," *Nickelodeon* ililenga kupeperusha aina mbalimbali za vipindi vya watoto kulingana na umri wao. Kutokana na mafanikio ya *Nickelodeon*, vituo vingine vya watoto na vituo vya vikatuni vilizinduliwa Marekani Kaskazini na Ulaya katika miaka ya 1980. Kufikia mwisho wa miaka ya 1990, vituo hivyo vilikuwa vimeenea kote ulimwenguni, ikiwemo Asia, Amerika ya Kusini, Mashariki ya Kati na Afrika (Callus, 2018). Miongoni mwa vituo hivi vya watoto, makundi mawili dhahiri yamejitokeza (Imaizumi, 2009). Kundi la kwanza lilijumuisha vituo vya watoto kutoka Marekani, kama vile *Nickelodeon, Cartoon Network, na Disney Channel*, ambavyo hutawaliwa na programu za Marekani. Kundi la pili linajumuisha vituo vilivyozinduliwa na nchi nyingine, hasa katika miaka ya 1980, kama vile *Children's Channel* ya Uingereza, *Canal J* ya Ufaransa, *YTV* ya Kanada na *KinderNet* ya Uholanzi.

Historia ya vikatuni nchini Kenya ilianza mwisho wa miaka ya 1950, wakati vikatuni vilipoanza kuonekana kwenye magazeti (Callus, 2018). Edward Gitau, anayejulikana kama "Juha Kalulu," ni miongoni mwa waanzilishi. Alitumia michoro kutoa maoni kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii, na kitamaduni. Kwa muda, vikatuni vilianza kubadilika. Badala ya uwasilishaji wa maoni ya kisiasa, vilianza kuonyesha aina mbalimbali za burudani. Vikatuni hivi viliendelea kuonekana kwenye magazeti kama vile *Taifa Leo*, *The Daily Nation* na *The Standard* (Otuoma, 2015).

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, kulikuwa na ushindani mkubwa kutoka kwenye vyombo vya habari mbalimbali nchini Kenya (Karani, 2021). Upanuzi na ushindani katika vipindi vya watoto nchini humo ulichochewa na mtandao wa intaneti, mitandao ya kijamii, umiliki wa simu na majukwaa ya kidijitali. Haya yaliwezesha wabunifu kufikia hadhira pana zaidi.

Mwisho wa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, kuanzishwa kwa televisheni kulileta uhuishaji kwa hadhira pana, huku maudhui ya hapa nchini yakianza kuibuka sambamba na vipindi vya kimataifa (Callus, 2018). Kipindi hiki kilishuhudia ongezeko la uhuishaji wa vikatuni vinavyowalenga watoto, vikichanganya elimu na burudani. Katika mwaka wa 2007, ilikuwa rahisi kutazama mtandaoni vikatuni vya kisiasa kiitwacho *The Stated Opinion Show* kilichooandaliwa na Musa Ihiga. Uhuishaji huo ulikuwa na muundo sawa na *The XYZ Show*. Ulikuwa na mazungumzo ambapo mhusika mwenyeji alimuhoji aliyekuwa rais wa Kenya, Mwai Kibaki kama mgeni katika mtindo wa vikatuni na lenye umbo rahisi.

Kupitia mabadiliko yanayohusiana na ujumuishaji wa kidijitali, vituo kadhaa vya televisheni vya kimataifa kama vile *Jimjam* na *Nickelodeon* vinapeperusha vipindi vya watoto, hasa vikatuni. Gitonga (2020) anasema kuwa idadi ya wastani ya watazamaji wa televisheni nchini Kenya walio chini ya miaka kumi na minne ni milioni moja na elfu mia mbili kila siku. Idadi hii hupatikana kati ya saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni. Aidha, kati ya mwaka wa 2014 na 2023, utazamaji wa televisheni na upatikanaji wa mtandao uliongezeka maradufu (*Communications Authority of Kenya*, 2024). Ongezeko hili linaonyesha jinsi Wakenya wanavyokumbatia na kukuza uhusiano wao na vyombo vya habari. Hivyo, televisheni na majukwaa ya mtandaoni yanachukua nafasi kubwa katika kuburudisha na kuelimisha hadhira.

Hata hivyo, Kacungira na Owuor (2023) wanaeleza kuwa mandhari ya vipindi katika televisheni nchini Kenya yamepata mabadiliko makubwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Vipindi hivi vimeanza kuzingatia masuala ibuka. Masuala ibuka ni mambo yanayochipuka katika jamii na yanaathiri au yatazidi kuathiri jamii kwa kiwango kikubwa (Wasike, 2015). Kwa sababu hiyo, Taasisi ya Elimu nchini Kenya ilipendekeza ufunzaji wa masuala ibuka katika shule za msingi na sekondari.

Pia, masuala ibuka yalipendekezwa kujumuishwa katika uandishi wa fasihi katika mwaka wa 2002 (Wizara ya Elimu, 2002). Aidha, waandishi wa fasihi ya watoto walipata motisha na mwamko kuanza kutunga maudhui yanayohusiana na masuala ibuka kutokana na Haki za Watoto.  Haki hizi zilitambuliwa na kutiwa saini mwaka

1989 huko Monrovia, wakati wa mkutano wa 16 wa viongozi wa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (Lloyd, 2010).

Amukowa (2018) anasisitiza kuwa kazi yoyote ile inayolenga watoto huakisi mambo wanayokabiliana nayo katika maisha. Hii ni hali inayoonekana kutokana na kazi mbalimbali zilizotungwa kwa ajili ya watoto. Katiba ya Kenya (2010) inatambua mtoto kama mtu ambaye hajafikisha miaka kumi na minane. Ukweli ni kwamba, kuna mahitaji mapya katika ulimwengu wa kisasa kutokana na masuala ibuka. Masuala haya yanahusu maeneo ya afya, mazingira, siasa, na elimu. Watoto wanapaswa kuandaliwa mapema ili kukumbana nayo. Miongoni mwa vipindi vya televisheni vinavyoakisi masuala ibuka ni vikatuni, ambavyo ni njia maarufu ya burudani kwa watoto.

Prithviraj na wenzake (2024) wanaeleza kuwa wahusika katika vikatuni—ambao kihistoria walikuwa kwenye vichekesho, televisheni, na filamu, sasa wanachukua nafasi muhimu katika maisha ya watoto. Baada ya kipindi cha virusi vya COVID, kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaotazama vikatuni. Kuongezeka kwa kutazamwa kwa vikatuni kunachangiwa na sababu kadhaa, ikiwemo: upatikanaji rahisi wa intaneti, kuongezeka kwa vifaa vya kisasa vya kidijitali, fursa chache za maingiliano, na matumizi ya vikatuni kama njia rahisi ya kuwaburudisha watoto. Vikatuni haviburudishi tu, bali pia huathiri mwingiliano wa kijamii na uzoefu wa kielimu. Hali hii inaangazia jinsi teknolojia inavyoendelea kuathiri ukuaji wa watoto.

Sani na wenzake (2012) nao wanasema kuwa, kupitia vikatuni vya kisiasa, vyombo vya habari hutoa maoni kuhusu masuala ya kisasa ya kijamii ili kubadilisha mitazamo ya watu na kuwapa taarifa kuhusu masuala yanayoathiri maisha yao. Ni wazi kwamba jukumu la vyombo vya habari la kuweka ajenda lina umuhimu mkubwa katika kuwaelekeza watu kuhusu masuala yanayohusiana na maslahi ya umma. Aidha, kuna njia nyingi ambazo vikatuni vinaweza kutumia kushughulikia masuala ya kijamii. Wanaobuni vikatuni wanaweza kuonyesha wahusika tofauti tofauti na wengine wanaweza kuunda hadithi zinazohusiana na matukio ya sasa.

Boyd (2015) anaeleza kuwa vikatuni huwa na msuko ulio na michoro iliyopangwa kwenye paneli inayozidisha moja ili kujenga mtiririko ndani ya hadithi. Hivyo, michoro ya picha hutumiwa kupambanua maana ya maandishi, na maandishi hutumiwa

kukamilisha vikatuni. Ingawa vikatuni si lugha kwa maana halisi, huwasilishwa kwa njia ya kuona, sawa na jinsi riwaya husimuliwa kwa maandishi. Kwa mujibu wa Eisner (1985), vikatuni hutumia lugha ya picha na istilahi zilizoandikwa ili kufikisha maana au dhana fulani. Mtazamo huu unaendelezwa na Neil (2012) ambaye anasisitiza kuwa vikatuni si aina ya sanaa tu, bali ni aina ya lugha inayozidi kukua. Kwa upande wake McCloud (1993), anafafanua kuwa vikatuni ni mtiririko wa michoro iliyopangwa kwa makusudi ili kuwasilisha taarifa au kuchochea uelewa.

*Ubongo Kids* ni vipindi vya vikatuni vinavyobuniwa Tanzania na ni maarufu barani Afrika kutokana na mbinu yake ya kipekee ya kufundisha watoto. Vipindi hivi vimechochea hamu nchini Kenya kutokana na thamani yao ya kielimu na maudhui yanayohusiana na changamoto zinazokumba jamii za Kiafrika na ulimwengu wote. Vipindi hivi vinachanganya burudani na elimu. Vinalenga masomo kama hisabati, sayansi na stadi za maisha ambazo huwasilishwa kupitia hadithi za kuvutia, muziki na michoro ya kuvutia. Vipindi vya *Ubongo Kids* vinalenga watoto kati ya umri wa miaka 7 na 14 (Ubongo, 2024). Tangu kuanzishwa kwake mwezi Julai 2013 jijini Dar es Salaam, Tanzania, *Ubongo Kids* inapeperusha maudhui ya elimu, kuwaburudisha na kuwatia watoto hamu ya kujifunza na kusoma. Vipindi hivi hutafsiriwa kwa lugha tofauti, zikiwemo Kiingereza, Kifaransa, Kiswahili, Kinyarwanda, Kikuyu na Kijaluo.

Yaliyomchochea mtafiti ni kuwa watoto ni kiungo muhimu katika jamii na vipindi vyao vya televisheni vina jukumu muhimu katika kukuza watoto kiakili, kijamii, na kihisia (Kajuna, 2015). Watoto hutumia muda mwingi kutazama vipindi wapendavyo kwenye televisheni. Nchini Kenya, matumizi ya burudani kupitisha ujumbe wa kielimu kupitia vyombo vya habari yamepata umaarufu. Licha ya ongezeko la umaarufu na mapokezi chanya ya vipindi hivi hasa vikatuni, ipo haja ya kuchunguza kwa kina ikiwa yapo masuala yanayoathiri jamii ya kisasa kwenye vipindi hivi ili kueleweka.

## 1.2 Suala la Utafiti

Vikatuni ni mojawapo ya zana maarufu zinazoburudiisha watoto. Pia zina uwezo wa kutumika kama nyenzo ya kuunda, kubadilisha na kuathiri mitazamo ya watoto. Nchini Kenya, watoto hutumia muda mwingi kutazama vipindi wapendavyo kwenye televisheni. Matumizi ya burudani kupitisha ujumbe wa kielimu kupitia vyombo vya

habari pia umepata umaarufu. Hata hivyo, mabadiliko ya haraka katika mazingira ya vyombo vya habari, pamoja na changamoto zinazoibuka katika jamii, zinasababisha kuwepo kwa haja ya kuchunguza kwa kina ikiwa yapo masuala yanayoathiri jamii ya kisasa kwenye vipindi hivi ili kueleweka. Pia, ipo haja ya kukuza watoto tangu utotoni mwao kuhusiana na masuala yanayoathiri jamii. Ingawa vipindi vya *Ubongo Kids* vimefanikiwa kuwavutia watoto, kuna haja ya kuvichunguza kutokana na mabadiliko ya mahitaji ya kielimu na kijamii. Kwa hivyo, utafiti huu ulinuia kuchunguza uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

i. Kujadili masuala ibuka yanayowasilishwa katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.
ii. Kubainisha mbinu zinazotumiwa kuwasilisha masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.
iii. Kuchunguza jinsi usawiri wa wahusika unavyofanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, ni masuala ibuka gani ibuka yanayowasilishwa katika vikatuni vya *Ubongo Kids*?
ii. Je, ni mbinu zipi zinazotumiwa katika vikatuni vya *Ubongo Kids* kuwasilisha masuala ibuka?
iii. Ni kwa jinsi gani wahusika wamesawiriwa ili kufanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utawasaidia walimu kutambua vikatuni kama nyenzo za kufundishia. Vikatuni hurahisisha uwasilishaji wa masuala magumu kwa njia ya burudani. Kupitia mbinu hii ya kielimu, walimu wataweza kuongeza ushiriki wa wanafunzi na kufanya mchakato wa kujifunza kuwa wa kuvutia na wenye maana zaidi. Pia, utafiti huu unanuia kuwapa wakuza mitaala maarifa kuhusu nafasi ya vikatuni katika kukuza ujuzi wa karne ya 21 kama vile ubunifu. Maarifa haya yanaweza kusaidia kuboresha mbinu za kisasa za ufundishaji na kuhakikisha mitaala inatimiza mahitaji ya kizazi cha sasa na kijacho. Aidha, matokeo ya utafiti huu yanaweza kusaidia watunga sera kushirikisha

teknolojia na elimu burudani ili kujenga mfumo wa elimu wa kisasa unaolenga ujuzi. Kwa jamii, utafiti huu unaongeza maarifa mapya kuhusu elimu burudani na jinsi inavyoweza kutumika kuwasilisha masuala yanayoiathiri jamii kama vile mabadiliko ya tabianchi, afya na lishe bora. Kupitia njia hii ya ubunifu, jamii inaweza kufaidika kwa kuhamasishwa na kuelimishwa katika mazingira yanayochanganya burudani na elimu. Hatimaye, utafiti huu utasaidia kuongeza ufahamu miongoni mwa watafiti kuhusu uwezo wa vipindi vya watoto kuwa kama kiungo muhimu cha elimu, kando na kuwaburudisha watoto.

### 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita kwenye *Ubongo Kids* ambacho ni kipindi cha vikatuni vya kielimu vinayobuniwa Tanzania. Mtafiti alitumia mbinu ya kiwango kifu. Alikusanya data hadi pale ambapo hakuna masuala au maarifa mapya yalibainika, na data ilianza kujirudia. Hii ilionyesha kuwa ukubwa wa sampuli uliokusudiwa ulifikiwa. Hivyo, mtafiti alichagua video 20 kimaksudi. *Ubongo Kids*, kama kipindi maalum cha uchunguzi, kilichambuliwa kwa kuzingatia yaliyomo ili kubaini masuala yanayoathiri mazingira ya vyombo vya habari vya kisasa. Kwanza, utafiti huu ulijikita katika kuteua na kujadili masuala ibuka teule yaliyowasilishwa katika vipindi vya *Ubongo Kids*. Pili, utafiti ulijikita katika kubainisha mbinu mbalimbali zilizotumiwa kuwasilisha masuala haya. Aidha, utafiti ulichunguza jinsi usawiri wa wahusika katika vipindi vya *Ubongo Kids* ulivyofanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka. Uchanganuzi wa masuala husika uliongozwa na nadharia ya Elimu Burudani.

**1.7 Maelezo ya istilahi**

Istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti huu ni:

**Mtoto:** Mtoto ni mtu yeyote aliye na umri chini ya miaka kumi na minane na ambaye ni mtazamaji wa vipindi vya *Ubongo Kids*.

**Masuala ibuka:** Mambo ambayo yanawasilishwa katika vipindi vya *Ubongo Kids* na yamekuwa au kuchipuka katika jamii na yanaathiri au yatazidi kuathiri jamii kwa kiwango kikubwa.

**Ubongo Kids:** Kipindi maarufu cha watoto ambacho huchanganya burudani, hadithi za kusisimua na wahusika wa kupendeza ili kuelimisha na kuburudisha watoto.

**Elimu ya kidijitali:** Elimu ya watoto katika vipindi vya *Ubongo Kids* kuhusu matumizi ya teknolojia ya kidijitali ikiwa ni pamoja na vifaa na mtandao.

**Uendelevu wa mazingira:** Kuwapa watoto mafunzo juu ya madhara ya uchafuzi wa mazingira na uhifadhi wa mazingira katika vipindi vya *Ubongo Kids*.

**Usawa wa kijinsia:** Ukuzaji wa ujumbe kwenye vipindi vya *Ubongo Kids* unaohimiza umuhimu wa haki sawa kwa wavulana na wasichana.

**Vikatuni:** Vikatuni ni aina ya sanaa ya uhuishaji inayotumia michoro kuonyesha wahusika na kusimulia kwenye vipindi vya *Ubongo Kids*.

# SURA YA PILI
# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii iliangazia tafiti za awali zilizohusiana na mada ya utafiti. Pia, sehemu hii ilitoa muhtasari wa maarifa ya sasa, mbinu, na mapungufu katika tafiti zilizokwisha kufanywa. Muhtasari huo ulisaidia kujaza pengo lililokuwepo katika utafiti huu. Sehemu hii imegawanyika katika vipengele vikuu: dhana ya vikatuni, masuala ibuka katika kazi za fasihi, mbinu katika fasihi, na uhusika.

## 2.2 Dhana ya Vikatuni

Vikatuni daima vimekuwa msingi wa burudani kwa watoto na watu wazima. Vikatuni vimekuwa sehemu ya utamaduni maarufu kwa zaidi ya miaka mia moja na ushawishi wavyo ulionekana katika vyombo anuwai vya burudani. Bagwan (2021) anaeleza ya kuwa neno vikatuni linahusiana na *caricature*. Neno *caricature* linatokana na neno la Kiitaliano, *caricare*, ambalo linamaanisha kutia chumvi. Mara nyingi vikatuni vina tabia ya kipekee kama vile uwiano usio wa kawaida, maumbo au rangi zisizo za kawaida, sehemu kubwa za mwili au vipengele vya uso ambavyo havifanani na miili yao. Kile kilichoanza kama michoro rahisi katika magazeti na vitabu vya vichekesho imeongezeka kuwa tasnia ya mabilioni ya dola, inayojumuisha maonyesho ya uhuishaji, filamu na michezo ya video (Bagwan, 2021). Katika ngazi yake ya msingi, vikatuni ni mchoro au mfululizo wa michoro ambayo huwasilisha maana kwa njia ya ucheshi. Vimekusudiwa kuburudisha na kushirikisha watazamaji katika ulimwengu wa fantasia au kwa kuonyesha upuuzi wa maisha ya kila siku.

Mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, vikatuni vilitumika kama njia ya kueneza siasa, kuchekesha na kuendeleza mjadala katika jamii. *Honoré Daumier* huko Ufaransa ni miongoni mwa wachoraji wa vikatuni kama hivyo. Hata hivyo, katika mwaka wa 1920 na 1930, ongezeko la uchapishaji wa magazeti lilipanua haja ya matumizi ya vikatuni kama njia ya burudani, hasa kuchekesha. Ni katika kipindi hiki ambapo majina maarufu kama vile Walt Disney na Charles M. Schulz walileta vikatuni kama vile *Peanuts* kwa hadhira yao. Katika karne ya ishirini, maendeleo ya teknolojia pamoja na uchapishaji yalichangia katika uendelezaji wa vikatuni (Leon, 2017). Pia, vyombo vya habari kama vile magazeti na televisheni vilitumika kuendeleza vikatuni. Leo hii, vikatuni hutumika

duniani kote na hutumika kuchekesha, kuelimisha na kutoa maoni katika mitandao ya kijamii, majarida na vyombo mbalimbali vya mawasiliano.

Hata hivyo, neno vikatuni limebadilika kadri muda unavyosonga. Maana yake ya awali ilirejelea mchoro wa maandalizi kwa ajili ya kazi ya sanaa, kama vile uchoraji (Kaula, 2015). Katika karne ya kumi na tisa na ishirini, neno vikatuni lilianza kumaanisha michoro ya kuchekesha katika majarida na magazeti. Matumizi ya sasa ya neno vikatuni mara nyingi hurejelea vipindi vya televisheni na filamu fupi za watoto. Vipindi hivi huhusisha mashujaa, matukio ya ujasiri, na mara nyingi huwaangazia watoto kama wahusika wakuu.

Utafiti huu ulinuia kuchanganua majukumu muhimu ya vikatuni vya *Ubongo Kids* katika kushughulikia masuala ibuka. Kamina na Mokua (2024) wanasema kuwa maisha ya watoto leo hii yanaathiriwa sana na mitandao ya kijamii kuliko wakati wowote ule. Vyombo vya habari vina uwezo wa kuathiri mitazamo ya kijamii na kubadilisha tabia kwa njia zisizo dhahiri lakini zenye nguvu. Hivyo, vikatuni huruhusu watoto: kubaini uhusiano kati ya burudani na elimu na kuwa na habari kuhusu matatizo katika mazingira. Vikatuni pia hukuza maendeleo ya utambuzi na ujuzi wa kihisia.

### 2.3 Masuala Ibuka

Maureen (2015) anaeleza masuala ibuka kama mambo mapya au mabadiliko yanayogusa jamii ya kisasa. Mabadiliko haya yanajumuisha nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidini, na kiteknolojia, na yanaathiri jamii kwa njia mbalimbali. Naye Simala (2016) anafafanua suala ibuka kama jambo ambalo halijafikiriwa lakini ni muhimu kufikiriwa na pia huweza kuwa jambo muhimu linalofahamika ila inabadilika. Masuala ibuka huhusu maisha kwa jumla, kutoka siasa, uchumi, teknolojia, utamaduni na afya. Jamii ya kisasa inakumbwa na masuala ibuka kama vile mihadarati, maadili, dhuluma dhidi ya watoto, ufisadi, haki za binadamu, uongozi, na ubaguzi wa kijamii.

#### 2.3.1 Masuala Ibuka Katika Fasihi

Nanda (2011) anaeleza kuwa ingawa binadamu ana mamlaka juu ya mazingira yenyewe yana haki ya kutunzwa na binadamu. Aidha, ukiukaji wa haki ya mazingira ndiyo chanzo kuu cha uharibifu wa mazingira. Binadamu hajaonyesha mafanikio ya kulinda

na kuhifadhi mazingira kutokana ukiukaji wowote. Kutokana na utafiti huu, ni wazi kwamba binadamu ana jukumu la kutunza na kulinda mazingira yake licha ya changamoto anazokumbana nazo. Utafiti huu una mchango kwa falsafa ya mazingira, kwani unapanua wigo wa uwajibikaji wa kimaadili. Licha ya Nanda kuzungumzia masuala muhimu ya kimazingira, anakosa mjadala kuhusu jinsi mawazo haya yanavyoweza kuwasilishwa katika mazingira ya darasani, uundaji wa mtaala, au vipindi vya watoto. Tofauti na utafiti wa Nanda (2011), utafiti huu ulibaini kuwa vipindi vya vikatuni vya watoto hutumika kupeperusha masuala ibuka kama vile mabadiliko ya tabianchi, afya, elimu, ulinzi wa watoto na usalama mtandaoni.

Maureen (2015) anaangazia jinsi masuala ibuka yanavyojitokeza katika riwaya za kisasa kwa kuteua riwaya mbili ambazo ni *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga Nafsi Yangu.* Waandishi katika riwaya hizi mbili wanateua masuala yanayorejelea jamii na kuyasimulia kupitia ubunifu wa kiwango cha juu. Utafiti huu ulibainisha kuwa masuala hayo ni pamoja na ulemavu, ukiukaji wa haki za kibinadamu, haki za watoto, ufisadi, elimu katika jamii na uongozi mbaya. Pia, kuna magonjwa sugu kama vile saratani na UKIMWI pamoja na ubaguzi. Maudhui yanayozingatiwa katika riwaya hizi yanazingatia hali halisi pamoja na mvutano na mkinzano anayokuwa nayo binadamu na mazingira yake. Riwaya zilizotathminiwa na Maureen ni za watu wazima na zina maudhui mazito ambayo hayalengi watoto moja kwa moja wala hayajaandikwa kwa mtazamo wa kisomo cha watoto. Hivyo yana ukomo katika kueleweka au kufundisha watoto masuala ibuka kulingana na umri wao. Tofauti na utafiti wa Maureen (2015), utafiti huu ulibainisha kuwa vipindi vya vikatuni vya watoto hutumia elimu burudani ili kupeperusha masuala ibuka kwa njia inayoeleweka kwa watoto na inayowatia hamu ya kutaka kutazama vipindi husika ili kuelimika.

Ngugi (2017) alifanya alitafiti kuhusu jukumu la hadithi katika kufafanua masuala yanayoibuka katika jamii, hususan jinsi masuala hayo yanashughulikiwa katika vitabu vya watoto. Kutokana na utafiti wake, jamii ni msingi wa kazi za fasihi na kazi hizi zina uwezo wa kuathiri watoto kwa njia tofauti. Zaidi ya hayo, ni muhimu kuzingatia kwamba fasihi inapaswa kuipa jamii, hasa watoto, fursa nzuri ya maisha kulingana na mabadiliko yanayotokea katika jamii ya sasa. Utafiti huu unafafanua kwamba jamii inakumbwa na masuala kama vile ulemavu, suala la UKIMWI na haki za watoto kama

vile malezi. Tofauti na utafiti huu, ambao umejikita katika vipindi vya watoto, hasa vikatuni vya *Ubongo Kids*, utafiti wa Ngugi ulijikita katika dhana ya hadithi-matini.

Dhana ya kijinsia na kiuana imekuwa ikifanyiwa mjadala na wataalamu kutoka maeneo mbalimbali, wanaochunguza sekta tofauti kama vile za kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kielimu. Opunde na wenzake (2018) waliangazia masuala ya kijinsia kwa kuegemea nyimbo za Daudi Kabaka na John Amutabi Nzenze. Kwa mtazamo wao, masuala ya kijinsia na kiuana ni miongoni mwa changamoto zinazoibuka katika jamii za sasa. Utafiti huu unamchora mwanamke kama kiumbe anayependa anasa, anayepaswa kuvumilia na mlezi mkuu wa ndoa. Nyimbo za Daudi Kabaka na John Nyenze pia zinahusishwa na masuala ya kiuchumi, kisiasa, kielimu na kiteknolojia. Utafiti huu ulisaidia kuelewa jinsi jinsia inawakilishwa katika fasihi. Pia, ulisaidia kutambua na kushughulikia ubaguzi wa kijinsia na upendeleo katika kazi za fasihi. Ingawa Opunde na wenzake (2018) walibainisha picha changamano kuhusu mwanamke kama mpenda anasa na mlezi wa ndoa, utafiti huu ulionyesha kuwa vipindi vya *Ubongo Kids* hunuia kupeperusha mtazamo chanya kuhusu masuala ibuka kwa kuwahamasisha watoto kuwa raia bora na wanaowajika na kupinga mila potofu katika jamii. Hivyo, vipindi hivi husaidia kuwafundisha watoto maadili mema na kuwahamasisha kubadilisha jamii kuwa bora zaidi.

Sapsağlam (2018) alifanya utafiti ili kuchunguza uelewa na matumizi ya mitandao ya kijamii miongoni mwa watoto wenye umri mdogo. Utafiti huu ulibaini kuwa idadi kubwa ya watoto ilikuwa inafahamu matumizi ya programu za mitandao ya kijamii na kwamba walikuwa wanazitumia kupitia simu za wazazi wao. *YouTube* ndio ulikuwa mtandao uliofahamika na kutumiwa zaidi, ambapo watoto walitazama vikatuni na video. Utafiti huo unaonyesha jinsi watoto wanavyozidi kuathirika kutokana na teknolojia. Tofauti na utafiti wa Sapsağlam, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa vipindi vya watoto vinaweza kuwa njia mwafaka ya kuwaelimisha watoto kuhusu mambo yanayowaathiri kupitia burudani.

Wesonga na wenzake (2020) walitathmini nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kwa kuangazia riwaya ya *Tikitimaji* na *Msimu wa Vipepeo*. Utafiti huu ulitumia nadharia ya fasihi mazingira na nadharia ya uhalisia. Watafiti wanaangazia

masuala yanayohusiana na uchafuzi wa mazingira kama vile ukataji miti, uhasama uliopo kati ya binadamu na wanyama na pia umwagaji wa taka chafu kutoka viwandani kwenda mitoni. Utafiti huu ulibaini kuwa fasihi ni nyenzo mwafaka inayoweza kutumika kuwasilisha masuala ya mazingira kikamilifu. Hii ni kwa sababu fasihi inaingiliana na jamii. Tofauti na utafiti wa Wesonga na wenzake, ambao ulichambua suala la mazingira pekee, utafiti huu ulijikita katika masuala ibuka kwa jumla.

Murimi na Mukuta (2024) walichunguza ukiukaji wa haki za watoto katika *Chozi la Heri* na *Nguu za Jadi.* Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia na kutumia muundo wa kimaelezo. Eneo la kukusanya data lilikuwa maktabani. Utafiti huu ulibanisha kuwa fasihi ni zao la wakati na inaweza kubadilika kutegemea mabadiliko katika jamii ili masuala mpya yanayoibuka yamulikwe. Masuala hayo mapya katika jamii ni kama usawa na haki za binadamu. Utafiti huu pia ulibainisha kuwa haki za watoto zinakiukwa kwa kudhulumiwa kimapenzi, ndoa za mapema, na kukatiziwa elimu. Pia, watoto walitelekezwa na wazazi wao, walibaguliwa, waliachishwa masomo, na walifanyiwa uavyaji mimba. Ni bayana kwamba uchunguzi wa Murimi na Mukuta ni tofauti na utafiti huu. Uchunguzi wao ulichunguza suala ibuka kwa kuegemea upande wa ukiukaji wa haki za watoto katika riwaya, huku utafiti huu ukiegemea masuala ibuka kwa jumla na jinsi yanavyojidhihirisha katika vikatuni vinavyotazamwa na watoto.

### 2.3.2 Masuala Ibuka Katika Vikatuni

Kidenda (2006) anaeleza kuwa vipindi vya watoto, hasa vikatuni kwenye televisheni, vina ushawishi mkubwa kwa tabia na utamaduni. Kwa watoto wengi, vyombo hivyo ndio chanzo kikuu cha kujifunza utamaduni. Pia vipindi vya televisheni vina ushawishi wa kijamii kwa watoto kuhusu mitazamo yao ya majukumu ya kijinsia. Vipindi hivi vinatoa ujumbe muhimu wa kuvutia kuhusu majukumu ya kijinsia yanayokubalika kijamii. Mara nyingi, majukumu hayo huwa na ubaguzi na mambo yaliyopitwa na wakati. Vipindi hivi wakati mwingine huwasawiri wanaume kama wenye majukumu ya uongozi na wa kufanya maamuzi. Wakati huo huo, wanawake wanahimizwa kuwa watiifu na kuwategemea wanaume. Utafiti wa Kidenda ulitoa mwanga kwa mtafiti kuhusu nafasi ya vikatuni katika kujenga au kubadilisha maadili ya kijamii, utamaduni, na tabia miongoni mwa watoto. Vikatuni vina uwezo wa kufundisha na kuunda mitazamo ya kijamii, ambayo mara nyingine inaweza kuwa na upendeleo wa kijinsia

au kuendeleza dhana za kitamaduni zilizopitwa na wakati. Tofauti na utafiti wa Kidenda (2006), utafiti huu ulibaini kuwa vipindi vya vikatuni vina uwezo wa kutumika kama chombo chanya cha kuburudisha na kuelimisha kuhusu changamoto za kijamii na kimazingira.

Eko (2010) anabainisha kuwa tangu mwanzo mwa miaka ya 1990, vikatuni vimeongoza mapambano ya uhuru wa kujieleza Barani Afrika. Mtafiti huyo alichambua sampuli za kimakusudi za vikatuni kutoka nchi zenye mapambano makubwa kati ya serikali na vyombo vya habari. Utafiti huo ulibaini kwamba vikatuni vya kisiasa vya Kiafrika husheheni mazungumzo ya upinzani yasiyo na heshima. Pia vikatuni hivi hutumia semi na hadithi za Kiafrika kuonyesha taswira ya huzuni kuhusu hali ya vyombo vya habari barani Afrika. Aidha, mbinu moja ambayo vikatuni vimetumia kukemea uongozi wa kimabavu ni kwa kuangazia ukandamizaji wa kisiasa dhidi ya vyombo vya habari. Wanaobuni vikatuni wako mstari wa mbele katika upinzani dhidi ya matumizi mabaya ya madaraka na ukiukaji wa haki za binadamu barani Afrika. Ingawa Eko (keshatajwa) anatoa uchambuzi wa kina kuhusu vyombo vya habari vya Afrika kupitia vikatuni vya kisiasa, mchango wake katika masuala ibuka ni mdogo; pengo lililozibwa na utafiti huu.

Zaidi ya hayo, uwezo wa vikatuni wa kuhifadhi na kuendeleza masuala katika jamii umekuwa muhimu katika kuharakisha uelewa juu ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa. Motswaledi (2022) anasema kuwa vikatuni hurahisisha uelewa wa mazingira kwa kuonyesha matatizo ya kimazingira kama vile uchafuzi wa mazingira, ukataji miti, na hali mbaya ya hewa kwa njia inayovutia na kueleweka. Kwa njia hii, ni wazi kwamba vikatuni vya kisiasa vinaunda sehemu muhimu ya vyombo vya habari vinavyotoa taarifa, kuhifadhi, na kuangazia maovu ya kijamii. Utafiti wa Motswaledi ulionyesha jinsi vikatuni viliweza kurahisisha masuala magumu kama mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutumia picha zenye mvuto na ujumbe rahisi kueleweka. Motswaledi (2022) alifanya utafiti kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa ambayo ni suala ibuka bali utafiti huu uliangazia masuala ibuka kwa jumla kama vile elimu ya kidijitali, ulinzi wa watoto pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Pia, vikatuni hufanikisha mabadiliko katika jamii kama inavyodhihirika katika utafiti wa Ikoro (2022). Mtafiti huyu alijikita katika sampuli ishirini za vikatuni kuanzia Agosti 1 hadi 11, 2021, kule Nigeria. Utafiti ulibaini kuwa wanaobuni vikatuni huvitumia kutoa maoni kwa siri juu ya masuala ya sasa kwa njia ya kejeli. Hii huweka wazi maovu ya kijamii kwa lengo la kuyarekebisha. Wanaobuni vikatuni huonyesha uzito wa mzigo unaotokana na maovu hayo, kama vile ufisadi kwa taifa la Nigeria. Vikatuni vina jukumu juu ya maoni ya umma kwa kupunguza ugumu wa kuelewa mambo ya kijamii ili kuleta mabadiliko, pale panapohitajika. Aidha, katika jamii yenye kiwango kikubwa cha watu wasio na elimu, vikatuni vinaweza kufanikisha mawasiliano kwani vikatuni hueleweka kwa urahisi kwa wale wenye elimu ya kiwango cha chini. Kwa kuwa vikatuni hupendwa na watoto, Ikoro alidhihirisha kuwa dunia inabadilika haraka na watoto wanahitaji njia ya kuelewa mabadiliko hayo. Hivyo, vikatuni vinakidhi mahitaji haya kwa uwezo wao wa kubadilika ili kuakisi hali halisi katika jamii.

### 2.4 Mbinu Katika Kazi Za Fasihi

Katika fasihi, lugha hutumika kueleza uzoefu wa binadamu kupitia mbinu mbalimbali (Mega, 2024). Mbinu za fasihi ni njia za kimakusudi na za kistadi zinazotumiwa na waandishi ili kuboresha muundo, maana, na uzuri wa maandishi. Ni vipengele vya msingi vya fasihi vinavyotumika kuwasilisha mawazo changamano, kuchochea hisia, na kuwashirikisha wasomaji kwa kiwango cha juu cha kiakili na kiubunifu. Mara nyingi, watunzi hutumia mbinu ya masimulizi, lugha ya taswira, nyimbo na majazi. Mbinu hizi zinaweza kuathiri jinsi simulizi linavyotafsiriwa na kueleweka. Hivyo, huunda tafsiri ya msomaji na uhusiano wake na maandishi. Ustadi wa mbinu za fasihi huwapa waandishi uwezo wa kudhibiti umbo na maudhui ili kufanikisha kazi ya sanaa yenye malengo maalum.

Utafiti wa Ochenja (2008) kuhusu maigizo kama mbinu ya kukuza maudhui katika riwaya za Ken Walibora; *Ndoto ya Amerika* na *Kufa Kuzikana* ulibaini kuwa mwandishi alitumia mbinu za maigizo zilizofanya kazi yake kuonekana kama tamthilia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mseto za Uigizaji na Uhalisia kwa kuwa riwaya hizi huakisi mambo halisi katika jamii. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa mwandishi alishirikisha wahusika wake katika matendo na kusema badala ya kusema pekee.

Matendo ya wahusika huandamana na mazungumzo. Vilevile, ili kufanya riwaya kuonekana kama tamthiliya, wahusika wa Ken Walibora wanawasiliana kwa kutumia hali iliyopo, hali inayofanya masimulizi kuwa na uhai na kuonekana kama maigizo. Isitoshe, utafiti ulibainisha kuwa kuna matumizi ya mabadiliko ya mandhari ili kujenga taswira ya uigizaji. Riwaya hizi zinaleta maandhari ya shule, sokoni, mahakamani na kituo cha polisi. Utafiti wa Ochenja (2008) ulifanya uchambuzi wa riwaya za watu wazima ila utafiti huu ulijikita katika vikatuni vya *Ubongo Kids* vinavyotumia mbinu kama vile vichekesho ili kuelimisha kuhusiana na masuala ibuka.

Herman (2012) anasema kuwa fasihi ina jukumu la kuwasilisha sanaa ya lugha ili kufikisha ujumbe wake katika jamii. Iwapo kuna uwasilishaji wowote utakaofanyika bila matumizi ya kisanaa, basi fasihi hukosekana. Ili ujumbe unaolengwa ufikie kundi lengwa katika jamii, hasa watoto, mipaka ya uhalisia huweza kuvukwa kwa kuhusisha mambo ya kifantasia kwa maksudi. Fantasia ina nafasi kubwa katika fasihi ya watoto. Kwa mfano, fantasia hutumika kujenga msuko wa matukio kwenye hadithi, kujenga taharuki kwa watazamaji au wasikilizaji, kuibua mgogoro na kuibua dhamira katika kazi husika. Vilevile, fantasia katika vikatuni hutumika kujenga mandhari ya kazi, kando na kuvuta usikivu wa hadhira. Kama Herman (2012) anavyosema, fasihi inapaswa kutumia sanaa ya lugha kufikisha ujumbe. Fantasia ni mojawapo ya mbinu hizo za kisanaa na huwafanya waone mambo magumu kwa njia rahisi na ya kufurahisha. Ingawa Herman anaeleza mbinu moja tu ya uwasilishaji katika kazi za kifasihi, utafiti huu ulijikita katika mbinu zaidi ya moja.

Mutua na Furaha (2014) walichunguza fantasia kama mbinu ya kutunga hadithi ya watoto. Utafiti huu ulitumia Nadharia ya Fantasia ya Bormann inayoshikilia kuwa maana zitokanazo na ishara kwenye fantasia huleta ushirikiano na utangamano. Kutokana na utafiti huu, fantasia huwa na vipengele mbalimbali vya kifasihi kama vile msuko, lugha, maudhui, wahusika, na mandhari. Wahusika katika kazi za kifantasia, kama vile wanyama, huwa na sifa za kibinadamu, ikiwemo kuwaza, kupigania haki zao, na kuzungumza. Wahusika hawa hupewa majukumu tofauti. Mhusika mkuu mmoja huwa na jukumu la kuchunguza na anatarajiwa kutoa suluhu kwa matatizo yanayozuka katika usimulizi. Utafiti wa Mutua na Furaha ulijikita katika mbinu moja ya uwasilishaji

katika fasihi. Tofauti na utafiti wao, utafiti huu ulinuia kuchambua mbinu zaidi ya moja ili kufanikisha uelewa wa malengo ya utafiti.

Utafiti wa Kaula (2015) ulichambua mitindo na lugha kama usemi wa kifasihi katika filamu ya vikatuni vya *Ben 10*. Mojawapo ya matokeo ya utafiti huu ni matumizi ya lugha ya kishujaa inayoakisi ukuaji wa mhusika mkuu kutoka mvulana wa kawaida hadi shujaa mwenye nguvu. Hii inaashiria hadithi ya kiasili inayopatikana katika vikatuni vingi vya watoto, ambapo lugha huonyesha ukuaji wa mhusika. Aidha, utafiti unaonyesha kuwa *Ben 10* inatumia ucheshi, misimu, na lugha ya kawaida ili kuvutia hadhira yake lengwa. Matumizi ya misemo na vipengele vya lugha vinavyorudiwa husaidia watoto kushirikishwa kwenye maudhui hayo na kuwezesha kujifunza lugha kupitia marudio. Kwa kuchambua vikatuni vya *Ben 10*, Kaula aliangazia masuala ibuka kama vile jinsi vyombo vya habari vinaweza kuathiri ukuzaji wa lugha kwa watoto, uundaji wa utambulisho na tabia za kijamii. Kaula alijikita katika uchanganuzi wa lugha na mbinu za kisanaa katika vikatuni, kwa lengo la kuangazia matumizi ya sanaa ya lugha katika kazi hizo. Tofauti, utafiti huu ulitumia mbinu za kifasihi kwa mtazamo unaolenga kuchunguza jinsi masuala ibuka yanavyowasilishwa katika vipindi vya *Ubongo Kids*.

Mose na Obuchi (2021) walifanya utafiti kuhusu kikale cha kifo kama mbinu inayotumiwa katika fasihi ya Kiswahili na kubaini kuwa kifo kinatumika mara nyingi katika tamthilia. Matumizi ya kifo huimarisha dhamira na ujumi wa watunzi wa kazi za fasihi. Kifo hutumika kama taashira tangu jadi na hujitokeza katika kazi za kisanaa kwa njia ya kujirudiarudia. Dhana ya kujirudiarudia inaweza kulinganishwa na motifu ya utunzi wa kazi za kifasihi zilizo na uwezo wa kuathiri muundo pamoja na dhamira ya kazi husika. Chanzo cha kifo katika kazi yoyote ile ya kifasihi huwa ni uhalifu au dhambi ya mhusika ambaye huteseka na mateso hayo huandamana na uchungu mwingi. Hata hivyo, matumizi ya kifo katika kazi za watoto ni swala nyeti linalohitaji umakinifu ili kuleta usawa kati ya elimu na burudani. Mbinu ya kifo inaposhughulikiwa ipasavyo, inaweza kuwafundisha watoto wadogo kuhusu mambo muhimu ya maisha kama huzuni. Mose na Obuchi (2021) walionyesha kuwa kifo huathiri muundo na dhamira ya kazi. Hata hivyo, vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* vinatumia vichekesho, picha za rangi, na wahusika wa kubuniwa ili kuwasilisha elimu burudani.

Dimbu (2021) aliangazia uchanganuzi makinifu wa diskosi katika vikatuni vya *Shujaaz.* Utafiti huu ulibaini kuwa muwala katika vikatuni hukuzwa na mada, sauti za kionomatopeya, maandishi kwenye paneli, maelezo ya mwandishi pamoja na uzungumzi nafsi. Wahusika pia walichangia katika kuwasilisha mahusiano ya uwezo. Kwa kuwa watoto hufurahia vikatuni na hujifunza kutokana na kile wanachotazama, maudhui, lugha na mbinu za uzalishaji wa vikatuni, vikatuni hivi vina uwezo wa kuathiri mtazamo wao kuhusu ulimwengu na jinsi wanavyothamini mambo. Pasipo kutambua, watoto hutafsiri wanachotazama na mawazo na matendo yao hufuata mifumo ya ujumbe wa vikatuni hivi. Watoto wanapotazama vikatuni ambavyo huonyesha kundi moja likiwa bora kuliko lingine, uwakilishi huo hujengwa ndani yao aidha kwa kujua au bila kujua, na huanza kuwa na mtazamo huo juu ya maisha. Hali hii huathiri mitazamo yao kuhusu maisha. Utafiti wa Dimbu (2021) ulitumia uchanganuzi makinifu wa diskosi, akiangazia lugha, maandishi, sauti na nafasi ya wahusika katika kujenga maana na uhusiano wa mamlaka katika *Shujaaz*, utafiti huu ulifanyika katika muktadha wa maudhui ya kijamii na kimazingira na mbinu za elimu burudani kama vile nyimbo, vichekesho na picha katika vipindi vya *Ubongo Kids*.

Madoshi (2022) alichunguza matumizi ya mbinu za fasihi simulizi katika nyimbo za injili kwa kuegemea wimbo wa Bahati Bukuku unaoitwa "Kampeni". Mtafiti alitumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo katika ufafanuzi wa matini. Mtafiti alibaini kuwa wimbo huo umetumia mbinu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile majigambo, chuku pamoja na kejeli inayojitokeza kupitia picha jongefu. Wimbo wenyewe pia ulitawaliwa na usimulizi unaotumia injili. Wimbo pia una matumizi ya mandhari ya kibunilizi kama vile ya duniani, jahanamu na mbinguni. Kupitia ruhusa ya fanani, wahusika walitokea kama vionwa katika picha jongefu ila maneno yanasemwa na msimuliaji. Kupitia utafiti wa Madoshi, ni wazi kuwa nyimbo zina uwezo wa kuathiri hadhira kupitia mbinu mbalimbali za kifasihi. Utafiti wa Madoshi ulijikita katika matumizi ya mbinu ya fasihi simulizi katika nyimbo za injili kwa kuegemea wimbo wa Bahati Bukuku unaoitwa "Kampeni". Hii ilikuwa tofauti na utafiti huu uliojikita katika mbinu mbalimbali ili kufanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Hata hivyo, utafiti wa Madoshi ulifaidi utafiti huu kueleza jinsi wimbo unavyoweza kutumika kuathiri hadhira kupitia mandhari ya kibunilizi.

Msangi (2023) alifanya uchambuzi wa mbinu za Kiaristotle na zisizo za Kiaristotle katika tamthilia ya *Sadaka* ya John Okello. Nadharia ya Kiaristotle mara nyingi hutumika katika uhakiki wa tamthilia yenye miundo ya tanzia inayoonyesha kushindwa au kuanguka kwa mhusika maarufu. Ukusanyaji wa data ulitumia mbinu ya usomaji makini huku uwasilishaji wa data ukitumia maelezo. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa mbinu za Kiaristotle zilijitokeza kupitia dayolojia, msuko na wahusika ambao ni viumbe wabebao mvutano. Pia, mbinu hizi zilijitokeza kupitia dhamira pamoja na uteuzi wa msamiati. Kwa upande mwingine, mbinu ambazo siyo za Kiaristotle zilijitokeza kupitia monolojia, dayalojia na pia kuchanganya nathari na matumizi ya nyimbo na lugha ya kishairi. Uchambuzi wa Msangi ulizingatia mbinu za Kiaristotle na zisizo za Kiaristotle katika tamthilia inayolenga watu wazima, tofauti na utafiti huu uliotumikiza mbinu za kifasihi kubainisha jinsi zinavyotumika kufanikisha masuala ibuka kwa watoto kupitia vipindi vya *Ubongo Kids*.

Ali na wenzake (2024) walichunguza vikatuni vya *Masha and the Bear*. Utafiti huu ulitathmini maudhui ya vikatuni hivyo pamoja na matumizi ya tamathali za usemi katika mazungumzo ya wahusika. Utafiti huu ulifuata muundo wa kimaelezo wa kidhahania, ambapo maudhui teule yalichambuliwa kwa kutumia uchanganuzi wa msamiati. Uchanganuzi huu ulijumuisha uchanganuzi wa maana, ulinganifu wa msamiati, mabadiliko wa msamiati, ulinganifu wa maana na mkengeuko wa maana. Matokeo yalionyesha kuwa kuna matumizi ya mbinu mbalimbali kama vile mazungumzo inayotumia lugha sahili ili, kuweza kuwasilisha maadili, kukuza ujifunzaji, na kuchochea ukuaji wa kiakili. Ali na wenzake wanaangazia tamathali za usemi na uchanganuzi wa msamiati na namna unavyotumika kuwasilisha maadili na kukuza ujifunzaji ila utafiti huu ulijikita katika uwasilishaji wa masuala ibuka kama vile mabadiliko ya tabianchi, usawa wa kijinsia na afya kupitia mbinu kama vichekesho, mazungumzo na nyimbo.

Naru na wenzake (2024) wanasema kuwa licha ya vikatuni kuwa na mwonekano wa kuchekesha, mara nyingi hutegemea mbinu mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe, kuburudisha, na kuvutia hadhira. Mbinu hizi husaidia kuunda uelewa wa mtazamaji kuhusu wahusika, mandhari, na ploti kwa njia yenye kina na hila. Baadhi ya mbinu zinazotumiwa ni sitiari, kejeli, na uhuishaji. Kuwa na uwezo wa kutambua mbinu hizi

katika vikatuni kunahitaji umakinifu juu ya jinsi lugha, taswira, na muundo wa simulizi vinavyoingiliana. Matumizi ya mbinu hizi hufanya vikatuni kuwa njia bora ya usimulizi wa hadithi, huku vikiwaruhusu waandishi kuchunguza mada changamano kama vile urafiki, utambulisho, na uhalisia wa maisha ya kila siku. Kupitia ucheshi na ubunifu katika mazungumzo, vikatuni huvutia hadhira na kuunda uhusiano wa kudumu kwa vizazi mbalimbali. Ingawa utafiti wa Naru na wenzake ulitathmini vikatuni kama sanaa ya usimulizi, utafiti huu ulichambua vikatuni kama zana ya elimu ya watoto.

### 2.5 Usawiri wa Wahusika Katika Kazi za Kubuni

Madumulla (2009) anafafanua wahusika kama viumbe au vitu vinavyotumiwa na msanii katika kuwasilisha ujumbe wake katika hadhira. Wahusika huweza kuwa mtu, miti, ndege au majini. Katika kazi yoyoye ya kisanii, usawiri wa wahusika huwa muhimu. Kupitia usawiri huu, fikra, hisia na msimamo wa msanii huonekana wazi. Wahusika ndio kiini cha kazi ya msanii. Kwa upande wake Ilomo (2017), anasema kuwa wahusika huwa na nafasi kubwa katika ujenzi wa kazi yoyote ya fasihi. Hali hii inatokana na ukweli kuwa wahusika wana uwezo wa kuathiri simulizi inayosimuliwa. Katika hali ya kawaida, wahusika siyo watu wa kawaida bali ni wa kubuniwa ili kuafikiana na malengo ya kazi za kiubunifu.

Utafiti wa Scott (2007) ulichunguza jinsi vikatuni vilitumika kama chombo cha propaganda wakati wa matukio muhimu ya kihistoria. Utafiti wa Scott unachambua jinsi uaminifu, uzalendo, na wahusika wa nguvu zisizo za kawaida, kama vile *The Shield* na *G-Man Extraordinary*, walivyowasilishwa katika muktadha wa utambulisho wa Marekani. Pia, Scott anajadili jinsi vikatuni vilivyojibu mashambulizi ya 9/11, ikiwemo uamuzi wa *Marvel Comic Books* kuandika upya *The Amazing Spider-Man #36* ili kushughulikia hisia zinazohusiana na tukio hilo. Wakati Scott anajikita zaidi katika uzalendo na siasa, wahusika katika vipindi vya *Ubongo Kids* hushirikisha watazamaji na kuwafanya wawe na uwezo wa kuelewa na kutafakari juu ya masuala ibuka kupitia elimu burudani.

Ahmed na Wahab (2014) walichunguza vikatuni kumi vilivyoonyeshwa kwenye *Cartoon Network* (CN). Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza jinsi wahusika wa kike na wa kiume walivyowakilishwa kwa misingi ya kijinsia. Matokeo ya utafiti

yalionyesha kuwa vikatuni vilivyotazamwa vilikuwa vinalenga zaidi jinsia ya kiume, na kulikuwa na vichache vilivyolenga jinsia ya kike. Aidha, wahusika wa kiume walionyeshwa kuwa wenye nguvu, wenye misuli, na wanaotawala. Kinyume chake, wahusika wa kike walionyeshwa kuwa wanyonge, wasio na nguvu na wenye kuvutia. Utafiti huo ulionyesha kuwa uwakilishi usio sahihi unaweza kutoa ujumbe hasi wa kupotosha kuhusu majukumu na uwakilishi wa kijinsia kwa watoto wengi katika jamii. Utafiti ulipendekeza matumizi ya vikatuni kama vyombo vya kuwasilisha picha zisizo na upendeleo za wahusika wa kike na wa kiume kwa watoto wakiwa na umri mdogo kutokana na uwezo wa vikatuni kuvutia hisia zao. Ahmed na Wahab walionyesha mtazamo wa kijinsia unaopendelea upande mmoja ila utafiti huu ulibaini kuwa wahusika wamesawiriwa kwa njia tofauti, shirikishi na sawa, wakikumbana na matatizo ya kijamii kisha kuyatatua kwa usaidizi wa elimu na ubunifu.

Muge (2015) anaeleza kuwa kile kinachofanya vipindi vya vikatuni kuvutia ni wahusika wake. Wahusika katika vikatuni ni wanyama, binadamu na wahusika wa kufikiriwa tu. Wahusika binadamu na wanyama ni mifano kutoka kwa maisha ya kila siku. Mafanikio ya wahusika katika vikatuni huhusishwa na uwezo wao wa kuonyesha sifa za binadamu, kutoa utambulisho na kushiriki hisia sawa. Hivyo, usawiri wa wahusika ulieleza hali halisi katika jamii, vyanzo vya matatizo, na jinsi wahusika katika kazi za kubuni wanavyoeleza mienendo ya binadamu wa kawaida. Muge anaonyesha kuwa wahusika huburudisha huku wakieleza maisha ya kila siku kupitia usawiri wao. Utafiti huu ulibaini kuwa vikatuni kwenye vipindi vya *Ubongo Kids* hushirikisha watazamaji kupitia burudani na kuwafanya wawe na uwezo wa kuelewa na kutafakari juu ya masuala ibuka. Utafiti wa Muge (keshatajwa) ulimfaidi mtafiti kuelewa jinsi wahusika huakisi hali halisi katika vikatuni na kuendeleza mienendo ya binadamu.

Njiiri na wenzake (2018) waliibua mjadala kuhusu athari za ushawishi wa vipindi vya kigeni vya vikatuni, hasa ikizingatiwa kwamba vikatuni vya kigeni vinaakisi tamaduni tofauti na zile zinazoshikiliwa na jamii za Kenya. Watafiti hawa waneleza kuwa watoto wana uwezo wa kujitambulisha na wahusika wa kishujaa katika vikatuni. Jambo hili linaweza kuwafanya watoto kuiga tabia za wahusika hao. Mashujaa katika vikatuni wana ushawishi mkubwa kwa watoto ambao karibu kila wakati hujaribu kucheza nafasi za mashujaa hao katika ulimwengu halisi. Hata hivyo, uwasilishaji wa vurugu, ubaguzi

wa kijinsia, na mafunzo tata ya kimaadili katika vikatuni vya kigeni unatofautiana pakubwa na matarajio ya kitamaduni ya Wakenya kuhusu upatanisho wa kijamii, heshima, na usawa wa kijinsia. Tofauti na utafiti wa Njiri na wenzake ulioangazia athari za vikatuni vya kigeni kwenye tabia za watoto Wakenya, utafiti huu ulijikita katika ufanikishaji wa masuala ibuka kwenye vipindi vya watoto kupitia elimu burudani. Utafiti wa Njiiri na wenzake ulimnufaisha mtafiti kueleza athari ya wahusika kwa watazamaji wake.

Wangui (2019) alifanya utafiti kuhusu ushawishi wa vipindi vya vikatuni vya televisheni vya kigeni juu ya tabia ya kijamii ya watoto nchini Kenya. Mtafiti alitumia sampuli za kimakusudi. Shule za binafsi pekee katika Wadi ya Township zilijumuishwa katika utafiti huu. Hii ilifanywa kwa sababu maeneo mengi ya Wadi hii yana miundombinu ya umeme, hali iliyowezesha utekelezaji wa masuala yaliyolengwa katika utafiti. Utafiti ulibaini kuwa wahusika katika vikatuni vya televisheni wanaathiri tabia za kijamii za watoto. Pia, mchango wa dhana potofu kuhusu jinsia katika uundaji wa mitazamo miongoni mwa watoto ulibainika. Watoto walionyesha kwamba walijihusisha sana na wahusika maarufu wa kishujaa huku wakijaribu kuwaiga kwa kujaribu kuzungumza, kutenda, na kuvaa kama wao. Watoto wengine waliomba wanunuliwe vifaa vyenye mandhari ya vikatuni kama vile nguo, vifaa vya kuandikia, na mikoba ya shule. Utafiti wa Wangui ulionyesha mabadiliko katika upendeleo wa watoto kutoka kwa fasihi ya jadi ya kuchapisha hadi kwa filamu na maudhui ya vikatuni. Mabadiliko haya yanaonyesha mwenendo mpana jinsi vyombo vya habari vya kidijitali vinabadilisha ushiriki wa watoto na maudhui ya elimu na burudani. Tofauti na utafiti wa Wangui anaohimiza hali ya wasiwasi juu ya jinsi vyombo vya habari vya kimataifa vinavyoathiri utambulisho wa watoto, utafiti huu uliangazia vipindi vya *Ubongo Kids* vinavyonuia kukuza elimu kuhusu masuala ibuka kupitia burudani kwenye vipindi vya watoto.

Abdalla (2020) alifanya utafiti kuhusu uhusika wa kitoto katika vibonzo jongevu kwa kuangazia *Ubongo Kids*, *The Adventures of Abne*y *and Teak* na *Dora the Explorer*. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ule wa Mwitiko wa Msikilizaji. Mtafiti alibaini kuwa watunzi wa vibonzo jongevu hutumia mbinu anuwai katika utungaji wa kazi zao. Baadhi ya mbinu zinazotumika ni wahusika watoto, matendo ya kitoto, rangi

yenye mvuto, kuchanganya wahusika pamoja na motifu za kitoto. Abdalla (keshatajwa) alitumia nadharia ya mwitiko wa msikilizaji ila utafiti huu ulitumia nadharia ya Elimu Burudani ili kuchunguza namna ambavyo wahusika katika vikatuni vya *Ubongo Kids* wanavyosawiriwa katika uwasilishaji wa masuala ibuka.

Kenduiya na wenzake (2020) waliangazia jinsi wahusika wa kimazingaombwe wanavyowasilishwa na kuhusika katika kazi za Kiswahili. Uchambuzi huu unazingatia misingi ya nadharia ya Umazingaombwe. Riwaya za *Babu Alipofufuka* na *Watu wa Gehenna* zilichaguliwa kwa makusudi. Hii ni kwa sababu kazi hizo huwasilisha wahusika kwa mbinu za kuvutia na za kifantasia, ambazo hujenga dhamira ya kimazingaombwe. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa wanaobuni kazi za kimazingaombwe hutumia mbinu za uhusika ambazo zina ubinafsi wa kipekee, ikitegemea ubunifu wa kila msanii wa kimazingaombwe. Tofauti na utafiti wa Kenduiya na wenzake ulioangazia uwasilishaji wa wahusika wa kimazingaombwe katika kazi za fasihi ya Kiswahili, utafiti huu ulijikita katika kuonyesha mbinu za elimu burudani kufanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka kwa watoto katika vipindi vya *Ubongo Kids*.

Burundi na wenzake (2024) walichunguza uhusika katika fasihi bulibuli ya Kiswahili kwa kuegemea utenzi wa Mikidadi na Mayasa na kubaini kuwa msanii huteua wahusika ili kuweza kukuza na kuwasilisha maudhui husika. Wanasema kuwa wahusika hushabihiana na watu kwa sababu huandikwa kwa minajili ya watu. Pia, wahusika huakisi masuala yanayohusu wanajamii na yanayokusudiwa kubainishwa, kujadiliwa, na kutatuliwa na wanajamii wenyewe. Wahusika si watu wa ukweli bali huwa wa kubuni ambao hupewa sifa zao kutokana na lengo la mtunzi. Kutokana na ubunifu wa msanii, wahusika wa aina mbalimbali huweza kusawiriwa ili kuashiria sifa na tabia katika jamii husika. Pia wahusika husawiriwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo, mbinu ya mazungumzo, mbinu ya majigambo, mbinu ya motifu ya safari na mbinu ya matendo. Wahusika wanatumika kama kiunzi muhimu cha kuwasilisha maudhui. Utafiti huu ulionyesha kuwa fasihi ya Kiswahili inatumia wahusika kwa urahisi na ubunifu ili kuakisi jamii. Ingawa Burundi na wenzake walinuia kuonyesha jinsi wahusika wa kubuni wanaweza kutumika kuakisi tabia na mienendo ya kijamii kupitia mbinu bunilizi za kifasihi kama vile majigambo, utafiti huu ulilenga kuonyesha jinsi

wahusika wanafanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka kupitia elimu burudani kwenye vipindi vya watoto.

Prithviraj na wenzake (2024) walieleza kuwa watoto kuvutiwa na wahusika kwenye vikatuni kunakuza vipengele mbalimbali vya ukuaji wao, ikijumuisha ubunifu, msamiati, ujuzi wa kuandika, lugha, na uwezo wa kiakili. Kwanza, wahusika kwenye vikatuni huwa chanzo kikubwa cha msukumo kwa watoto, na kuchochea ubunifu wao. Kupitia matukio ya kubuni na kufikirika yanayoonyeshwa na wahusika, watoto huhimizwa kuchunguza na kuunda hadithi zao, jambo linalokuza ubunifu tangu utotoni. Michezo hii ya kufikirika inaweza kuchangia kuimarika kwa ujuzi wa kutatua changamoto na uwezo wa kufikiria kwa njia isiyo ya kawaida. Pia, vikatuni mara nyingi hutumiwa kubuni maneno mapya, misemo, na dhana kwa watazamaji wachanga, hivyo kupanua misamiati yao. Hata hivyo, Prithviraj na wenzake walionya kuwa kuna changamoto zinazoweza kutokea kwa kutegemea vikatuni kupita kiasi kama chanzo kikuu cha burudani. Kutazama vikatuni vinavyohusu vurugu huweza kuchangia kuongezeka kwa tabia za ukali miongoni mwa watoto kwani wanaweza kuiga vitendo vya vurugu vinavyoonyeshwa. Tofauti na utafiti wa Prithviraj na wenzake uliotafiti kuhusu jinsi wahusika huchochea ubunifu, huendeleza lugha na huwafanya watoto kuiga sifa zao, utafiti huu ulilenga kuonyesha jinsi wahusika hushirikisha watazamaji, huonyesha hali halisi ya maisha, hutatua changamoto, huhamasisha na kuelimisha kuhusu masuala ibuka kwenye vipindi vya watoto.

### 2.6 Kiunzi Cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Elimu Burudani inayohusisha kutumia burudani kwa lengo la kuelimisha au kushawishi hadhira (Sharma, 2023). Nadharia hii ilianzishwa na Miguel Sabido (2003) wakati ambapo kulitokea mafanikio ya telenovela ya *Simplemente Maria (Simply Mary).* Hii ni telenovela iliyohusu maisha ya mwanamke wa kijijini ambaye anahamia mjini na kuwa mjakazi kisha baadaye kufanikiwa kutokana na bidii masomoni na maishani (Singhal na wenzake, 1995). Hivyo, Sabido (2003) alitumia ujuzi wake wa uelekezi na ukurugenzi katika televisheni kujaribu kuelezea jambo hili la kufanikiwa kwa telenovela ya *Simplemente Maria (Simply Mary)* mwaka wa 1970. Aliegemea nadharia mbalimbali za mawasiliano na tabia, akichanganya vipengele kutoka kwa Albert Bandura, Eric Bentley, Carl Jung, na

Paul MacLean. Sabido (2003) alikuwa na jukumu muhimu katika kuibua Elimu Burudani kama uwanja wa kimataifa wa utafiti na utendaji. Kwa kuegemea nadharia ya utambuzi wa kijamii ya Albert Bandura, Sabido anawaona watu kama mawakala hai walio na uwezo wa kuathiriwa au kuathiri mazingira yao. Watu wanaweza kujifunza tabia zinazofaa na zisizofaa kupitia uchunguzi.

Muundo wa hadithi au simulizi unaweza kusaidia kuchochea mabadiliko kwa hadhira kwa kuonyesha wahusika wema wanaozawadiwa na wahusika wabaya wanaoadhibiwa (Sabido 2003). Elimu Burudani inaweza kuwa na ufanisi hasa wakati watu wanatazama kipindi na kujihisi kama mmoja wa wahusika. Wakati watazamaji wanaelewa na kufurahishwa na hadithi fulani, kuna uwezekano wa kushawishika na kutetea msimamo fulani. Pia, mtazamaji anapojitambulisha na mhusika maalum, huchukua mtazamo wa mhusika huyo na kushawishika kwa urahisi.

Vipengele muhimu katika Elimu Burudani ni kama vile kutumia burudani kwa lengo la kuelimisha na kushawishi hadhira, kuhimiza ushirikiano kati ya watendaji wa vyombo vya habari na mawakala wa mabadiliko na kutegemea utafiti (Brown, 2017). Pia, hadithi, wahusika, na ploti hushirikisha watazamaji. Hii huwafanya wawe na uwezo mkubwa wa kuelewa na kutafakari juu ya maudhui ya elimu. Nadharia ya Elimu Burudani inahimiza wasikilizaji au watazamaji kufikiri kwa kina juu ya masuala yaliyowasilishwa na hivyo kusababisha uelewa bora. Isitoshe, kuwatazama wahusika wakifanikiwa kutokana na masuala fulani yanayowakumba huongeza imani ya watazamaji katika uwezo wao wa kufikia matokeo sawa. Hata hivyo, ujumbe wa elimu hujumuishwa katika maudhui ya burudani bila kuathiri kipengele chochote. Kwa kutumia vipengele hivi, Elimu Burudani inalenga kuunda maudhui ya kuvutia watazamaji kando na kukuza mabadiliko mazuri ya kijamii na tabia.

Aidha, mbinu inayotumika kufanikisha burudani hutegemea mitindo mbalimbali kama vile matumizi ya muziki, filamu, picha na michezo kwa lengo la kupunguza uchovu. Wanaobuni vipindi vya burudani hujitahidi ili wanaoshiriki wajifunze kupitia mtindo usio rasmi.

Mihimili katika nadharia ya Elimu Burudani kulingana na Sabido (2003) ni kama ifuatayo:

i. Wahusika kwenye hadithi pamoja na ploti hushirikisha watazamaji, na kuwafanya wawe na uwezo wa kuelewa na kutafakari kuhusu maudhui ya elimu. Kuona wahusika wakifanikiwa huongeza imani ya watazamaji katika uwezo wao wa kufikia matokeo sawa.
ii. Burudani inategemea sana nadharia ya Utambuzi wa Kijamii ya Bandura, ambayo inapendekeza kuwa watu hujifunza kwa kutazama wanachofanya wengine, hasa wanapoona wengine wakizawadiwa au kuadhibiwa kwa tabia fulani.
iii. Kuna mbinu mbalimbali katika kufanikisha elimu ndani ya burudani kama vile matumizi ya muziki, filamu, picha na michezo kwa lengo la kupunguza uchovu.
iv. Elimu Burudani hufanikiwa inapohusiana na utamaduni ya kundi lengwa. Maudhui kwenye kazi yoyote huandamana na maadili ya kitamaduni, imani, na uzoefu wa kila siku ya hadhira.
v. Elimu Burudani inatambua kuwa mabadiliko ya kijamii na kitabia huhitaji muda na kwa hivyo ni mchakato wa kuendeshwa polepole. Ujumbe wenye elimu mara nyingi huchukua muda mrefu na hujumuishwa kwenye vipindi vingi ili kuwapa watazamaji muda wa kutosha wa kutafakari na kukubali mienendo mipya.
vi. Mipango ya elimu ya burudani mara nyingi inajumuisha vipengele vya ushirikiano vinavyowaruhusu watazamaji kushiriki kikamilifu na kuelewa maudhui kwenye kazi husika. Hii inaweza kujumuisha mijadala au ushirikiano wa mitandao ya kijamii.

Kutokana na maelezo haya, utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo:

Kwanza, kuwa burudani hutumika kwa lengo la kuelimisha na kushawishi hadhira. Kwa kutumia mhimili huu kwa vikatuni vya *Ubongo Kids,* mtafiti alionyesha jinsi vikatuni vinaweza kurahisisha kujifunza masuala ibuka kupitia burudani. Pili, kuna mbinu mbalimbali katika kufanikisha elimu burudani. Mhimili huu ulimfaidi mtafiti kuelewa mbinu wanazotumia wanaobuni vikatuni vya *Ubongo Kids* kufanikisha elimu.

Mwisho, wahusika kwenye hadithi hushirikisha watazamaji, na kuwafanya wawe na uwezo wa kuelewa na kutafakari juu ya maudhui ya elimu. Pia kwa kuwatazama

wahusika wakifanikiwa kutokana na masuala fulani yanayowakumba huongeza imani ya watazamaji katika uwezo wao wa kufikia matokeo sawa. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kufahamu jinsi wahusika katika vikatuni vya *Ubongo Kids* wanasawiriwa ili kufanikisha uwasilishaji wa masuala yanayowakumba wahusika mbalimbali.

Hivyo, mihimili hii ilifaa utafiti huu kwa sababu ilimsaidia mtafiti kujadili masuala ibuka yanayowasilishwa katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Pia, mtafiti aliweza kubainisha mbinu zinazotumiwa kuwasilisha masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Mwisho, mtafiti aliweza kuchunguza jinsi usawiri wa wahusika unavyofanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Sura inayofuata inaangazia mbinu zilizotumika katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii iliangazia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti. Sehemu hii ilishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo na maadili ya utafiti.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo uliotumiwa katika utafiti huu ni wa kimaelezo. Muundo huu ulimsaidia mtafiti kukusanya na kuchambua data huku, akihakikisha kuna udhabiti, uaminifu na uhalali katika utafiti mzima (Orodho, 2003). Muundo huu pia ulimwezesha mtafiti kueleza na kuchambua data kulingana na malengo ya utafiti. Data za utafiti huu ilikuwa video kutoka *YouTube* ambazo mtafiti alikusanya na kuchunguza ili kuchanganuliwa kutoa matokeo.

## 3.3 Eneo La Utafiti

Data ya kimsingi katika utafiti huu ilitolewa kwenye mtandao wa *YouTube*. Mtafiti alichagua mtandao wa *YouTube* kimakusudi kwa sababu vipindi vya *Ubongo Kids* hupakuliwa pale. Hili lilifanikisha kunakili data kwa sababu mtandao wa *YouTube* una vifaa vilivyomwezesha mtafiti kurejesha nyuzi nyuma pamoja na kupunguza kasi ya matukio.  Kando na video kutoka kwenye mtandao huu, kazi nyingine inayohusiana na vikatuni pamoja na masuala ibuka kama vile tasnifu na vitabu vilisomwa na kuchanganuliwa.

## 3.4 Uteuzi wa Sampuli

Mbinu ya usampulishaji iliyotumiwa ilikuwa ya mbinu ya usampulishaji kimaksudi. Mbinu hii humruhusu mtafiti kuamua kwa hiari yake kundi la vitu anavyoamini vinaweza kumpa data inayoweza kufanikisha malengo ya utafiti wake (Palys, 2008). Aidha, kwa sababu ya kina cha uchambuzi kilichohitajika, ilikuwa muhimu kuzingatia sehemu ya sampuli ambayo iliruhusu uchambuzi wa kina. Hivyo, mtafiti alijikita katika vipindi vilivyohusiana na malengo ya utafiti.

Video zilizolengwa na mtafiti zilikuwa mkanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, mtafiti aliteua kimaksudi video 20 kutokana na jumla ya video 200 zinazotumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Kiwango cha sampuli kilichoteuliwa kilikuwa takriban asilimia kumi. Asilimia hii inaafikiana na mawazo ya Mugenda (1999), anayesema kuwa asilimia kumi ya kundi lote ni kiwakilishi tosha cha utabia na sifa za jumla za kundi kubwa linalotafitiwa.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulitumia mbinu ya kiwango kifu katika ukusanyaji wa data. Kulingana na Naeem na wenzake (2024) mbinu ya kiwango kifu hurejelea hatua katika ukusanyaji wa data ambapo hakuna masuala au maarifa mapya yanayobainika, na data huanza kujirudia kiasi kwamba kuendelea kukusanya data hakuzai matokeo mapya, jambo linaloashiria kuwa ukubwa wa sampuli uliokusudiwa umefikiwa. Mbinu hii hujitokeza kama dhana muhimu kwa sababu inasaidia kuhakikisha kwamba matokeo ni dhabiti, na kwamba data zinatumiwa kwa uwezo wao kamili ili kufikia lengo la utafiti. Pia, mbinu hii hutumika kama mwongozo wa kutathmini ikiwa sampuli imetosha.

Data ya kimsingi ilikusanywa kwa kutazama video zilizochaguliwa na mtafiti. Kwa hivyo, mtafiti alitazama video na kurekodi data iliyopangwa katika makundi tofauti kulingana na maswali ya utafiti. Hatua ya kwanza ambayo mtafiti alichukua ni kufafanua masuala maalum yaliyoshughulikiwa kama ilivyoelezwa katika malengo ya utafiti. Mtafiti aliendelea kukusanya data kwa kuchagua vipindi vilivyohusiana moja kwa moja na malengo haya. Hali hii ilihusisha kutazama vipindi hivi kwa makini. Baada ya video hizi kutazamwa kama sehemu ya mchakato wa ukusanyaji wa data, kauli, matendo ya wahusika na visa vilivyoambatana na malengo ya utafiti vilinukuliwa ili kuweza kurahisisha uchunguzi wa kina.

#### 3.5.1 Zana za Utafiti

Mulokozi (1983) anaeleza kuwa aina ya utafiti huamua zana zitakazotumika katika utafiti. Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo, mtafiti alitumia orodha ya ukaguzi kama kifaa cha utafiti. Pia, kompyuta na wavuti zilitumika kupata makala za kitaaluma, vitabu pepe na machapisho ya kitaaluma kupitia majukwaa kama Google Scholar,

ResearchGate na maktaba za vyuo vikuu. Aidha, mtandao wa *YouTube* ulitumika kupata vipindi, video, na taarifa ya moja kwa moja kuhusu malengo ya utafiti huu.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data ilichanganuliwa kwa kupangwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza lilihusu lengo la kwanza ambalo ni kujadili masuala ibuka yaliyowasilishwa katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Uchambuzi huu ulijumuisha maudhui ya vipindi vilivyochaguliwa na ulihusisha kupitia kwa umakini kila kipindi ili kutambua mada kuu au masuala yanayojadiliwa. Kundi la pili lilihusu kubainisha mbinu zilizotumiwa kuwasilisha masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Uchambuzi huu ulizingatia mbinu mbalimbali zilizotumika katika kipindi hiki. Kundi la tatu lilihusu lengo la tatu: kuchunguza jinsi usawiri wa wahusika ulivyofanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids.* Uchambuzi huu ulihusisha kutathmini majukumu na tabia za wahusika, pamoja na mwingiliano wao, ili kuelewa jinsi walivyosaidia kuwasilisha masuala yaliyokusudiwa. Aidha, mihimili ya Nadharia ya Elimu Burudani ilimwongoza mtafiti katika uchanganuzi huu. Kwa kutumia njia ya maelezo, mtafiti alifanikiwa kuchanganua data yake kwa njia wazi.

### 3.7 Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kutumia njia ya maelezo. Uwasilishaji huu ulihusu kufasiri matokeo ya utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Matokeo yaliandaliwa kwa kufuata mada kuu, yakilenga jinsi masuala yaliyolengwa yalivyowasilishwa katika vipindi husika kupitia mbinu za kifasihi kwa usaidizi wa wahusika mbalimbali. Kila sehemu ilikuwa na nukuu kutoka kwenye vipindi zilizotumiwa kuonyesha hoja, pamoja na maelezo ya matukio. Njia hii ilitoa wigo sahihi wa kuchambua jinsi vipindi vya *Ubongo Kids* huandikisha na kuingiza mada za elimu katika hadithi zake.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Kothari (2009) anaeleza kuwa maadili huwa na nafasi kubwa katika kazi yoyote ya utafiti. Kabla ya utafiti kufanyika, mtafiti anapaswa kuwa na ujuzi kuhusiana na maadili ya utafiti, muundo wake na uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Kwa kuzingatia mawazo haya, suala la maadili halikuepukwa katika kazi hii. Mtafiti aliomba kibali kutoka Chuo Kikuu Cha Chuka pamoja na Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na

Uvumbuzi (NACOSTI). Pia, mtafiti alitambua mchango wa wataalamu wengine katika kufanikisha kazi yake. Kwa hivyo, mtafiti aliwanukuu na kuwarejelea. Data ilikusanywa na kuchanganuliwa kulingana na mihimili ya nadharia ya Elimu Burudani iliyochaguliwa na mtafiti. Matokeo ya utafiti huu yaliwekwa wazi kwa kuchapishwa ili iweze kuwafaidi watafiti wengine.

# SURA YA NNE

# MASUALA IBUKA YANAYOWASILISHWA KATIKA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS*

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kujadili matokeo yanayohusiana na lengo la kwanza la utafiti, ambalo lilikuwa ni kujadili masuala ibuka yanayowasilishwa katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*. Katika sura hii, utafiti umefanya uchambuzi wa vipindi hivyo kwa kuangalia jinsi masuala mapya au yanayobadilika kijamii, kiuchumi, na kiutamaduni yanavyojitokeza na kuwaathiri watoto na jamii kwa ujumla. Masuala ibuka yanayozingatiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, usalama mtandaoni, elimu, usawa wa kijinsia, lishe bora na ulinzi wa watoto. Uchambuzi ulifanywa kwa kutumia Nadharia ya Elimu Burudani ya Miguel Sabido (2003) inayosisitiza kuwa burudani inaweza kutumika kama njia ya kuelimisha na kushawishi hadhira.

## 4.2 Mabadiliko ya Tabianchi

Kwa mujibu wa Jopo la Serikali za Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC, 2013), mazingira ya binadamu yako katika hatari ya kuangamia kutokana na vitendo vya binadamu. Vitendo hivi vinajumuisha ukataji wa miti, ujenzi holela katika maeneo ya mabondeni, matumizi ya teknolojia yenye madhara kwa mazingira, na ukosefu wa uadilifu katika uongozi. Matokeo ya vitendo hivi ni ongezeko la joto duniani, mabadiliko mabaya ya hali ya hewa, kuenea kwa magonjwa, vifo, kupungua kwa mavuno, na hatimaye kuongezeka kwa njaa. Sehemu hii inaangazia chanzo cha mabadiliko ya tabianchi, madhara ya mabadiliko ya tabianchi, na jinsi madhara haya yanavyoweza kuepukwa kulingana na vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*.

### 4.2.1 Chanzo cha Mabadiliko ya Tabianchi

Kama anavyosema Vasquez (1983), fasihi ina mchango mkubwa katika kuendeleza maadili na kuunda mitazamo ya wanadamu kuhusu masuala mbalimbali katika jamii. Kadri mazingira yanavyobadilika, ndivyo fasihi inavyozidi kuchukua jukumu la kuchunguza hali ya jamii. Fasihi hufanya hivyo kwa kutumia mbinu mpya za uandishi, mitazamo ya kina ya kimajadiliano na kushughulikia matatizo yanayoibuka katika jamii ya kisasa. Ndani ya kazi hizi za kifasihi, maudhui hutumika kuakisi uhalisia wa maisha ya kijamii (Wesonga na wenzake (2020). Kwa sababu suala la mazingira ni suala la

kijamii, linapaswa kuchunguzwa kwa kina, hasa linapojitokeza katika fasihi kwa sababu huwa linaonyesha mitazamo na hisia za wanajamii.

Mabadiliko ya tabianchi husababishwa na shughuli mbalimbali katika jamii katika vipindi vya *Ubongo Kids*. Kwa mfano:

(1). Koba: ... *Lakini pia sisi tunhitaji utusaidie, tunataka kujifunza kuhusu mabadiliko ya tabianchi na dharura ya tabianchi*
Baraka: *Ili tumshawishi Shiko kuja kujenga kituo cha kuzalisha umeme hapa Kokotoa*
Koba: *Na hili litasaidia marafiki zake Nina waliopoteza shule yao kwenye mafuriko...*
Kibena: *Nafikiri ninajua kinachosababisha mabadiliko ya tabianchi…Ninachokumbuka ni kwamba, tukichoma mafuta kwenye gari au pikipiki au kuchoma mkaa kwa ajili ya kupikia au kuchoma takataka, tunatoa hewa ya kabonidioksaidi angani. Kabonidioksaidi ni hewa ukaa.*
Koba: *Hewa ukaa hairuhusu joto kutoka kwenye dunia…*
(Ubongo Kids Kiswahili 2021b, 0:33 - 1:21)

Kwa mujibu wa dondoo la (1), chanzo kuu cha mabadiliko ya tabianchi ni shughuli za binadamu kama vile kuchoma mafuta kwenye magari na pikipiki, kuchoma mkaa kwa kupikia, na kuchoma takataka. Shughuli hizi hutoa hewa ya kaboni dioksaidi (hewa ukaa). Hewa hii inapojikusanya angani, hairuhusu joto kutoka duniani na hivyo kuvuruga hali ya hewa ya kawaida. Hali hii husababisha athari kama mafuriko, ambayo yanaafikiana na mawazo ya Greg (2004) anayeeleza kuwa matatizo ya mazingira yanaweza kufikishwa kwa jamii kupitia fasihi, kwani fasihi ina uhusiano wa karibu sana na utamaduni wa jamii.

Maudhui haya ya chanzo cha mabadiliko ya tabianchi huwasilishwa kwa njia inayoburudisha kupitia vikatuni kwenye vipindi vya *Ubongo Kids*. Kwa mujibu wa Sabido (2003), matumizi ya burudani kama njia ya mawasiliano husaidia kuelimisha watazamaji kuhusu chanzo cha mabadiliko ya tabianchi kwa namna rahisi na ya kuvutia. Hali hii huwezesha watazamaji kuelewa athari za matendo yao kwa mazingira na kuwahamasisha kubadili tabia zao ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mbinu hii ya elimu burudani huondoa ugumu wa kueleza masuala ya kisayansi kwa lugha ya

kitaalamu. Badala yake, hufanya ujumbe ufikie kila kila mtu kwa urahisi, hasa watoto ambao ni kizazi kinachotarajiwa kuishi na kushughulikia changamoto hizi kwa muda mrefu zaidi.

### 4.2.2 Madhara ya Mabadiliko ya Tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi ni tatizo la kimataifa linalozidi kushika kasi kutokana na ongezeko la shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira. Madhara ya mabadiliko ya tabianchi yameanza kuonekana wazi katika sehemu mbalimbali za dunia. Madhara haya yanaleta changamoto katika maisha ya binadamu, viumbe hai na mifumo ya ikolojia. Yafuatayo ni baadhi ya madhara makuu ya mabadiliko ya tabianchi kulingana na vipindi husika katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.

#### 4.2.2.1 Ongezeko la Joto Ulimwenguni

Njeru na wenzake (2022) wanaeleza kuwa mazingira asilia kama vile misitu, mito, milima na maziwa ni sehemu muhimu katika maisha ya binadamu. Mazingira asilia hutoa mahitaji ya msingi kama chakula, maji, hewa safi na makazi. Hata hivyo, kutokana na ongezeko la viwango vya joto duniani na mabadiliko ya tabianchi, kumekuwa na wasiwasi mkubwa katika jamii ya kimataifa. Hali hii imeibua mijadala ya kitaifa na kimataifa kuhusu namna bora ya kuhifadhi mazingira, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali asilia. Kwa hivyo, mjadala huu umechochewa na uelewa wa kwamba mazingira ni rasilimali na nguzo kuu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Suala la ongezeko la joto katika eneo la Kokotoa kwenye kipindi cha *Ubongo Kids* inadhihirika katika mazungumzo kati ya Nina na Koba:

(2). Nina: *Aise! Nahisi naweza kuyeyuka hapa! Hivi kokotoa ndio huwa kuna joto namna hii?*

Koba: *Huwa kuna joto lakini sio kama hili*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 17:09- 17:19)

Katika mazungumzo kati ya Nina na Koba katika dondoo la (2), kuna ongezeko la joto lisilo la kawaida katika eneo la Kokotoa. Nina anaeleza kuwa anahisi kama anaweza kuyeyuka kutokana na joto kali. Jambo hili linaonyesha mshangao na wasiwasi wa Nina kuhusu mabadiliko yasiyo ya kawaida katika hali ya hewa. Koba anasisitiza kuwa

Kokotoa huwa na joto, lakini anasisitiza kuwa kiwango cha joto cha sasa si cha kawaida. Mazungumzo haya yanaangazia athari za mabadiliko ya tabianchi, hasa kuongezeka kwa mawimbi ya joto kali yanayoathiri mifumo ya ikolojia na afya ya binadamu. Suala hili linawasilishwa kupitia burudani ili kuvutia watoto. Mtindo huu unaafikiana na mawazo ya Sabido (2003) kuwa burudani inaweza kutumika kama chombo cha kuelimisha na kushawishi tabia chanya katika jamii. Kupitia burudani, kipindi hiki cha *Ubongo Kids* huchochea uelewa wa kijamii kuhusu ongezeko la joto na umuhimu wa kulinda mazingira.

#### 4.2.2.2 Kukosekana kwa Vyakula

Kwa maoni ya Toromade na wenzake (2024), mabadiliko ya tabianchi huwasilisha vikwazo vikubwa kwa uwepo wa chakula duniani. Mabadiliko haya huathiri moja kwa moja uzalishaji wa mazao, kuvuruga kilimo, kuongeza uhaba wa chakula na kuzidisha utapiamlo. Pia, mabadiliko ya halijoto na mifumo ya mvua pamoja na kuongezeka kwa matukio ya hali mbaya ya hewa yanatishia mazao ya kilimo, afya ya mifugo na mifumo ya usambazaji wa chakula hasa katika maeneo yaliyo hatarini.

Katika vipindi vya *Ubongo Kids*, mabadiliko ya tabianchi huleta madhara kwenye sekta ya ukulima. Haya yanadhihirika wazi kutokana na mazungumzo kati ya Baraka na Mama:

| | | |
|---|---|---|
| (3). | Baraka: | *Shikamoo, tunatafuta maparachichi* |
| | Mama: | *Poleni wanangu, sijapata maparachichi zaidi ya wiki sasa.* |
| | Baraka: | *Jameni! Hata sokoni hatukupata hata moja* |
| | Mama: | *Ni kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Hakuna maji ya kutosha kwa ajili ya maparachichi.* |

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 19:33- 19:49)

Kulingana na mazungumzo haya kati ya Baraka na Mama kwenye dondoo la (3), mabadiliko ya tabianchi huathiri maisha ya kila siku ya watu, hasa katika sekta ya kilimo na upatikanaji wa chakula. Baraka na mwenzake wanaonekana kutafuta maparachichi bila mafanikio. Mama anawaeleza kuwa hajapata maparachichi kwa zaidi ya wiki na hata sokoni hakuna. Hali hii inasababishwa na mabadiliko ya tabianchi, hasa

ukosefu wa maji unaotokana na ukame au mvua zisizotabirika. Hii ndiyo sababu mazao kama maparachichi hushindwa kuota au kukomaa. Mazungumzo baina ya mama na Baraka yanaweka wazi jinsi mabadiliko ya hali ya hewa yanavyoathiri kilimo. Kupungua kwa uzalishaji wa chakula huathiri upatikanaji wa lishe bora, kando na kusababisha uhaba wa vyakula sokoni. Hali hii ni mfano wa jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri usalama wa chakula na maisha ya kila siku ya jamii. Wale wanaoathirika zaidi ni wanaoishi katika maeneo yanayokabiliwa na changamoto za kimazingira.

#### 4.2.2.3 Kuyeyuka kwa barafu Kaskazini mwa Dunia na Kuzuka kwa Moto wa Porini

Sharapov (2023) alifafanua kuwa Aktiki, eneo lenye umuhimu wa kiikolojia, linapitia mabadiliko makubwa kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kipengele cha kushangaza cha mabadiliko ya hivi karibuni katika Aktiki, hasa kuhusu barafu ya baharini ni kasi kubwa ambayo joto linaongezeka na barafu inayeyuka kwa haraka. Kupungua kwa kiwango na unene wa barafu kunaonyesha athari za ongezeko la joto duniani.

Kadiri barafu za ncha zinavyoyeyuka, jamii za asili na wanyamapori wanakabiliwa na changamoto ambazo hazijawahi kushuhudiwa hapo awali. Kwa mfano:

(4). Mama Ndege: *Marafiki zangu walikuwa wanapaa kwenye anga la ustaria na waliona moto mkubwa sana msituni. Lakini kwenye sehemu zingine za dunia, marafiki zangu batabuku wameona barafu kaskazini mwa dunia inayeyuka…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 5:12- 5:28)

Kauli ya Mama Ndege kwenye dondoo la (4) inatoa uchambuzi wa kina kuhusu athari tofauti za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali ya dunia. Mama Ndege anaposema kwamba marafiki zake waliona moto mkubwa msituni, anaangazia tatizo la ongezeko la joto duniani linalochangia ukame na hatimaye kusababisha moto wa porini. Hii huhatarisha maisha ya viumbe. Aidha, Mama Ndege anataja pia kuwa marafiki zake batabuku wameona barafu kaskazini inayeyuka, jambo linaloonyesha athari za ongezeko la joto katika maeneo ya baridi sana kama vile Aktiki na Antaktika. Kuyeyuka kwa barafu kunaweza kusababisha kuongezeka kwa kina cha bahari. Hii

inatishia jamii za pwani na mifumo ya ikolojia ya baharini. Kauli ya Mama Ndege pia inaashiria kuwa mabadiliko ya tabianchi yana madhara yasiyo na mipaka ya kijiografia, na yanaathiri sayari nzima kwa namna tofauti.

Ujumbe kwenye dondoo la (4) unaeleza kuwa kuyeyuka kwa barafu na moto wa porini huathiri mazingira duniani kote. Ujumbe huo unalenga kuelimisha na kuhamasisha kupitia burudani (Sabido, 2003). Barafu inayoyeyuka inakuwa wito wa dharura, ikihamasisha harakati kuelekea uendelevu na usimamizi bora wa mazingira. Vipindi vya *Ubongo Kids* vinachukua nafasi ya mapambano haya. Vipindi hivi huonyesha kubadilika kwa tamaduni na kuhama kwa aina mbalimbali za wanyama ambao wamefanikiwa katika mandhari za barafu kwa milenia. Vipindi hivi vinachunguza ustahimilivu unaohitajika ili kukabiliana na hali mpya.

#### 4.2.2.4 Uchafuzi wa Mto, Hatari ya Magonjwa na Vifo vya Wanyama

Ogola na wenzake (2024) wanaeleza kuwa kimataifa, uchafuzi wa maji ni mojawapo ya matatizo makubwa ya kimazingira. Chanzo chake ni ongezeko la idadi ya watu, maendeleo ya haraka ya viwanda na shughuli duni za kilimo. Uchafuzi wa maji pia hutokana na uchafuzi wa mazingira na uchafuzi wa udongo pamoja na mashapo kwa kutumia viuadudu na kemikali nyingine zinazosababishwa na shughuli za binadamu. Mito na vijito vingi nchini Kenya hupoteza ubora wa maji yanapopita katika miji. Mara nyingi mito huchafuka kutokana na shughuli za binadamu kama utupaji ovyo wa taka na uchafuzi wa viwanda. Pia, mvua nyingi na mafuriko huweza kuzidi uwezo wa mifumo ya usafi wa mazingira kama vile tangi ya maji taka. Hali hii huifanya kuvuja na kusafirisha vichafuzi (kama mbolea na taka) kwenye mto, maziwa na baharini. Kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| (5). | Kibena: | *Tunaweza tukafanya usafi lakini tukashindwa kuogolea* |
| | Koba na wenzake: | *Kivipi je?* |
| | Kibena: | *Mimi naona, maji hayawezi kuwa na rangi ya kahawia kisha tu takataka.* |
| | Koba: | (*Akicheka), Jameni, ebu fikirieni vizuri….* |

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 4:20-4:42)

Dondoo la (5) linaonyesha changamoto zinazotokana na uchafuzi wa mazingira, hasa vyanzo vya maji, na jinsi watoto wanavyojaribu kukabiliana na hali hiyo kwa vitendo. Kibena na wenzake wanaonyesha dhamira njema ya kulinda mazingira yao kwa kupanga kufanya usafi kila Jumamosi. Hata hivyo, Kibena anatoa tahadhari kwamba usafi usiofanywa kwa umakinifu hauwezi kutosha ikiwa chanzo halisi cha uchafuzi (kama sumu ndani ya maji) hakitatambuliwa. Kauli yake inaonyesha fikra za kina na uwezo wa kuchanganua matatizo kwa undani. Kwa upande mwingine, majibu ya Koba, hasa ya kucheka, yanaweza kueleza ukosefu wa uelewa wa kina au mwelekeo wa kubeza hoja za tahadhari. Mtazamo huu unatoa picha ya tofauti za mitazamo katika jamii kuhusu masuala ya mazingira: kuna wanaochukua hatua, wengine wanaoelewa kwa undani zaidi na pia wanaochukulia mambo kwa wepesi. Kauli ya Kibena kwamba: *maji hayawezi kuwa na rangi ya kahawia kisha tu takataka*, inadokeza umuhimu wa kuchunguza chanzo halisi cha matatizo ya mazingira.

Pia, vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* vinaangazia jinsi wanyama wanaoishi majini kama vile samaki hutaabika kutokana na athari za uchafuzi wa mito. Kwa mfano:

(6). Kiduchu: *Una shida gani?*
Samaki: *(Akikohoa) Naumwa sana. Ni haya sabuni na mapovu zote zote hizi zinanifanya nasikia vibaya!... (Anaendelea kukohoa).*
Kiduchu: *Nenda nyumbani ukapumzike.*
Samaki: *Lakini hapa ndipo nyumbani kwetu.*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 7:29- 7:45)

Kifungu cha (6) kinaangazia uchafuzi wa mazingira kama tishio kwa maisha ya viumbe wa majini. Samaki anayeugua kutokana na sabuni na mapovu anawakilisha madhara ya moja kwa moja ya tabia za kibinadamu zisizowajibika. Kauli ya samaki kama: *Lakini hapa ndipo nyumbani kwetu*, inaonyesha hisia za huzuni na kukata tamaa. Hii ni kwa sababu hata katika mateso yake, hawezi kuondoka kwani maji hayo ndiyo makazi yake ya asili. Hili linaibua hisia nzito kuhusu wajibu wa binadamu kulinda mazingira kwa ajili yao na ya viumbe wengine wanaotegemea mazingira hayo kuishi. Hivyo, kipindi hiki kinalenga kuwazindua watoto na jamii kwa jumla kuhusu athari za kutotunza mazingira, ikiwajengea moyo wa uwajibikaji na huruma kwa viumbe hai.

### 4.2.3 Jinsi ya Kuzuia Mabadiliko ya Tabianchi

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi huakisi uhusiano, mwingiliano na migongano kati ya binadamu na mazingira yao. Msanii wa fasihi hutumia hali halisi inayomzunguka kama chanzo cha ubunifu wake. Kazi za fasihi hutumika kama nyenzo ya kusaidia jamii kukabiliana na changamoto za maisha. Pia, hutoa maarifa ya kujielewa na mbinu za kutatua matatizo mbalimbali yanayoukumba ulimwengu kwa ujumla. Kwa mujibu wa Reuveny (2007), watu wana mitazamo tofauti kuhusu suala la uchafuzi wa mazingira: baadhi yao huchagua kuishi katika mazingira machafu bila kuchukua hatua yoyote. Wengine hukubali tu hali hiyo kama changamoto ya kimazingira na wapo pia wanaochukua jukumu la kufanya mabadiliko ili kuboresha maeneo yaliyoathiriwa.

Kupitia elimu burudani, vipindi vya *Ubongo Kids* huchochea matumizi ya mbinu endelevu za kimazingira kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| (7). Shiko: | *Tunaweza tukaipanda hapa* |
| Msaidizi wa Shiko: | *Mamilioni ya hela ambazo…* |
| Shiko: | *Hii ndio biashara sasa…* |
| Mwanafunzi 1: | *Unawezaje kufanya hivyo?* |
| Shiko: | *(Akielekea aliko Koba) Utakuwa mfanya biashara mmoja mzuri kijana. Ulikuwa sahihi. Tunaweza kupanda miti hapa kufunika eneo hili lote na kuongeza msitu halafu watu ulimwenguni kote watakuwa wanatulipa kwa kufanya hii kazi kwa sababu tutakuwa tunavuta kaboni inayotoka angani na kuihifadhi kwenye ardhi. Inaitwa… Inaitwaje vile?* |
| Mwanafunzi 1: | *Krediti za kaboni…* |

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 33:12- 33:45)

Mazungumzo kwenye dondoo la (7) yanaangazia umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kupitia upandaji miti. Mazungumzo haya yanadhihirisha kuwa miti inaweza kusaidia kupunguza hewa ya kaboni na hivyo kulinda mazingira. Pia, yanaonyesha jinsi uhifadhi wa mazingira unaweza kugeuzwa kuwa fursa ya kiuchumi kwa jamii. Ni jukumu la binadamu kuheshimu na kutunza dunia kama sehemu muhimu ya maisha yao. Watu wanafaa kupanda miti, kutumia nishati mbadala, na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu

wa mazingira. Kipindi hiki kinaandaa watoto kuwa raia wanaojali mazingira huku kikijenga hisia ya uwajibikaji kwa maumbile mapema.

Hatimaye, ushirikiano na uwajibikaji pia husaidia kuzuia mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano:

> (8). *...Lazima tupambane kwa pamoja kila saa, lazima tubadilike na kuishi kwa kujali kuwa tabianchi inabadilika…*
>
> (Ubongo Kids Kiswahili, 2023, 0:13-0:21)

Kauli hii kwenye dondoo la (8) inatilia mkazo jukumu la kila mtu kuchukua hatua ya kulinda mazingira. Watazamaji kwenye kipindi wanaelimishwa kuwa mabadiliko ya tabianchi si suala la mtu mmoja au taasisi moja, bali ni changamoto inayokumba watu wote. Ili kubadilisha mienendo yao, kauli kama: *lazima tupambane kwa pamoja* na *lazima tubadilike na kusihi kwa kujali tabianchi inabadilika*, hutumika kuwarai watazamaji kusisitiza kujali kwani tabianchi inabadilika. Burudani kwenye kipindi hiki cha vikatuni huchochea mabadiliko ya tabia kwa njia isiyo ya kulazimisha. Badala yake, hushirikisha kihisia na kielimu na kuifanya hadhira kuona kuwa kulinda mazingira ni jukumu lao la kila siku, wala sio jambo la watu wa fani fulani pekee.

## 4.3 Afya na Usafi

Kwa mujibu wa Ngugi (2017), fasihi ya watoto imekuwa chombo muhimu katika kuhamasisha maadili ya kiafya na usafi miongoni mwa watoto. Maudhui haya huandikwa kwa lugha rahisi na yenye mvuto. Lengo kuu likiwa ni kuafikiana na uwezo wa ufahamu wa watoto na kuwahamasisha kwa njia ya burudani. Naye Mwilaria na wenzake (2024) wanaeleza kuwa fasihi ya Kiswahili ya watoto imekuwa na mchango mkubwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya afya kama vile magonjwa na umuhimu wa usafi. Kwa sababu hiyo, kazi nyingi za fasihi ya watoto zimeandikwa zikilenga kuangazia masuala haya. Hii ni kutokana na ukweli kwamba afya ni nguzo muhimu katika ustawi wa jamii na katika kufanikisha maendeleo endelevu.

### 4.3.1 Usafi wa Mazingira

Kwa mujibu wa Wesonga na wenzake (2020), uchafuzi wa mazingira ni jambo lililoenea kila pahali. Ni suala linaloendelea kuzungumziwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo fasihi. Hata hivyo, Wesonga na wenzake wanaonya kuwa suala la uhifadhi wa

mazingira huenda likawa suala gumu iwapo binadamu hawatajitolea kulikabili vilivyo. Kenya na sehemu nyingi za dunia zinakabiliwa na changamoto kama vile ukataji miti ovyo, uchafuzi wa mazingira, uhaba wa maji na usimamizi hafifu wa taka (*National Environment Management Authority*, 2021). Ukuaji wa haraka wa miji na viwanda umesababisha ongezeko la uchafuzi wa hewa na maji, hasa katika miji kama Nairobi na Mombasa. Aidha, Kenya imechukua hatua kukabiliana na changamoto hizi, ikiwemo kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kutekeleza sera za kuboresha usimamizi wa taka. Hata hivyo, maeneo ya taka haramu na utekelezaji hafifu wa sheria za mazingira bado ni vizingiti vikuu. Uchafuzi unaotokana na maji machafu na taka za viwandani umesababisha kuenea kwa bakteria sugu kwa viuavijasumu. Hali hii inafanya magonjwa kama vile kifua kikuu na homa ya matumbo kuwa magumu kutibu.

Usafi wa mazingira hupeperushwa kupitia njia ya burudani kwa kutumia kauli za kwenye vipindi hivi vya vikatuni. Kwa mfano:

9 (a). *…Usafi wa mazingira. Shirikiana nasi kuzuia maradhi, Okota takataka. Saidia jamii…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2017b, 0:30- 0:38)

Dondoo hili la 9 (a) linalenga kuhimiza usafi wa mazingira na ushirikiano wa kijamii katika kuzuia magonjwa. Usafi wa mazingira ni suala nyeti katika jamii ya kisasa, hususan mijini na maeneo yenye msongamano wa watu (*National Environment Management Authority*, 2021). Matumizi ya burudani kuwasilisha ujumbe mzito kwa hadhira huondoa ukavu wa ujumbe wa moja kwa moja kwa kutumia kauli kama vile: *Safisha mazingira* na *shirikiana nasi* (Sabido, 2003). Pia, kauli hii huongeza ushawishi kwa kuwa watu wanapoburudika, wako tayari kupokea maarifa. Kwa njia hiyo, watazamaji wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika juhudi za kijamii zinazolenga kulinda afya kwa kudumisha mazingira safi.

Kauli iliyonukuliwa kwenye 9 (a) imewekwa katika muktadha wa vikatuni, ambavyo vina sifa ya kuvutia, kuchekesha, na kufundisha bila kuchosha. Vipindi hivi vinavyotumia sauti na picha hufanikiwa kuvutia umakini wa watoto na kuwa chombo bora cha kuwafundisha watoto kuhusu usafi. Kwa mujibu wa Brown (2017), watazamaji huburudishwa kando na kupata mafunzo kutoka kwenye vipindi vya

televisheni. Watoto wanaweza kujifunza kuhusu usafi wa mazingira kupitia hadithi za kuburudisha na za kugusa hisia. Burudani huwasaidia kuelewa umuhimu wa kudumisha usafi wa mazingira kwa njia ya kufurahisha na isiyosahaulika. Kwa kuwasilisha usafi kwa njia ya kufurahisha na inayoeleweka, watoto wana uwezo wa kukubali tabia hizi kama sehemu ya mifumo yao ya kila siku. Aidha, vipindi hivi vinakuza hisia za uwajibikaji wa kimazingira na kuwasaidia watoto kutambua kwamba hata vitendo vidogo (kama vile kuweka taka kwenye takataka au kudumisha chumba chao kikiwa safi) vinaweza kuwa na athari chanya kwa jamii kubwa na kwa dunia nzima.

Hali ya mazingira katika vipindi vya *Ubongo Kids* pia huonyeshwa kuwa chafu na iliyotelekezwa, huku taka zikisababisha harufu mbaya na kuleta minyoo. Kwa mfano:

9 (b). Amani: *Dah! Watu wa taka na usafi wako wapi jameni?*

Toto Tembo: *Nyie binadamu, mnategemea watu wengine wawafanyie usafi. Sisi wanyama wa msituni tunafanya wenyewe.*

Amani: *Mimi siwezi kufanya kazi hiyo!*

Toto Tembo*:* *Hapana, ni kazi muhimu sana maana huwezi kuishi mazingira safi na salama bila kufanya usafi.*

Amani: *Ah! Taka zinanuka! Na wameleta minyoo...*

Toto Tembo: *Kama kila mtu angefanya usafi mara kwa mara, usingekuwa mwingi hivi*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 1:02-1:30)

Mazungumzo kati ya Amani na Toto Tembo kwenye dondoo la 9 (b) la *Ubongo Kids* yanatumika kama chombo cha burudani kinachowasilisha ujumbe mzito kuhusu usafi wa mazingira. Mazungumzo haya yanawasilisha hali halisi ya kijamii ambapo kuna uchafuzi wa mazingira na watu wengi hutelekeza wajibu wao wa kutunza mazingira. Wanasubiri wengine wafanye hivyo kwa niaba yao. Amani anawakilisha mtazamo huu wa kutegemea wengine, huku Toto Tembo akiwakilisha kundi linalosisitiza kuwa mazingira safi ni matokeo ya juhudi za pamoja. Kupitia burudani, watazamaji, hasa watoto, wanaelimishwa kuwa usafi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja, na si la mamlaka pekee (Sharma, 2023). Burudani hiyo inafanikisha uhamasishaji kuhusu uwajibikaji na kuchochea mabadiliko ya mitazamo kuhusu mazingira katika jamii kwa kuficha ujumbe ndani ya burudani.

### 4.3.2 Umuhimu wa Lishe Bora na Mazoezi

Okowa (2024) aliweka wazi kuwa Kenya inakabiliwa na mzigo wa ujalivu na utapiamlo. Upungufu wa virutubisho pamoja na magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanayotokana na lishe vinaongezeka kwa pamoja. Okowa anaeleza kuwa takriban Wakenya milioni 23 wanakabiliwa na utapiamlo. Mwaka wa 2022, asilimia kumi na nane ya watoto wachanga chini ya umri wa miaka mitano walikuwa wamekudumaa, huku asimilia kumi wakiwa na uzito mdogo kuliko inavyostahili (Okowa, 2024). Kitovu cha janga hili ni mfumo wa chakula uliogawanyika nchini Kenya. Mfumo huo unakumbana na changamoto za uzalishaji, minyororo ya ugavi isiyo na ufanisi, na athari za uharibifu zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Ngugi (2017) alibainisha kwamba maisha ya kisasa yameleta changamoto na matarajio mapya yanayomhusu mwanadamu, hasa ya afya. Hali hii ya mabadiliko katika jamii imesababisha umuhimu wa kuzingatia masuala ya afya katika muktadha wa elimu ili kumwezesha mtoto kuelewa kwa kina mazingira yanayomzunguka.

Katika muktadha wa lishe bora na mazoezi, vipindi vya *Ubongo Kids* vinatumika kama njia ya burudani na elimu vinavyowasilisha maudhui ya afya kwa watoto kwa njia rahisi na ya kuvutia. Kauli kama:

10 (a). *"Wanga hutupa nguvu mwilini. Twahitaji kuishi vyema" …*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 0:40: 0:47)

Kauli kwenye dondoo la 10 (a) inaonyesha umuhimu wa vyakula vya nishati katika shughuli za kila siku, hasa kwa watoto wanaohitaji nguvu kwa michezo na masomo. Mtazamaji huelewa kwamba wanga ni chanzo muhimu cha nguvu mwilini. Wanajifunza kuwa vyakula vya wanga (kama vile ugali, wali na viazi) ni muhimu kwa kuwawezesha kufanya shughuli zao za kila siku kwa ufanisi. Watazamaji wanaelekezwa kuelewa kuwa lishe bora ndiyo msingi wa afya njema na maisha yenye ufanisi. Kupitia lishe inayojumuisha makundi yote ya chakula, mtu huimarisha mwili, akili na kinga dhidi ya maradhi. Hivyo, ulaji bora hujenga msingi wa ukuaji, ujifunzaji, na ustawi wa kila siku.

Aidha, mchango wa protini katika ukuaji wa mwili huelezwa kwenye vipindi vya Ubongo Kids kama inavyodhihirika kwenye kauli ya 10 (b). Kwa mfano:

10 (b). *"Protini hujenga mwili na kurekebisha seli zetu"*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 1:37: 1:45)

Kauli kwenye dondoo la 10 (b) inaeleza kuwa protini husaidia kujenga na kurekebisha misuli mbalimbali mwilini. Watazamji huelewa kuwa protini hurekebisha seli zilizoharibika, hivyo kusaidia miili yao kupona wanapojeruhiwa au kuugua. Kauli hii inafungamana na umuhimu wa mazoezi yanayohitaji misuli imara. Hii inasisitiza umuhimu wa kula vyakula vyenye protini ili kudumisha afya bora.

Vilevile, watazamaji hupata mafunzo jinsi ambavyo mboga na matunda hufanikisha lishe bora. Tazama hapa chini dondoo ya 10 (c):

> 10 (c). … "*Mboga na matunda zinatulinda na magonjwa. Hutujengea kinga na kutulinda" …*
>
> *(*Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 2:32- 2:40)

Kauli kwenye dondoo la 10 (c) inasisitiza uhusiano kati ya lishe bora na kinga ya mwili. Hii ni muhimu kwa mtoto anayejihusisha na mazoezi ya kila siku. Matunda huwa chanzo kikubwa cha vitamini na madini na kupunguza hatari ya magonjwa mwilini. Kauli hii inawafanya watazamaji waone umuhimu wa kula mboga na matunda kila siku kama sehemu ya lishe bora.

Ikoro (2022) anaeleza kuwa vikatuni vina uwezo wa kushawishi umma kwa kupunguza ugumu wa kuelewa mambo ya kijamii ili kufanikisha mabadiliko panapohitajika. Kwa kuangazia vyakula hivi kwa mtazamo chanya, vipindi hivi kwenye *Ubongo Kids* vinawahamasisha watoto kuanza kuthamini lishe bora tangu utotoni. Hali hii inaafikiana na mawazo ya Sharma (2023) anayesema kuwa watu huweza kujifunza kupitia elimu burudani. Watoto hujifunza suala la lishe bora huku wakifurahia vipindi vya kuburudisha.

**4.4 Elimu**

Gitau na wenzake (2023) wanaeleza kuwa elimu inayowasilishwa darasani inaendelea kupanuka duniani kote kadri changamoto mpya zinavyoibuka kila siku. Jamii zinakabiliwa na hali na matukio tofauti yanayohitaji kuzingatiwa katika mipango ya elimu. Ufundishaji unapaswa pia kuchochea mabadiliko miongoni mwa wanafunzi na jamii kwa ujumla kuhusu masuala mtambuko. Hivyo basi, maarifa, ujuzi na maadili yanayofundishwa darasani yanapaswa kuwa na maana na umuhimu kwa wanafunzi ili

kuwasaidia kukabiliana na changamoto zinazotokana na masuala hayo. Schleicher (2018) anasisitiza jambo hili kwa kueleza kuwa mifumo ya elimu inapaswa kulingana na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii. Hii itawasaidia wanafunzi kupata elimu itakayowawezesha kuboresha ujuzi, maarifa, mitazamo na maadili muhimu kwa maisha baada ya shule. Mtaala wa umilisi unalenga kuwawezesha wanafunzi kukuza uwezo wa kutumia ujuzi na maarifa wanayojifunza shuleni katika kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii. Mtaala huu humwezesha mtoto kufikiri, kuwa mbunifu, na kuhusika katika suluhisho za changamoto za kisasa.

### 4.4.1 Mtaala wa Umilisi

Chiduo na wenzake (2016) wanafafanua kuwa mtaala ni mpangilio wa masomo unaolenga kiwango fulani cha elimu. Katika muktadha wa utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu nchini Kenya (ulioanzishwa mwaka wa 2017), masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati yamepewa kipaumbele. Hii ni kwa sababu yanayozingatiwa kuwa msingi wa maandalizi ya wanafunzi kwa dunia ya sasa inayozidi kuongozwa na teknolojia (Wataka na wenzake, 2021). Hata hivyo, utekelezaji wa mtaala huu unatatizwa na changamoto kama uhaba wa walimu, mitazamo hasi ya kijamii, na miundombinu duni (Wataka na wenzake, 2021; Cheruiyot, 2024). Televisheni, kama chombo cha mawasiliano, huunganisha elimu na maisha halisi (Özer & Avcı, 2015). Vipindi vya *Ubongo Kids* hutumia burudani kuwasilisha dhana za kisayansi kwa namna inayoeleweka na kuvutia watoto. Hii ni muhimu hasa kwa maeneo yasiyo na vifaa vya kisayansi, kwani inasaidia watoto kuelewa kuwa sayansi ipo katika maisha yao ya kila siku (Kitainge na wenzake, 2022). Baadhi ya masuala katika mtaala wa umilisi ambayo yameangaziwa katika vipindi vya *Ubongo Kids* ni umilisi wa teknolojia, umilisi wa hisabati na umilisi wa sayansi.

#### 4.4.1.1 Umilisi wa Teknolojia

Ukosefu wa maarifa na stadi sahihi katika matumizi ya teknolojia miongoni mwa walimu ni mojawapo ya vikwazo vinavyolemaza utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi (Ondimu, 2018). Naye, akieleza kuhusu umuhimu wa teknolojia katika elimu, Owala (2021) anasisitiza kuwa teknolojia inapochukua nafasi kama nyenzo ya ufundishaji, huwezesha walimu na wanafunzi kupata maarifa mapya, stadi, mitazamo na maadili yanayoboresha matokeo ya ufundishaji. Vilevile, mbinu na vifaa vya ufundishaji

vinategemeana ili kufanikisha mchakato wa ufundishaji. Vifaa sahihi vya ufundishaji huchangia kuimarisha mbinu zinazotumiwa kufunza, na hivyo kurahisisha kufikiwa kwa malengo ya ufundishaji. Katika muktadha huu, vipindi vya *Ubongo Kids* huchangia katika kuziba pengo hili kwa kutoa vipindi vya kielimu vinavyotumia teknolojia. Kwa mfano:

(11). Ngendere: *…sasa naambiwa redio hio inapatikana mia moja na mbili na nusu FM. Inaitwa redio Mikuge. Sasa nimekuja kujaribu katika redio yangu hii, nakuta mtindo ulioandikwa ni tofauti. Hapo ndio wakanichanganya kabisa. Njoo muone wenyewe…*

Kibena: *Nishagundua, unajua nini Kiduchu, Ngendere hajui desimali na ndio maana ameshindwa kujua kabisa kama namba alilotajiwa ipo katika redio...Sikiliza Ngendere ili usitusumbue tena siku nyingine, ngoja tukuelekeze kitu.*

Kiduchu: *Mwambie faster Kibena tukacheze mpira*

Kibena: *Wewe unakumbuka kuhusu sehemu?*

Ngendere: *Yeah, nakumbuka*

Kibena: *Sasa kama unakumbuka leo nataka nikuambie kwamba kuna mtindo mwingine wa kuandika namba na mtindo huu unaitwa desimali. Katika desimali, tunaandika namba, nukta, namba. Hii ina maana kwamba namba kabla ya nukta ni kitu kamili…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2014c, 5:47-7:12)

Dondoo la (11) linaonyesha jinsi changamoto za kutofahamu dhana za kimsingi katika somo la hisabati (kama vile desimali) huathiri uwezo wa watazamaji kutumia teknolojia kwa ufanisi. Ngendere anaeleza kuchanganyikiwa kwake kuhusu kutafuta kituo cha redio katika mzunguko sahihi wa *FM* kwa sababu hajui maana ya namba desimali. Hili linadhihirisha ukosefu wa uelewa wa dhana hiyo ya kihisabati. Kibena, ambaye anaelewa vizuri, anatumia fursa hiyo kumueleza Ngendere kwa lugha rahisi kuhusu namna ya kuandika namba katika mfumo wa desimali. Anaeleza kuwa namba huandikwa kwa mpangilio wa namba, nukta, na kisha namba nyingine, ambapo namba kabla ya nukta huwa ni kitu kamili. Hivyo, vipindi vya *Ubongo Kids* hujenga uelewa wa watoto kwa kuhusisha masuala ya maisha ya kila siku na maudhui ya kitaaluma. Hii hukuzwa maarifa na stadi za kiakademia na kuwasaidia kutumia teknolojia kwa ufanisi zaidi.

Aidha, dondoo la (11) linaweza kufasiriwa vyema kwa kutumia muktadha wa Mtaala wa Umilisi unaotekelezwa nchini Kenya. Ujumbe wa kijamii kwenye vipindi vya televisheni huunganishwa na mazungumzo ili kuvifanya vivutie na kuelimisha

(Sharma, 2023). Katika hali hii, kipengele cha Hisabati kinajitokeza wazi, ambapo ufahamu wa namba za desimali ni msingi muhimu unaoathiri uwezo wa mtu kutumia vifaa vya teknolojia kama vile redio, simu au kompyuta. Tukio hili linaonyesha uhusiano wa karibu kati ya maarifa ya kihisabati na matumizi ya teknolojia, kwani Ngendere alihitaji kuelewa desimali ili kuingiza masafa sahihi kwenye redio.

Mulenga (2025) anadhihirisha kuwa Kenya imepiga hatua na kuwa kitovu cha teknolojia barani Afrika. Hii imechochewa na ubunifu wake, idadi kubwa ya vijana, ongezeko la upatikanaji wa intaneti, na sera za serikali zinazohimiza maendeleo. Mageuzi ya kidijitali nchini Kenya yanahusu sekta mbalimbali, zikiwemo huduma za kifedha, mawasiliano, ubunifu, na uanzishaji wa biashara ndogo na wajasiriamali. Hali hii inaiweka Kenya kama mfano wa kuigwa katika ukanda huu. Kenya inapozidi kuwa kitovu cha ubunifu, vipindi vya *Ubongo Kids* hulinganisha hali hiyo kwa kutumia vipindi vyake vinavyotatua changamoto kwa kutumia fikra za kisayansi na kiteknolojia. Hivyo, hali hii inaangazia umuhimu wa Mtaala wa Umilisi katika kushiriki kikamilifu katika maisha ya kisasa yanayotawaliwa na teknolojia.

#### 4.4.1.2 Umilisi wa Hisabati

Hisabati kwa muda mrefu imekuwa changamoto kwa wanafunzi wengi nchini Kenya, na maendeleo ya hivi karibuni yanaonyesha kuwa bado ni suala muhimu (Mong'ina, 2025). Uanzishaji wa Mtaala wa Umilisi umeibua mjadala kuhusu iwapo Hisabati inapaswa kuendelea kuwa ya lazima katika shule za upili ya juu. Baadhi ya watu wanapendekeza kuifanya hiari kutawapa wanafunzi nafasi ya kuzingatia uwezo wao binafsi, ilhali wengine wana wasiwasi kuwa hatua hiyo inaweza kupunguza fursa za kazi siku za usoni. Mwangi na wenzake (2024) walikiri kuwa nchini Kenya, changamoto kuu katika ujifunzaji wa Hisabati ni jinsi ya kuboresha uelewa wa dhana miongoni mwa wanafunzi unaohusiana na mchakato wa ujifunzaji. Brown (2017) alisisitiza kuwa vipindi kwenye televisheni vinaweza kutumika kuelimisha kando na burudani.

Kwenye vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids,* watazamaji hufunzwa hisabati kwa njia ya burudani. Vipindi hivi huchambua dhana ngumu kama desimali, asilimia, kuzidisha, kutoa, kugawanya na vipimo kwa njia rahisi na ya kuvutia. Kwa mfano:

(12) …*Tisa jumlisha tisa ni kumi na nane. Naandika tisa hapa, nabeba moja…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2020a, 0:23 – 0:40)

Maelezo haya kwenye dondoo la (12) yanahusiana moja kwa moja na somo la hisabati katika muktadha wa Mtaala wa Umilisi. Mwanafunzi anajifunza kufanya mjumuisho wa tarakimu na kuelewa dhana ya *kubeba* moja. Hii ni mbinu ya kimsingi katika mjumuisho wa nambari zaidi ya kumi. Maarifa haya hukuza stadi za maisha inayotumika kila siku katika hali kama vile kupanga bajeti au kuhesabu muda. Kwa kutumia mbinu shirikishi kama kutumia vitu halisi au maumbo ya kuhesabia, wanafunzi wanaweza kuelewa dhana hii kwa kina na kuweza kuitumia kwa uhuru. Mtaala wa Umilisi unalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi hawajifunzi kwa kukariri tu, bali wanapata uelewa wa kweli unaowawezesha kutumia hisabati kwa ufanisi katika mazingira halisi ya maisha yao ya kila siku.

#### 4.4.1.3 Umilisi wa Sayansi

Ufundishaji wa masomo ya sayansi nchini Kenya ni suala ibuka, hasa kwa kuzingatia vipengele vinavyohusiana na mafunzo ya walimu, upatikanaji wa rasilimali, na marekebisho ya mtaala. Ufundishaji wa sayansi hukumbwa na changamoto kama uhaba wa walimu, matumizi duni ya rasilimali za kufundishia sayansi, pamoja na hitaji la maendeleo ya kitaaluma kwa walimu (Odhiambo, 2024). Juhudi zimefanywa kuboresha elimu ya sayansi, kama vile mpango wa *Strengthening Mathematics and Science Education (SMASE)*, unaolenga kuongeza uwezo wa walimu katika kufundisha masomo ya sayansi na hisabati kwa ufanisi. Vilevile, marekebisho katika mafunzo ya walimu yamependekezwa ili kuboresha upatikanaji wa elimu, ubora, na usawa katika sekta ya elimu. Licha ya juhudi zilizofanywa, changamoto bado zipo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sayansi kama vile uhaba wa vitabu vya kiada na miundombinu ya kutosha (Cheruiyot, 2024). Hata hivyo, vipindi vya televisheni vipo mstari wa mbele katika kukuza ujifunzaji wa sayansi kwa watoto na kuwasaidia kuelewa dhana za kisayansi kwa njia rahisi na ya kuvutia, hivyo kuleta mabadiliko chanya katika mtazamo wao kuhusu sayansi.

Vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* hufundisha umilisi wa sayansi kwa njia ya kuvutia. Njia hii huwasaidia watoto kuelewa masuala ya kisayansi kama vile mzunguko wa dunia. Kwa mfano:

> (13). …*Lakini tukiwa huku duniani, tunalizunguka jua, tunalizunguka wakati wote…Kwa Kiingereza tunasema orbiting...Hatulizunguki kwa haraka hivyo, inachukua mwaka mmoja kwa dunia kumaliza mzunguko mmoja...*
> (Ubongo Kids Kiswahili, 2017c, 3:01 – 3: 56)

Katika muktadha wa mtaala wa umilisi, maelezo haya kwenye dondoo la (13) kuhusu mzunguko wa dunia na mwezi yanatoa fursa muhimu ya kujifunza sayansi kwa njia inayohusiana moja kwa moja na maisha halisi. Dhana ya dunia kulizunguka jua, inayojulikana kama *orbiting* kwa Kiingereza imeelezwa. Kando na kutoa maelezo ya kimasomo, vipindi hivi huwa msingi wa kuelewa mabadiliko ya misimu, majira, na vipindi vya mwezi. Mabadiliko haya huathiri shughuli mbalimbali za binadamu kama vile kilimo, uvuvi, na hata kalenda ya kijamii. Uwezo wa kuelewa mienendo hii ya kiastronomia huwajengea wanafunzi misingi thabiti ya kufikiri kisayansi, kuhoji mazingira yao, na kuelewa nafasi yao katika ulimwengu.

### 4.5 Masuala ya Kijamii

Masuala ya kijamii katika dunia ya leo yanahusisha changamoto nyingi na nzito zinazogusa maisha ya watu duniani. Jamii zinakabiliwa na matatizo yanayohitaji uangalizi makini na hatua madhubuti ili kupata suluhisho. Masuala haya si dhana za kufikirika tu, bali hujitokeza katika maisha ya kila siku, yakionekana katika familia, shule, mahali pa kazi na mitaani. Baadhi ya masuala ya kijamii katika vipindi vya *Ubongo Kids* ni ulinzi wa watoto na usawa wa kijinsia.

#### 4.5.1 Ulinzi wa Watoto

Kwa mujibu wa Ngugi (2017), watoto wana haki ya kutunzwa, kulishwa, kuvishwa kusomeshwa, kutodhulumiwa na hata kupewa nafasi ya kushiriki michezo na wenzao. Hata hivyo, Gitonga (2022) alieleza kuwa nchini Kenya kwa ujumla, kumekuwa na ukosefu wa utii wa masharti ya haki za mtoto, hasa yanayohusu ulinzi wa maslahi bora ya watoto. Ingawa Kenya imepiga hatua katika kulinda haki za watoto (hasa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Watoto ya mwaka 2022), bado kuna changamoto kama vile watoto wengi kukumbana na ukatili mtandaoni na itikadi kali. Pia kuna changamoto

kama vile kuondolewa kwa watoto katika taasisi za malezi na tatizo la ulinzi wa watoto wa jinsia mbili. Vilevile, watoto wengi wanadhulumiwa kingono ila hawana ujasiri wa kuripoti visa hivi.

Katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*, watoto wanafunzwa kuhusu haki zao za kutoruhusu kudhulumiwa. Tazama dondoo la (14):

> (14). *…Usinishike nywele bila ridhaa, usinishike ngozi bila ridhaa...*
> (Ubongo Kids Kiswahili, 2018b,19:00-19:09)

Kwa mujibu wa dondo la (14), watoto wanaelimishwa kuhusu haki zao za kimwili na umuhimu wa ridhaa. Kauli hii inasisitiza kwamba kila mtoto ana haki ya kuwa na udhibiti kamili juu ya mwili wake. Kuguswa, kushikwa au kushughulikiwa kwa namna yoyote ile inayohusiana na mwili wake kunapaswa kufanyika kwa hiari na kwa idhini yake. Kauli hii ina uhusiano wa karibu na suala la unyanyasaji wa kingono ambalo ni suala linaloendelea nchini Kenya. Thaker (2025) anafafanua kuwa umri wa wastani wa wasichana kufanya ngono kwa mara ya kwanza ni miaka 11.7 (chini ya miaka 12), na karibu asilimia 100 ya matukio hayo hayakuwa kwa hiari wala kutakikana. Mara nyingi matendo hayo husababishwa kwa kulazimishwa na wanaume wakubwa kwa umri. Wakati mwingine, watoto hawa hawajui kuwa wanaweza kusema neno kama vile: *hapana* au hawakujua jinsi ya kusema *hapana*, mara nyingi kutokana na utamaduni wa kijamii wa kumtii mtu mzima bila kujali matokeo ya vitendo au maamuzi. Maichuhie (2025) naye anaripoti kuwa watoto wa kiume pia wananyanyaswa kingono kwani mwaka wa 2020, serikali ilibaini kuwa wanaume zaidi ya mia mbili walidhulumiwa kingono jijini Nairobi, 121 wakiwa chini ya 11 huku 87 wakiwa kati ya mika 12 na 17.

Kwa mujibu wa Wangamati na wenzake (2019), unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto nchini Kenya unachangiwa na masuala ya maendeleo pamoja na ukosefu wa usawa wa kiuchumi, kijamii na kijinsia. Mambo haya ni pamoja na shinikizo la rika, matumizi ya dawa za kulevya na vileo, uyatima, umaskini, ushawishi wa mitandao ya kijamii, utamaduni wa ukimya kuhusu masuala ya ngono, na tofauti kubwa za kijinsia. Thaker (2025) anabainisha kuwa msichana mmoja kati ya watatu wa umri wa miaka 19 nchini Kenya ni mjamzito au tayari ana mtoto. Pia, kuna uwezekano wa mara tatu zaidi wa wanaume nchini Kenya kujiua ikilinganishwa na wanawake.

Aidha, vipindi kuhusu haki za watoto huweka msingi wa kuwasaidia watoto kuelewa kuwa wanapaswa kujihisi salama, kuheshimiwa, na kuwa na uwezo wa kukataa jambo lolote linalowahusu kimwili. Kauli ya: *...usinishike bila ridhaa…* pia inalenga kulinda watoto dhidi ya aina mbalimbali za unyanyasaji wa kimwili na kingono. Kwa kuwaelekeza kwamba hawapaswi kushikwa nywele au ngozi bila ridhaa yao, watoto wanajengewa uwezo wa kutambua vitendo visivyofaa na kujua kuwa si kila mguso unakubalika, hata kama inafanywa na mtu mzima au anayewajua.

### 4.5.2 Usawa wa Kijinsia

Kibui na Mwaniki (2014) wanabainisha kuwa usawa wa kijinsia ni mchakato wa kuhakikisha haki sawa kati ya wanaume na wanawake kwa kuondoa vikwazo vya kijamii vinavyohujumu usawa huo. Jambo hili ni muhimu kwa maendeleo ya Kenya, hasa katika muktadha wa Dira ya Maendeleo ya 2030. Serikali imeweka mikakati mbalimbali kama vile Sera ya Kitaifa kuhusu Jinsia na Maendeleo ili kuhakikisha usawa wa kijinsia unazingatiwa katika miradi ya kitaifa. Hata hivyo, changamoto kama ukosefu wa usawa wa fursa bado zipo. Kenyatta (2023) anaongeza kuwa katiba ya 2010 ya Kenya ina vifungu vinavyokubali usawa wa kijinsia, ikiwemo kifungu cha 10 kuhusu ushirikishwaji, kifungu cha 27 kuhusu marufuku ya ubaguzi wa kijinsia na kifungu cha 59 kinachoanzisha Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu na Usawa. Vifungu vingine kama 69 vikisisitiza usawa katika matumizi ya rasilimali. Utafiti wa Olubiyi na wenzake (2022) unaonyesha kuwa licha ya mchango mkubwa wa wanawake katika maendeleo ya jamii, wanakumbana na changamoto kama umasikini na ubaguzi.

Vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* vinapeperusha kwa ufanisi kuhusu usawa na ukosefu wa usawa wa kijinsia. Vipindi hivi hutoa taswira yenye uwiano wa changamoto za kijamii zinazowakumba wavulana na wasichana. Kwa mfano:

15 (a). Mwalimu: *Unaenda wapi?*
Kiduchu: *Kwenye useremala. Nataka kutengeneza kigoda.*
Mwalimu: *Ulishaona wapi wasichana wanajifunza useremala. Wasichana kazi zao ni jikoni tu na wavulana ni useremala…*
(Ubongo Kids Kiswahili 2018c, 2: 16 – 2:28)

Mazungumzo haya kwenye dondoo la 15 (a) yanaonyesha changamoto ya kijinsia inayohusiana na ubaguzi wa majukumu katika jamii, ambapo kazi na nafasi fulani

zinaaminika kuwa ni za jinsia moja pekee. Ahmed na Wahab (2014) wanaeleza kuwa jinsia ya kiume imepewa kipaumbele katika vipindi vya watoto. Mwalimu anamzuia Kiduchu (msichana) kujifunza useremala kwa hoja kwamba ni kazi ya wavulana, huku akisisitiza kuwa kazi ya wasichana ni jikoni pekee. Wavulana nao wanahimizwa kuchukua majukumu ya uongozi au kufuata kazi za kiufundi, wakati wasichana wanakatishwa tamaa kuingia katika nyanja hizi. Hizi ni changamoto za kijinsia zinazotokana na mitazamo ya kijadi na dhana potofu zinazoweka mipaka kwa wanawake na wasichana katika kujiendeleza kitaaluma au kimaisha. Inazuia usawa wa fursa na haki ya kuchagua taaluma. Hivyo, fikra kama hizi huendeleza ubaguzi na kudumaza maendeleo ya kijinsia na kijamii. Mazungumzo haya yanashadidiwa na mawazo ya Opunde na wenzake (2018) wanaosema kuwa masuala ya kijinsia na kiuana ndizo changamoto zinazoikumba jamii ya kisasa.

Aidha, kadri jamii inayvobadilika ndivyo majukumu yanazidi kubadilika. Kidenda (2006) anasisitiza kuwa vipindi vya televisheni vina ushawishi wa kijamii kwa watoto kuhusu mitazamo yao ya majukumu ya kijinsia. Kazi zilizoaminika kuwa za wasichana na wavulana haina mipaka katika dunia ya sasa. Wanaume wengi wanafanya kazi zilizotengewa wanawake, huku wanawake nao wakifanya kazi zilizoaminika kuwa za wanaume. Kwa mfano:

15 (b). Mwanafunzi 1: *…Kwa kweli unajua kupika mpaka tunaacha tunachokifanya hadi tunakuja kuona unachokipika…*

Koba: *Kwenye mapishi Koba ndiye mwenyewe yaani. Yaani baba na Mama wanafurahi nikipika, sanasana wakitoka kazini wamechoka wakirudi nyumbani wanakuta chakula kitamu kinawasubiri…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2018c, 3:50 – 4:06)

Kutokana na dondoo hili la 15 (b), Koba, ambaye ni mvulana, anajivunia ujuzi wake wa kupika na anapata pongezi kutoka kwa wazazi wake. Jambo hili linaonyesha kuwa majukumu ya nyumbani yanaweza kufanywa na jinsia yoyote bila ubaguzi. Hivyo, mitazamo ya kijadi kuhusu kazi za kike na kiume inabadilika na jamii inaanza kukubali usawa wa kijinsia katika kugawana majukumu ya kila siku.

Kazi kama vile ya udereva pia inaaminika kuwa ya wanaume. Pia wanaosubiri gani kwenye baraste wanashangaa kuona mwanamke ni dereva baada ya leseni yake ya udereva kuanguka kwenye lami:

> 15 (c). …*Sijawahi kumwona mtu kama huyo*! *Tangu lini mwanamke akaendesha bajaji? Hizo kazi ni za wanaume bwana (kicheko)...*
> (Ubongo Kids Kiswahili, 2018c, 8:25 – 8:35)

Dondoo hili la 15 (c) linaonyesha changamoto ya mitazamo ya kijinsia na dhana potofu zinazoweka mipaka kwa wanawake kushiriki katika kazi ambazo zimezoeleka kufanywa na wanaume. Kauli ya mshangao na kicheko inaonyesha unyanyapaa na dharau dhidi ya wanawake wanaojitosa katika taaluma zisizo za kawaida katika jamii, kama vile kuendesha bajaji. Dondoo hilo la 15 (c) linaonyesha kuwepo kwa upinzani na mtazamo hasi kutoka kwa baadhi ya watu kuhusu kubadilika kwa majukumu ya kijinsia. Mitazamo hasi inaweza kuwakatisha tamaa wanawake wanaojaribu kuvunja vikwazo na kuchukua nafasi katika sekta zisizo za kawaida kwao. Upinzani huu wa kijinsia unadhihirisha hitaji la kuelimisha jamii kuhusu usawa wa kijinsia na umuhimu wa kuruhusu kila mtu (bila kujali jinsia) kufanya kazi au taaluma yoyote kulingana na uwezo na mapenzi yake.

Licha ya changamoto anayopitia mwanamke, vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* humpa matumaini ya kujikomboa na kupigania hali yake na wale watakaomsaidia kufaulu. Kwa mfano:

> 15 (d). Kiduchu: *Hongera sana Uncle T, nimependa ujasiri wako na nimejifunza kweli hata Twiga wa kiume anaweza kusimamia shule ya kulelea watoto. Siyo wa kike tu ambao wanaweza kulea watoto.*
> Unclce T: *Hakuna kazi ya mnyama fulani pekee au kazi ya jinsia fulani kila mtu au kila mnyama anatakiwa afanye kazi anayoiweza na anayoipenda.*
> Kiduchu: *Na mimi napenda somo la useremala lakini naambiwa ni kazi ya wavulana*
> Uncle T: *Hamna kitu kama hicho. Unajua maendeleo mengine hayapo au yanacheleweshwa kwa sababu hatuwapi wavulana na wasichana fursa sawa. Inabidi wote wapewe fursa sawa ili kukuza uwezo wao na kukuza vipaji vyao…*
> (Ubongo Kids Kiswahili, 2018c, 11:12 – 11:50)

Dondoo hili la 15 (d) linaonyesha jinsi Kiduchu, ambaye ni msichana, anazinduka kimawazo kuhusu mgawanyo wa majukumu na kazi katika jamii kulingana na jinsia. Awali, Kiduchu alikuwa ameaminishwa kuwa kazi kama useremala ni ya wavulana pekee. Kupitia mazungumzo yake na Uncle T, Kiduchu anaanza kuelewa kuwa kazi yoyote inaweza kufanywa na mtu yeyote bila kujali jinsia. Anaelewa kuwa uwezo na vipaji havipaswi kuzuiliwa kwa misingi ya jinsia. Uncle T anampatia msukumo wa kufikiri kwa upana zaidi kwa kusisitiza umuhimu wa kutoa fursa sawa kwa wote ili kuleta maendeleo na kuendeleza vipaji. Hivyo, mabadiliko haya ya fikra kwa Kiduchu yanaonyesha mwanzo wa ukombozi wa kijinsia na ujasiri wa kuvunja vikwazo vya kijadi.

Kulingana na Mboya (2018), jamii pana inatiwa changamoto jinsi watakavyohusiana na mwanamke aliyezinduka. Hii ni kwa sababu kadri muda unavyosonga, ndivyo mwanamke wa kisasa anapata uwezo wa kushiriki mambo anuwai yanayohusu maisha yake. Katika jamii nyingi za Kiafrika, ubabedume hutawala, na mwanamke husawiriwa kama kiumbe dhaifu anayepaswa kutegemea mwanaume. Aidha, vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* huwasilisha mada zake (kama vile usawa wa kijinsia) kwa njia ya kufurahisha na kuelimisha. Vipindi hivi huzingatia mbinu alizopendekeza Sabido (2003), ambaye alisisitiza matumizi ya vipindi vya burudani kama zana ya mabadiliko ya kijamii kupitia elimu burudani.

## 4.6 Maarifa ya Kidijitali

Kwa maendeleo bora ya mtoto, elimu ni ya muhimu. Katika enzi hii ya utandawazi, sayansi na teknolojia zimeendelea kwa kiwango kikubwa kiasi kwamba ni nadra kufikiria sekta yoyote ya elimu bila Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Maarifa ya Kidijitali ni sehemu muhimu ya TEHAMA, kwani huwasaidia watoto kuelewa matumizi ya teknolojia na kuwasiliana kwa ufanisi katika nyanja hii. Uelewa huu unawaandaa watoto kushiriki kikamilifu katika dunia ya kisasa ya kidijitali. Katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*, maarifa ya kidijitali inayopeperushwa inahusiana na usalama mtandaoni.

### 4.6.1 Usalama Mtandaoni

Weru na wenzake (2017) wanadai kuwa mtandao umejaa maudhui na shughuli zinazowaburudisha na kuwaelimisha watoto. Mamilioni ya watoto wanatumia mtandao na kubadilishana barua pepe na ujumbe mfupi na kuvinjari mtandao mpana wa dunia. Masuala yanayohusu usalama wa mitandao, ulaghai mtandaoni na ulinzi wa watoto yameongezeka kwa kiasi kikubwa. Nao Humphrey na wenzake (2023) wanaweka wazi kuwa watoto wanakabiliwa na ongezeko la hatari mtandaoni, jambo linalochochea juhudi za kuboresha uelewa wa kidijitali na elimu ya usalama mtandaoni. Vijana huripoti kuhisi kutokuwa salama mtandaoni. Hili hutokana na maudhui ya kuhuzunisha na ugumu wa kuondoa yaliyomo kwenye mtandao. Matatizo wanayokumbana nayo vijana ni pamoja na picha au video za kikatili au za kuchukiza. Video au picha hizi hulenga mtu au kikundi kwa sababu ya jinsia, rangi, au utambulisho wa kijinsia. Kadiri matumizi ya mtandao kwa watoto na vijana yanavyozidi kuongezeka, ndivyo pia wasiwasi kuhusu usalama wao mtandaoni unavyozidi kuongezeka. Katika muktadha wa mawasiliano ya kisasa, watoto huwekwa wazi kwa dhana ya intaneti. Hili hufanyika kwa kuelekezwa kuhusu matumizi yake yenye manufaa, hasa kwenye vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*. Kwa mfano:

> (16). …*Chagua nini cha kuweka ambacho hakina madhara, usiweke chochote, kisicho na heshima. Unachoposti chaweza umiza hisia za wengine…Usiweke chochote usichoweza kufanya hadharani, utawajibika na utendacho mtandaoni. Nyayo za kidijitali, kila mahali unaziacha…*
>
> (Ubongo Kids Kiswahili 2019b, 0:47- 1:14)

Kutokana na dondoo hili la (16), watazamaji huelimishwa na kuonywa kuwa wanapaswa kumakinika kwa kile wanachofanya, kuandika, na kupakia mtandaoni. Hii ni kwa sababu kila kitu kinaacha nyayo ya kidijitali mtandaoni. Nyayo hizi humwezesha mtu mwingine kumfuatilia na kumjua mtu mwingine kiurahisi. Tofauti na nyayo zingine, inakuwa vigumu kufuta nyayo za mtandaoni. Kile ambacho mtu anachapisha mtandaoni kina faida na hasara. Hivyo, watu wanapaswa kuchagua ni nini wanafaa kuweka mtandaoni. Intaneti ni kama uwanja wa dunia nzima, kwani kile mtu anachapisha mtandaoni kinaweza kutazamwa na wazazi, walimu, na marafiki zetu. Aidha, watazamaji wanajifunza umuhimu wa kutumia intaneti kwa uwajibikaji. Pia, wanajifunza kuhusu madhara ya kushiriki taarifa binafsi na umuhimu wa kudumisha faragha mtandaoni.

# SURA YA TANO

# MBINU ZINAZOTUMIWA KUWASILISHA MASUALA IBUKA KATIKA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS*

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ilibainisha matokeo ya lengo la pili la utafiti kwa kuangazia mbinu mbalimbali zinazotumika kuwasilisha masuala ibuka. Sura hii ilitumia Nadharia ya Elimu Burudani ya Sabido (2003) ili kubainisha mbinu za kifasihi katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*. Mbinu zilizobainishwa katika sura hii ni kama vile matumizi ya picha, vichekesho, lugha rahisi, nyimbo, mazungumzo na mazingira yanayofahamika kwa watoto. Mbinu hizi hutumika kuwasilisha hoja kwa njia shirikishi.

## 5.2 Uchambuzi wa Mbinu za Kifasihi

Naru na wenzake (2024) wanaeleza kuwa matumizi ya mbinu za kifasihi hufanya vikatuni kuwa njia bora ya usimulizi. Pia, mbinu za kifasihi huruhusu mada changamano kama vile utambulisho na uhalisia wa maisha ya kila siku kuchunguzwa. Mbinu hizi husaidia kuimarisha maudhui, kuvutia hadhira, na kuchochea ushawishi wa kihisia au kiakili kwa watazamaji.

### 5.2.1 Maelezo ya Picha na Michoro ya Rangi

Kazi nyingi zinazolenga watoto huwa na vielelezo na picha tena zenye rangi (Malugu, 2022). Vielelezo na picha havitumiki kama mapambo tu katika kazi za watoto, bali ni sehemu ya kimakusudi inayotumika kufikisha ujumbe na kuvutia hadhira. Michoro na picha huwavutia na kuwashawishi watoto ili waweze kutazama vipindi husika. Vielelezo pia huwamakinisha watazamaji na kuwafanya kutosahau kwa urahisi kile walichokitazama na kukihusisha na ulimwengu halisi. Aidha, Cass (1967) anadokeza kuwa uwezo wa mtoto kuelewa na kufasiri picha na vielelezo unatokana moja kwa moja na kiwango chake cha maendeleo ya kitabia, ambacho kwa kiasi kikubwa kinategemea umri wake. Katika mazingira ya kisasa, kuna ongezeko wa vyombo vya habari (kama vile televisheni na vitabu vya picha) ambavyo vinatumia vielelezo kama mbinu ya mawasiliano. Vielelezo huwa rahisi kueleweka kwa watoto kwa sababu vinashughulika moja kwa moja na hisia zao za kuona, ambazo huchangia kwa kiwango kikubwa katika mchakato wa kujifunza. Tazama kielelezo cha #1:



Kielelezo cha #1, Umuhimu wa Lishe Bora **(**Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 0:39)

Watazamaji kwenye vipindi vya *Ubongo Kids* hujifunza kuhusu lishe bora kupitia picha zenye rangi zinazoonyesha vyakula vya afya kama matunda, mboga, maziwa na nafaka. Vielelezo hivi, kama ilivyo katika kielelezo cha #1, huwasaidia kutofautisha kati ya chakula chenye virutubisho na chakula kisicho na faida mwilini. Hivyo vinahamasisha ulaji wa vyakula bora kwa afya njema. Cass (1967) kwa upande wake anasisitiza kuwa michoro na vielelezo katika kazi za watoto inapaswa kubuniwa kwa uangalifu ili kusaidia mtoto kufahamu kwa kina ujumbe wa hadithi. Cass anabainisha kuwa rangi zinazotumika katika picha zina jukumu muhimu la kuvutia na kushikilia umakini wa watoto.

Vilevile, katika enzi ya kidijitali, vielelezo vinasaidia watoto kuelewa hatari zilizopo mtandaoni. Hatari hizi ni pamoja na kuwasiliana na watu wasiowajua au kushiriki taarifa binafsi. Watazamaji pia huelezwa jinsi mawasiliano au faili zao huweza kusambazwa mtandaoni kama ilivyo kwenye kielelezo cha #2.



Kielelezo cha #2, Usafirishaji wa faili Mtandaoni **(**Ubongo Kids, 2021a, 1:06)

Kupitia michoro na mifano rahisi, (kama ilivyo katika kielelezo cha #2), huonyesha jinsi faili (kama hati au picha) zinavyosafirishwa kati ya vifaa kama simu na kompyuta. Mbinu hizi za wanazotumia wanaobuni vipindi vya *Ubongo Kids* kufanikisha elimu kupitia burudani (Brown, 2017). Mtazamaji hujifunza kuwa taarifa zao zinaweza kusambaa kwa urahisi mtandaoni. Hivyo ni muhimu kuwa makini kabla ya kushiriki chochote. Picha na mchoro kama huo husisitiza umuhimu wa kutumia nywila salama na watazamaji kutowasiliana na watu wasiowajua mtandaoni. Pennell (2014) anadai kuwa kazi yenye vielelezo vya picha hutumika kama chombo muhimu cha kuwapa watoto fursa ya kujadili na kuchambua mambo magumu ya maisha ya kila siku. Kwa kutumia picha za kuvutia, watoto hupata hamu ya kutaka kujua uhusiano kati ya yanayotazamwa na mazingira halisi.

Pia, mabadiliko ya tabianchi huonyeshwa kwa kutumia picha. Tazama kielelezo cha #3:



Kielelezo cha #3, Mabadiliko ya Tabianchi (Ubongo Kids Kiswahili, 2021c)

Picha ya moto porini hutumika kama mbinu ya kuelezea athari za mabadiliko ya tabianchi. Picha hii kwenye kielelezo cha #3 huibua hisia za hofu na tahadhari kwa sababu inaonyesha hali halisi inayoweza kutokea katika mazingira. Kwa watoto, kuona picha ya moto porini huwasaidia kuhusisha dhana tata ya mabadiliko ya tabianchi na maisha yao ya kila siku. Badala ya kuiona kama jambo lisilowezekana, wanatambua kuwa ni hali inayoweza kuathiri misitu wanayoifahamu, wanyama wanaowapenda, na hewa wanayopumua. Hivyo, picha hii inakuwa chombo cha kielimu na cha kihisia kinachowasaidia kuelewa na kujihusisha moja kwa moja na changamoto za mazingira.

Pia, picha zinazohusiana na kufanya usafi wa mazingira huwaelekeza watoto kuwajibikia mazingira yao. Tazama kielelezo cha #4:



Kielelezo cha #4, Usafi wa Mazingira (Ubongo Kids Kiswahili, 2021c)

Picha za watoto au jamii wakishiriki katika shughuli za kusafisha mazingira hutumika kama mbinu ya kufundisha na kuchochea vitendo vya kimaadili (kama ilivyo katika kielelezo cha #4). Picha hizi hubeba ujumbe unaoonyesha uwajibikaji wa pamoja na athari chanya za kulinda mazingira. Kutazama picha hizo huwasaidia watoto kuhusisha juhudi kama kuokota taka na faida kama vile mazingira safi. Kwa maoni ya Boyd (2015), michoro ya picha hutumiwa kueleza maana ya maandishi na kukamilisha vikatuni kwa njia ya kuona. Kwa njia hii, picha inabadilika kutoka kuwa maelezo ya kinadharia hadi chombo cha vitendo kinachoonyesha kwamba kila mtu anaweza kuchangia kupunguza athari za uchafuzi wa mazingira.

Kwa mtazamo wa Ngugi (2016), kazi ya fasihi huwa na jukumu la kumuelimisha mtoto. Watoto wanapochunguza michoro pamoja, wanaweza kuona mambo ambayo mtu mmoja peke yake angekosa kuyaona. Zaidi ya hayo, michoro huwapa watoto fursa ya kufanya uchambuzi wa kina. Hii ni kwa sababu michoro huvutia watoto na husaidia kukuza uwezo wao wa kufikiria kwa kina kuhusiana na maudhui yanayolengwa.

### 5.2.2 Vichekesho

Kwa mujibu wa Naru na wenzake (2024), vichekesho hufanya vikatuni kuwavutia watoto. Masuala yanayoibuka (kama vile mabadiliko ya tabianchi, usalama wa kidijitali, changamoto za afya ya umma na usawa wa kijinsia) huweza kuwa magumu kwa watoto kuyaelewa kwa kutumia mbinu za moja kwa moja za kufundisha. Ucheshi

katika vipindi vya watoto unatoa fursa ya kuburudisha na kuelimisha (Sabido, 2003). Vipindi vinavyotumia mbinu za ucheshi havifurahishi tu, bali pia hutoa mafunzo kwa watoto na kuhamasisha mabadiliko chanya katika jamii.

Kwa mfano, vichekesho katika ***Mwizi wa Ndizi*** vinatokana na mazungumzo na hali za kushangaza ambazo uhusiana na maisha ya watoto ya kila siku (Ubongo Kids Kiswahili, 2014b, 1:53- 8:25). Katika kisa hiki cha kuchekesha, Kiduchu anaahidi kurejesha ndizi tatu alizopewa na Koba kabla ya kufuturu, lakini badala ya kutekeleza ahadi hiyo, anatumia ujanja kwa kumshawishi Mzee Kigo ampe ndizi nyingine. Akiwa njiani, anateleza kwenye gogo la mti na kuanguka. Ndizi inaruka na kunaswa na Ngedere aliyekuwa juu ya mti. Ngedere anamwekea masharti ya kupewa pilau ili amrudishie ndizi, akisisitiza kuwa wanyama pia hupenda vyakula vingine kando na ndizi.

(17). Kiduchu: *Ah! Unauza ndizi*
Ngendere: *Kwani unataka ndizi ngapi?*
Kiduchu: *Mimi nataka ndizi saba, bei gani?*
Ngendere: *Aaah…Chukua ndizi halafu wewe uniletee pilau*
Kiduchu: *Unataka pilau ya nini? Si Ngendere wanapenda ndizi tu*
Ngendere: *Aaah! Mimi nilijua, shida ya binadamu mnadhani sisi Ngendere tunapenda ndizi tu.*
(Ubongo Kids Kiswahili 2014b, 4:08- 4:31)

Mazungumzo ya Ngendere kwenye dondoo la (17) yanaonyesha kupinga wazo kwamba watu wa jamii au jinsia fulani wanapenda au wanapaswa kuwa na kitu fulani pekee. Ngendere analalamika kuhusu *shida ya binadamu* ambao wanaamini wanyama kama yeye wanapenda ndizi tu. Hii ni kejeli inayodhihaki tabia ya binadamu ya kuwa na fikra zilizopitwa na wakati au zisizobadilika kuhusu wengine. Pia, mazungumzo haya yanaonyesha mabadiliko katika jamii ambapo wanyama wanabadilisha mitindo ya maisha na kuanza kula pilau badala ya ndizi. Kisa hiki kinasisitiza umuhimu wa usawa kwa wote na uvunjaji wa dhana potofu katika nyanja zote za maisha.

Pia, mabadiliko ya tabianchi yanatolewa kwa njia ya ubunifu na burudani kupitia mhusika anayejulikana kama Mama Ndege anayeeleza mabadiliko ya tabianchi (Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 4:48-6:13). Mama Ndege hutekeleza wajibu wa

kuelimisha kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia isiyo ya kawaida. Mama Ndege huongea akiruka angani huku akitumia sauti ya kuchekesha na ya kuvutia watoto. Kwa mfano:

> (18). *…Tabianchi inabadilika katika dunia nzima lakini inaathiri hali ya hewa kwenye maeneo tofauti kwa namna tofauti…*

Uwasilishaji wa Mama Ndege kwenye dondoo la (18) unaonekana kuwa wa kipekee kwani anachanganya ucheshi na elimu. Hili linafanya ujumbe wake kueleweka kwa urahisi kwa hadhira ya watoto. Aidha, ucheshi unawasaidia watoto kuelewa mambo magumu kwa njia rahisi, huku ukifanya ujumbe kuwa wa kuvutia na rahisi kukubalika.

### 5.2.3 Mazungumzo

Mazungumzo ni chombo muhimu cha kupitisha elimu katika vipindi vya televisheni vya watoto, hasa vinaposhughulikia masuala yanayoibuka kama vile utunzaji wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi, afya ya umma, na haki za kijamii. Ali na wenzake (2024) wanasema kuwa mazungumzo, hasa inayotumia lugha sahili husheheni kwenye vikatuni. Mazungumzo haya hutumika kuwasilisha maadili na kuchochea ujifunzaji. Tofauti na masimulizi ya kinadharia au mbinu za kufundisha za moja kwa moja, mazungumzo haya kwenye vikatuni huleta elimu hai kupitia mwingiliano kati ya wahusika. Mbinu hii ya mazungumzo inaakisi mawasiliano ya maisha halisi. Hii huwezesha watoto kufuatilia, kuelewa, na kuelekeza dhana mpya kwa urahisi. Naru na wenzake (2024) pia wanaeleza kuwa vikatuni huvutia hadhira kwa kutumia mazungumzo, hali inayoweza kuunda uhusiano wa kudumu kwa vizazi mbalimbali. Kwa mfano:

> (19). Kiduchu: *Wasichana na wavulana tupo tofauti kijinsia lakini hatupo tofauti kiuwezo au katika vitu tunavopenda kufanya hivyo tuna haki ya kupata fursa sawasawa.*
>
> Wanafunzi: *Kweli, tuna haki ya kuishi maisha ya furaha.*
>
> (Ubongo Kids Kiswahili, 2018c, 12:35- 12:49)

Kupitia mazungumzo yake na wanafunzi wenzake kwenye dondoo la (19), Kiduchu anasisitiza haja ya kila mtu kupata haki sawa. Kiduchu anasisitiza kwamba ingawa kuna tofauti za kibayolojia kati ya wasichana na wavulana (yaani jinsia), hawatofautiani katika uwezo wao wa kufikiri, kufanya kazi au kufanikisha mambo. Wasichana na wavulana wanaweza kufanya na kupenda mambo kama vile michezo, masomo na

sanaa. Kwa hivyo, Kiduchu anadai kuwa wote wanapaswa kupewa fursa sawa bila ubaguzi wowote wa kijinsia. Wanafunzi pia wanakubaliana na Kiduchu na wanasisitiza kwamba kila mtoto, bila kujali jinsia au hali yake, ana haki ya kuishi maisha yenye furaha.

Mazungumzo katika vipindi vya vikatuni yana uwezo wa kuwasilisha elimu katika muktadha wa maisha kwa kutumia lugha sahili (Ali na wenzake, 2024). Wahusika wanapojadili au kukumbana na tatizo (kama vile kujilinda mtandaoni), watazamaji huonyeshwa changamoto na suluhisho kwa njia ya asili inayoweza kuhusishwa na maisha yao. Mazungumzo haya hufanyika kwa njia ya burudani inayolenga kuwafunza watazamaji kuhusu suala linaloathiri jamii (Sharma 2023). Zaidi ya hayo, mazungumzo huimarisha fikra za kina hasa kuhusu jambo linalozungumziwa.

### 5.2.4 Matumizi ya Lugha sahili

Kahigi (2021) anaeleza kuwa lugha inayolenga watoto inapaswa kulingana na kiwango chao cha uelewa. Msamiati unaotumiwa unapaswa kuwa rahisi kueleweka kulingana na umri. Wahiga (2003) anafafanua kuwa lugha hutumia maneno ambayo hutumiwa na watu wanapowasiliana katika maisha ya kila siku. Maneno haya yanapaswa kupangwa kwa mpangilio maalum ili yaweze kueleweka vizuri na kufikisha maana kamili.

Lugha inayotumika katika vipindi vya *Ubongo Kids* imeundwa kwa umakinifu ili iwafae watoto kulingana na umri wao na kiwango chao cha uelewa. Kwa mfano:

20 (a). *...Shikamoo baba na mama… Marahaba mwanangu… leo ni siku ya kuogelea….*

(Ubongo Kids Kiswahili 2021c, 0:40- 0:0:46)

Kwa mujibu wa dondoo la 20 (a), maneno kama vile: *shikamoo* na *marahaba* ni salamu za kila siku ambazo huwa na muundo rahisi. Sentensi zimetumiwa kwa ufupi, zikiwa wazi na rahisi kueleweka. Kauli kama: *leo ni siku ya kuogelea,* ni tamko la taarifa moja linalotumia maneno machache bila virejeshi au vishazi changamano. Matumizi ya sentensi sahili katika dondoo hili huchangia kueleweka kwa ujumbe kwa haraka na kwa urahisi kwa hadhira lengwa. Msamiati katika vipindi vya *Ubongo Kids* hutokana na lugha ya mazungumzo ya kila siku wanayoifahamu watoto. Watoto humakinika na

kuhusishwa moja kwa moja na maudhui yanayowasilishwa kupitia matumizi ya lugha sahili.

Matumizi ya lugha sahili katika vikatuni vya *Ubongo Kids* pia hutoa fursa kwa vipengele vya lugha vinavyowavutia watoto kama vile marudio ya maneno, vina, na maswali ya moja kwa moja kwa watazamaji. Tazama dondoo la 20 (b):

20 (b). *Eti tatizo ni kubwa, huwezi fanya lolote*
*Ila ni juu yako, ikitokea chochote*
*Lazima tupambane kwa pamoja, kila saa….*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2021c, 34:15-34:29)

Kwa mujibu wa dondoo la 20 (b), matumizi ya maneno kama: *tatizo, huwezi, chochote,* na *tupambane,* ni ya kawaida na yanayoeleweka kwa urahisi kwa watazamaji, hasa watoto. Vina hufanya mistari isomeke au iimbike kwa mdundo wa kuvutia. Mdundo huu huongeza mvuto wa vipindi na kufanya wasikilizaji wavutiwe kutazama kipindi husika hadi tamati ili wajifunze (Sabido, 2003). Mbinu hii huondoa vizingiti vya lugha na kuhakikisha kuwa elimu inayopeperushwa inawafikia watazamaji. Kwa kuwa watoto hujifunza kwa kuiga na kupitia muktadha wa kusikia mara kwa mara, urahisi wa lugha huongeza uwezekano wa kufahamu na kukumbuka dhana muhimu (Njiiri na wenzake, 2018). Mbinu hizi hujenga msingi thabiti wa maarifa huku zikiendeleza usikivu na umakini kwa njia ya kufurahisha.

### 5.2.5 Nyimbo

Mulokozi (1996) alifasili wimbo kama kitu kinachoimbwa na kuleta dhana kuwa wimbo hujumuisha tanzu nyingi kama vile hadithi. Mulokozi anaendelea na ufafanuzi wake wa wimbo na kusema kuwa nyimbo hutambulishwa na vitu muhimu kama vile muziki, sauti ya mwimbaji, maneno yanayoimbwa na hadhira inayoimbiwa. Naye Mazigwa (1991) alieleza wimbo kama kifungu cha maneno yaliyopangwa kwenye utaratibu maalum ili kutimiza mapigo ya muziki na hutumia lugha ya mkato. Mara nyingi, nyimbo huwa fupi na huwa na ubeti mmoja wenye mistari mitatu. Kwa kuwa nyimbo huchochea hisia, mara nyinyi hutumiwa kama mbinu ya kuwahamasisha watu kutenda jambo fulani. Pia, nyimbo hutumika kama mbinu mwafaka wa kurithisha utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nyimbo katika sampuli teule zilifanikisha shughuli mbalimbali katika vipindi mbalimbali. Shughuli hizi zinahusiana

na usafi na uhifadhi wa mazingiriza, mabadiliko ya tabianchi na usalama mtandaoni. Pia shughuli hizi zinahusiana na usawa wa kijinsia, Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati na ulinzi wa watoto.

#### 5.2.5.1 Wimbo unoambatana na Shughuli za Usafi na Uhifadhi wa Mazingira

Nyandwaro na Malugu (2024) wanabainisha kuwa uhifadhi wa mazingira unahusu utunzaji wa mimea na wanyama dhidi ya uharibifu wowote. Nayo kwa mujibu wa Katiba ya Kenya (2010) sura ya tano kifungu cha pili, kila mtu anapswa kushirikiana na serikali ili kutunza mazingira na kuendeleza maendeleo endelevu kielkolojia. Kulingana na Mosha na Omari (2023), mazingira dhana ya mazingira hujitokeza katika nyimbo za watoto. Dhana ya mazingira huwahusisha watoto na mazingira yao ili wawe na uhusiano wa karibu na wa kudumu. Nyimbo hizi huwatia watoto hamu ya kuchunguza masuala ya mazingira na kulinda mazingira yao.

Kwa mfano, wimbo kuhusu usafi kama ufuatao unaweza kuwafunza watoto kuhusu mazingira:

(21). *Usafi, usafi,*
*Usafi wa mazingira,*
*Shirikiriana nasi, kuzuia maradhi,*
*Okota takataka,*
*Saidia jamii.*

*Taka ziko za aina mbalimbali,*
*Plastiki na glasi zilizo ardhini,*
*Karatasi, majani na vitu vilivyooza,*
*Zaleta mende, panya na nzi,*
*Okota takataka*…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2018a, 0:28-0:55)

Wimbo kwenye dondoo la (21) unafanikisha shughuli za usafi wa mazingira. Wimbo huo unalenga kuwaelimisha watoto kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi katika mazingira yao ya kila siku kwa kushirikiana kama jamii. Kwa kutumia lugha rahisi, inayojirudia na yenye mdundo wa kuvutia, wimbo huu huwasilisha ujumbe kwa namna ambayo watoto wanaweza kuelewa kwa urahisi na kuukumbuka. Mawazo haya yanashadidiwa na Naru na wenzake (2024) anayeeleza kuwa vikatuni huvutia hadhira kwa kutumia muundo wa usimulizi unaoeleweka kwa watazamaji.

Mojawapo ya mbinu kuu zinazotumika katika wimbo wa (21) ni urejeleaji wa maneno kama vile: *usafi, usafi* na *okota takataka*, ambayo husaidia kusisitiza ujumbe wa kuondoa uchafu. Kwa mujibu wa Mose na Obuchi (2021), urudiaji wa maneno katika kazi za kifasihi huwa na uwezo wa kuathiri muundo pamoja na dhamira ya kazi husika. Wimbo huu unatumia mbinu ya kishairi na sauti za kurudiarudia ili kuwahamasisha watoto kuhusu wajibu wao katika kujenga maisha bora ya baadaye kwa kuchagua mitindo ya maisha inayohifadhi mazingira. Monaghan na Rowson (2008) wanaeleza kuwa watoto wanaposisitiziwa maneno, wanaanza kuelewa kinachoendelea katika mazingira yao. Aidha, wimbo huu unaainisha aina mbalimbali za taka kama plastiki, glasi, karatasi, majani na vitu vilivyooza, jambo ambalo linaongeza maarifa ya msingi kuhusu usimamizi wa taka. Mbinu hii huwapa watoto uelewa wa kimazingira tangu utotoni.

Zaidi ya hayo, wimbo katika dondoo la (21) unaonyesha uhusiano wa moja kwa moja kati ya uchafu na magonjwa, kwa kutaja wadudu hatari kama mende, panya na nzi ambao hujitokeza katika mazingira machafu. Kwa hivyo, unasisitiza kuwa kuokota takataka si tu tendo la usafi bali pia hatua ya kuzuia maradhi na kulinda afya ya jamii. Kwa maoni ya Sharma (2023), vipindi vya televisheni vina uwezo wa kuelimisha kando na kuburudisha. Kwa kutumia mbinu za kuvutia na kufurahisha, watoto wanaweza kujifunza namna ya kutunza mazingira kwa njia rahisi na ya kueleweka.

#### 5.2.5.2 Wimbo unaofanikisha Shughuli za Mabadiliko ya Tabianchi

Makwaya na Dick (2014) walibainisha kuwa kuhusisha watoto katika ulinzi na uelewa wa mazingira ni njia mojawapo ya kuibua na kukuza uwezo wao wa kushiriki kupitia wimbo. Morton (2012) anadai kuwa uhusiano uliopo kati ya binadamu na mazingira ni ya kisiombiotiki. Hivyo, uharibifu wa mazingira ni tishio kubwa kwa binadamu. Ikiwa watoto hawataandaliwa mapema, wanaweza kukumbana na changamoto hizi wakiwa na hofu au kukata tamaa. Elimu burudani ni hatua ya kwanza muhimu kupata mafanikio katika kushughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, hasa kwenye vipindi vya watoto (Sabido, 2003).

Vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* hutumia nyimbo ili kufanikisha shughuli za maadiliko ya tabianchi kama ifuatavyo kama inavyodhihirika katika dondoo la (22):

(22). *Maisha bora na afya, tunayayataka (×2)*
*Maisha salama yasiyo na magonjwa, tunayataka (×2)*
*Na tuyatengeneze sasa, na tuyatengeneze sasa (×2)*
*Maisha bora ya kesho wajibu wetu watoto, sio kwa kulaumu au kutoa vilio,*
*Bali chukua hatua na kufanya vitendo (×2)*
*Tumia nishati safi kama sola, maji au upepo badala ya nishati chafu kama mafuta au makaa*
*Kuwa wa kwanza kutangangaza nishati safi, hivyo ndivyo tutapata maisha bora…*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2022, 19:47-20:40)

Wimbo katika dondoo la (22) ni mfano wa jinsi nyimbo katika vipindi vya watoto zinatumiwa kuwaelimisha kuhusu changamoto za kisasa kwa njia rahisi na ya kuvutia. Kando na kuburudisha, wimbo huu unaendeleza afya ya jamii na uendelevu wa mazingira kupitia matumizi ya nishati safi (Sabido, 2003). Wimbo unasisitiza hitaji la *maisha bora na afya*, inayohusu maisha salama yasiyo na magonjwa. Nayo kipengele cha *tuyatengeneze sasa*, kinahamasisha hatua za haraka na kushirikisha watoto kama sehemu ya suluhisho ya matatizo katika jamii. Wimbo huo unabadilisha mtazamo wa kawaida wa kulaumu au kulalamika, na badala yake, kuhimiza watazamaji kuchukua hatua ili watoto waweze kuwajikia jamii na mazingira. Matumizi ya vyanzo vya nishati vinavyohifadhi mazingira inahimizwa kupitia kauli kama: *Tumia nishati safi kama sola, maji au upepo...*. Hatimaye, wimbo huu hukuza uelewa wa watoto kuhusu masuala ibuka kama afya ya jamii, uendelevu wa nishati na majukumu yao katika jamii.

### 5.2.5.3 Wimbo wa Shughuli za Usalama Mtandaoni

Usalama mtandaoni ni suala ibuka katika ulimwengu wa kisasa unaotawaliwa na teknolojia. Mtandao una maudhui na shughuli zinazowaburudisha na kuwaelimisha watoto (Weru na wenzake, 2021). Usalama mtandaoni unahusu hatua na maarifa yanayohitajika ili kujilinda dhidi ya hatari zozote zinazoweza kutokea watazamaji wanapotumia mitandao au vifaa vya kidijitali. Masuala haya hujitokeza kwenye vipindi vya watoto kwa njia ya elimu burudani (Sabido, 2003). Kwa mfano, wimbo ufuatao unaangazia usalama mtandaoni katika kipindi cha *Ubongo Kids*:

(23). *Unaangalia nini, unabonyeza nini*
*Na unaweka nini mtandaoni?*
*Hizi ni nyayo za kidijitali unazoacha mtandaoni,*
*Mtu aweza kufuatilia na kujua wewe ni nani*
*Nyayo za kidijitali,*

*Kila mahali unaziacha,*
*Tofauti na nyayo zingine*
*Ni vigumu kuzifuta…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2019b, 0:08-0:44)

Wimbo huu katika dondoo la (23) unashiria jinsi watoto wanaweza kukuzwa, hata katika umri mdogo kuhusu hatari za mienendo yao mtandaoni. Wimbo unachanganya burudani na elimu kwa ustadi mkubwa, ukitoa mafunzo kuhusu umuhimu wa usalama mtandaoni kwa njia ya kuvutia (Brown, 2017). Wimbo huu unaelezea kwa kina suala ibuka la usalama mtandaoni, ambalo limekuwa muhimu katika maisha ya watoto wa kizazi cha kidijitali. Msingi wa ujumbe kwenye wimbo huu unaanza kwa kuibua swali la moja kwa moja: *Unaangalia nini, unabonyeza nini, na unaweka nini mtandaoni?* Hili ni swali la kutafakari linalolenga kumfanya mtoto afikirie kuhusu mienendo yake ya kidijitali na kumhamasisha mtoto awe makini na awajibike kwa kile anachofanya kwenye majukwaa ya mtandao. Hivyo, wimbo huo unachukua nafasi ya kuwa chombo cha kukuza uelewa wa hatari zilizopo katika matumizi ya mitandao bila tahadhari.

Dhana kuu inayotumika katika wimbo kwenye dondoo la (23) ni ya *nyayo za kidijitali*. Hii ni dhana inayotumika kueleza kwamba kila mtu anaacha alama au historia ya matumizi yake mtandaoni. Humphrey na wenzake (2023) wanaeleza kuwa watoto hukabiliwa na ongezeko la hatari mtandaoni. Ongezeko hili la hatari ni jambo linalopaswa kushughulikiwa ipaswavyo. Tofauti na nyayo halisi zinazoweza kufutwa kwa urahisi, nyayo za kidijitali, kama wimbo unavyosema kuwa: *ni vigumu kuzifuta*. Hii ina maana kwamba kila kinachowekwa mtandaoni kinaweza kubaki huko kwa muda mrefu na kufikiwa na watu mbalimbali. Hivyo, watu wanapaswa kutumia mtandao kwa njia isiyoweza kuleta madhara kwao.

### 5.2.5.4 Wimbo Unaoambatana na Shughuli za Usawa wa Kijinsia

Kidenda (2006) anaeleza kuwa vipindi vya watoto, hasa vikatuni, wakati mwingine husawiri wanaume kama wenye majukumu ya uongozi na wa kufanya maamuzi. Wanawake nao huhimizwa kuwa watiifu na kuwategemea wanaume. Katika fasihi ya kale, majukumu ya kijinsia yalikuwa magumu na yaliyowekwa wazi. Wanaume walionyeshwa kama mashujaa, viongozi na watoa maamuzi, huku wanawake wakichorwa kama watiifu, wenye hisia nyingi au wanaotegemea wengine. Taswira hizi

hazikuonyesha tu mila na desturi za kijamii, bali pia zilizidumisha mitazamo hiyo. Kaula (2015) anasema kuwa mwanamke katika kazi za fasihi kama vile vikatuni, huzidi kubaguliwa. Hata hivyo, kadri uelewa wa kijamii unavyoendelea kukua, fasihi ya kisasa inazidi kukumbatia usawa wa kijinsia. Hali hii inadhihirika katika nyimbo mbalimbali katika vikatuni vya *Ubongo Kids* kama ifuatavyo:

(24). *Kila mtu ana haki ya kuishi maisha ya furaha, afya na usawa,*
*Wasichana na wavulana wanastahili pewa wote fursa sawa,*
*Nani kasema kuna kazi za wasichana na kazi za wavulana*
*Hii sio sawa*
*Wenyewe twaweza badili kanuni zetu,*
*Zisifungwe na jinsia zetu ili kuleta maendeleo endelevu…*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2020b, 0:08- 0:50)

Wimbo huu kwenye dondoo la (24) unaangazia usawa wa kijinsia na jinsi ujumbe huo unaweza kuwasilishwa kwa watoto kwa njia rahisi na yenye mvuto. Katika jamii nyingi, watoto huanza kujifunza kuhusu majukumu ya kijinsia kupitia familia, shule na vyombo vya habari (Mokua, 2024). Mara nyingi, majukumu haya huambatana na mitazamo finyu kama vile: *kazi hii ni ya msichana* au *kazi hii ni ya mvulana*. Wimbo huu unalenga kupinga mitazamo hiyo potofu ya kazi fulani kutengewa jinsia fulani kwa kusisitiza haki, fursa sawa na umuhimu wa kuchangia maendeleo bila ubaguzi wa kijinsia.

Katika mstari wa kwanza kwenye dondoo la (24), wimbo unaashiria kwamba: *Kila mtu ana haki ya kuishi maisha ya furaha, afya na usawa*. Hii ni kauli ya msingi ya haki za binadamu, inayomjumuisha kila mtoto bila kujali jinsia. Kauli hio pia inahimiza mazingira ya haki na usawa kama msingi wa maisha bora kwa wote. Kulingana na Kilonzo (2015), suala la ukombozi wa kijinsia limezidi kuangaziwa katika nyanja za kifasihi. Hata hivyo asasi za kijamii kama vile utamaduni, dini na siasa imezidi kuongeza uwepo wa udhalimu wa kijinsia. Mistari kama: *Wasichana na wavulana wanastahili pewa wote fursa sawa* na *…Nani kasema kuna kazi za wasichana na kazi za wavulana* zinapinga dhana ya kazi au majukumu kulingana na jinsia. Wimbo unashughulikia mitazamo ya kijamii kuhusu jinsia unaoweza kuvunjwa ili kuwezesha kila mtoto kufikia ndoto zake.

Kauli ya: *Hii sio sawa*, kwenye dondoo la (24) ni tamko linalodhihirisha kutoridhishwa na hali ya sasa ya ukosefu wa usawa. Ni tamko la msimamo kuhusu suala la usawa linalofuatwa na kauli ya mabadiliko kama: *Wenyewe twaweza badili kanuni zetu*. Mwisho wa wimbo unahusisha usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu. Hii ni hoja yenye mizizi katika malengo ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa, hasa lengo nambari tano linalohusu usawa wa kijinsia (*United Nations*, 2025). Lengo hili la nambari tano linahusu kufanikisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote. Kutokana na kauli hizi, watoto wanahimizwa washiriki katika kupata suluhisho kwa suala la usawa wa kijinsia kwa kuhoji, kubadilisha mitazamo potofu na kujenga jamii inayotambua nafasi sawa kwa wote. Wimbo huo unasisitiza kwamba kanuni za kijinsia si za kudumu, bali ni mitazamo inayoweza kufanyiwa marekebisho kupitia elimu na mabadiliko ya kijamii.

#### 5.2.5.5 Nyimbo zinazoambata na Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati

Nyimbo zinazoambatana na shughuli za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati za watoto hubuniwa kwa njia rahisi na ya kuvutia. Lengo ni kuwatia watoto hamu ya kuzisikiza na kuwahamasisha kujifunza masomo haya muhimu ya karne ya ishirini na mmoja. Aidha, nyimbo hizo huchochea ushirikiano wa kihisia, jambo ambalo huimarisha ujifunzaji (Kajuna, 2015). Kwa kuwa watoto wengi hutumia muda mwingi kutazama vipindi wanavyopenda kwenye televisheni, vikatuni huruhusu watoto kuwa na habari kuhusu matatizo katika mazingira yao pamoja na kukuza maendeleo ya utambuzi na ujuzi wa kihisia. Kwa mfano:

25 (a). *Hisabati ni kipimo, urefu na upana,*
*Hisabati ni maneno, herufi na matendo, kuongeza na kutoa, hayo ndiyo maisha*
*Nani anabisha, toa, gawanya, halafu zidisha, umepata jibu?*
*Unaona aibu? Acha wewe…*
*Hesabu ni kila kitu hapa duniani*
*Unapokula ugali, unahesabu matonge,*
*Unapotembea, unahesabu hatua…*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2014a, 0:15-0:35)

Wimbo huu kwenye dondoo la 25 (a) unaeleza kwa njia rahisi na ya kuvutia kwamba hisabati ni sehemu muhimu ya maisha ya kila siku ya watoto, hasa mtaala wa umilisi nchini Kenya. Wimbo unapoanza kwa kutaja maneno kama vile: *Hisabati ni kipimo, urefu na upana*, unaonyesha kuwa hisabati hutumika darasani na maarifa yake

yanaweza kutumika katika shughuli halisi kama kupima vitu na kutatua changamoto mbalimbali. Pia, kwa kutumia burudani, wimbo huu unasaidia watazamaji kuelewa kuwa hisabati inahusiana na matendo yao ya kila siku kama vile kuhesabu matonge ya ugali au hatua wanazochukua wanapotembea (Brown, 2017). Hivyo, watazamaji huburudika na kuwa uhusiano wa karibu na somo la hisabati. Hii ni kwa sababu wanaona matumizi yake moja kwa moja katika maisha yao ya kawaida. Uhusiano huu wa karibu unachochea umahiri wa kutatua matatizo na stadi ya kufikiri kwa kina. Stadi hizi ni miongoni mwa stadi kuu zinazolengwa katika mtalaa huo mpya.

Aidha, wimbo kwenye 25 (a) unahamasisha watoto kutokata tamaa au kuaibika kujifunza hisabati. Mstari kama: *Unaona aibu? Acha wewe…* unaondoa hofu au mitazamo hasi kuhusu hisabati. Hii ni mbinu ya kisaikolojia inayowasaidia watoto kuwa na msimamo chanya kuhusu somo hilo, jambo linalofaa sana katika ujifunzaji wa msingi. Zaidi ya hayo, wimbo unatoa mafunzo kuhusu msingi wa ujuzi wa kihisabati kama vile kujumlisha, kutoa, kugawanya na kuzidisha. Haya ni maarifa ya msingi katika mtaala wa umilisi, hasa katika nyanja za sayansi na teknolojia ambapo hesabu hutumika kila wakati (Cheruiyot, 2024). Kwa kutumia lugha inayoburudisha (Sabido, 2003), wimbo unawavutia watoto na kuwasaidia kujifunza bila shinikizo. Kwa hivyo, wimbo huu unatumika kwa lengo la burudani na nyenzo ya kisomi inayotimiza malengo ya elimu na kukuza vipengele vya mtaala wa umilisi.

Mbali na kuelimisha kuhusu hisabati, wimbo pia hutumika kufundisha elimu ya msingi ya sayansi, hasa kuhusu utafiti. Kwa mfano:

25 (b). *Nina maswali, nafanya utafiti,*
*naweka makisio, nafanya jaribio,*
*nakusanya taarifa za matokeo, nakusanya taarifa za matokeo,*
*nataka kuelewa tatizo kutatua, nataka kuelewatatizo kutatua,*
*nakusanya taarifa za matokeo, nakusanya taarifa za matokeo…*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2017a, 0:17- 0:39)

Wimbo huu kwenye dondoo la 25 (b) unahusu udadisi katika sayansi. Wimbo huu unatumika kama mbinu ya kukuza elimu kando na kuburudisha ili kukuza umilisi wa kisayansi unaohitajika kwa mafanikio ya kitaaluma na kimaisha katika mtaala wa umilisi (Sharma, 2023). Ujumbe wa wimbo huo unasisitiza hatua za msingi katika mchakato wa kisayansi ambao ni kiini cha mbinu shirikishi na tendaji zinazolenga

kumwezesha mtazamaji kujifunza kwa kufanya. Maneno kama: *nafanya utafiti, naweka makisio, nafanya jaribio* na *nakusanya taarifa za matokeo* yanaonyesha wazi kuwa mtazamaji anahimizwa kushiriki kikamilifu kutafuta maarifa kupitia uchunguzi wa kitaaluma. Hii ni tofauti na kufundishwa kwa kukaririshwa. Wimbo uliorejelewa unahamasisha mtazamaji kutatua matatizo kwa kutumia mbinu ya kisayansi. Mbinu ya kisayansi huhakikisha matatizo yanashughulikiwa kwa njia ya kimfumo, yenye uthibitisho na isiyoegemea maoni binafsi. Mugaya (2022) anaeleza kuwa wimbo hutumika kufanikisha burudani na kuwasilisha ujumbe. Hivyo, wimbo huwa njia nyepesi ya kufikisha ujumbe kwa watoto kwani huwashirikisha.

Aidha, kupitia marudio, vina, na midundo inayovutia, wimbo huathiri watazamaji kwa kuwaburudisha. Kwa mujibu wa Madoshi (2022), wimbo una uwezo wa kuathiri hadhira kupitia mbinu za kifasihi kama vile majigambo ambayo hupitishwa kupitia mandahari ya kibunilizi. Wimbo katika vipindi vya *Ubongo Kids* ni tofauti na hadithi za picha pekee kwani, unaweza kukumbukwa na kuimbwa nje ya muktadha wa televisheni kama vile darasani, nyumbani, viwanjani, au kwenye matukio ya kijamii. Mafunzo yanayotolewa kupitia nyimbo yanaweza kuendelea kukumbukwa na watoto hata baada ya kipindi kumalizika, na hivyo kuchangia katika kuimarisha tabia na maarifa yao.

#### 5.2.5.6 Wimbo unoambatana na Haki za Watoto

Wimbo katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* huwafunza watazamaji kuhusu haki zao kwa njia ya kusisimua. Wimbo huo pia hutumia lugha sahili ili watoto waweze kuelewa kwa kina. Mara nyingi, wimbo katika vipindi hivi huwa na uradidi ili kusisitiza suala linalolengwa. Kwa mfano:

(26). *Ridhaa yangu ni, na haki yangu ni kusema ndio au hapana,*
*kwa vitu vya kuni, athiri mwilini na ndoto zangu kuzizima,*
*Niombe ridhaa yangu kila saa, naweza badili mara kwa mara,*
*Ridhaa yangu na yako sio sawa,*
*lakini heshimu nikisema hapana…*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2018b, 19:35 – 20:07)

Wimbo huu kwenye dondoo la (26) unahusu umuhimu wa ridhaa na haki ya kujilinda dhidi ya vitendo visivyofaa vinavyoweza kuathiri miili au ndoto za watoto. Watoto wanaelimishwa kuwa wana haki ya kusema *ndiyo* au *hapana* kwa mambo

yanayowahusu, hasa yale yanayohusiana na miili yao. Madoshi (2022) anabainisha kuwa nyimbo huwa na uwezo wa kuathiri hadhira kwa kutumia mandhari ya kibunilizi. Kwa mfano, watoto wanapofundishwa kusema kuwa: *usinishike nywele bila ridhaa, usinishike ngozi bila ridhaa*, wanajifunza kutambua mipaka ya kibinafsi na kuelewa kuwa hakuna mtu anayepaswa kuwagusa bila ruhusa yao. Kauli hii inaashiria kuwa watoto wana haki juu ya maisha yao na kile kinachoendelea katika mazingira yao.

Aidha, wimbo kwenye dondoo la (26) hufanikisha elimu burudani (Brown, 2017). Wimbo huu unawatia watazamaji ujasiri wa kujieleza na kutetea maamuzi yao, jambo linalosaidia kukuza kujiamini na uwezo wa kujitetea katika mazingira mbalimbali. Wimbo huu unasisitiza kuwa ndoto za watoto ni za thamani na lazima walindwe dhidi ya vikwazo. Pia, unafundisha kuheshimu neno kama: *hapana*, na maamuzi ya wengine. Kwa jumla, wimbo huu unatumika kama chombo muhimu cha kuwaelimisha watoto kuhusu haki zao, usalama wa kibinafsi na maadili ya kuheshimiana.

### 5.2.6 Matumizi ya Taswira na Mazingira Yanayofahamika kwa watazamaji

Mazingira yanayofamika huandamana na taswira ambayo M'Ngaruthi (2008) anaieleza kama mbinu ya kifani inayotumiwa na msimulizi wa hadithi ili kumsaidia mtazamaji kuona kwa uwazi kile kinachosimuliwa. Maelezo ya kina humsaidia mtazamaji kufikiria mazingira, wahusika, sauti au milio mbalimbali, pamoja na matukio ya kutisha. Kwa upande wao, Njogu na Chimerah (2011) wanaeleza kuwa taswira ni picha ya mawazo inayojitokeza akilini mwa mtu. Taswira ni mbinu inayotumika na msimulizi kumsaidia msomaji kufikiria hali fulani kwa urahisi na kukielewa kwa kina zaidi.

Kwa mfano:

(27). Mama Ndege: …*Marafiki zangu walikuwa wanapaa kwenye anga la ustaria na waliona moto mkubwa sana msituni. Lakini kwenye sehemu zingine za dunia, marafiki zangu batabuku wameona barafu kaskazini mwa dunia inayeyuka…*

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 5:12- 5:28)

Kwa mujibu wa dondoo la (27), taswira inayojengeka akilini mwa mtazamaji ni ya kimazingira, hasa inayohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Mama Ndege anatumia mazungumzo ya kuburudisha kuelezea matukio makubwa ya kimazingira kama vile

moto wa msituni na kuyeyuka kwa barafu, ambayo ni ishara ya ongezeko la joto duniani. Hivyo, taswira inayojengeka akilini mwa mtazamaji ni ya uharibifu wa mazingira.

Mazingira yanayoonyeshwa katika vikatuni vya *Ubongo Kids* kama vile vijiji, mashambani, mitaa ya mijini, shule za mitaa na sokoni huakisi maisha halisi ya kila siku ya watazamaji wengi. Ili kudhihirisha hali halisi, vipindi hivi hutumia mandhari kama nchi tambarare zilizojaa magogo makavu ya miti. Hii ni ishara ya ukame au uharibifu wa mazingira. Mandhari haya hutumika kama mapambo na nyenzo za kimkakati za kufikisha ujumbe wa mazingira. Aidha, vipindi hivi huwasilishwa kupitia elimu burudani ambayo huwapa watoto mafunzo kwa njia ya kufurahisha (Sharma, 2023). Kwa hivyo, elimu burudani hupeperushwa katika muktadha inayoeleweka na inayoweza kutekelezwa na watazamaji ili kufanikisha lengo la kipindi husika.

# SURA YA SITA

# JINSI USAWIRI WA WAHUSIKA UNAVYOFANIKISHA UWASHILISHAJI WA MASUALA IBUKA KATIKA VIKATUNI VYA *UBONGO KIDS*

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inaonyesha na kujadili matokeo ya lengo la tatu la utafiti huu. Sura hii ililenga kuchunguza jinsi usawiri wa wahusika unavyofanikisha uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Sura hii inatumia nadharia ya Elimu Burudani ya Sabido (2003) ili kufanikisha lengo la utafiti.

## 6.2 Uchunguzi wa Wahusika

Madumulla (2009) anaeleza kuwa wahusika ni viumbe wanaoonekana katika kazi za hadithi yoyote. Wahusika ni sehemu muhimu ya kazi ya kifasihi na wanatumiwa kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), wanyama kama wahusika wamekuwa na nafasi ya kipekee katika fasihi simulizi tangu enzi za kale hadi nyakati za sasa. Wahusika huwasilishwa kama binadamu walio na sifa zinazowakilisha maadili, tabia, itikadi na falsafa mbalimbali. Sifa hizi hujitokeza kupitia maneno na matendo yao. Kwa kutumia vigezo kama vile lugha, mienendo, sauti, na mazingira yanayowazunguka, usawiri wa wahusika hujengwa kwa uangalifu ili kusaidia kufikisha ujumbe unaolengwa. Sabido (2003) anaeleza kuwa wahusika kwenye hadithi husika hushirikisha watazamaji. Pia, wahusika huwashirikisha watazamaji au wasikilizaji ili wawe na uwezo wa kuelewa na kutafakari juu ya maudhui ya elimu. Kuwatazama wahusika wakifanikiwa kutokana na masuala fulani yanayowakumba huongeza imani ya watazamaji wa kufikia matokeo sawa.

Wahusika katika vipindi vya *Ubongo Kids* ni wanyama waliopewa tabia za wanadamu ili kuweza kuwasilisha masuala yanayoiathiri jamii. Wahusika hawa hubuniwa kwa maumbo tofauti, hutumia lugha rahisi na huwa na matendo ya kufurahisha watoto. Miongoni mwa wahusika katika vipindi vya *Ubongo Kids* ni pamoja na Ngendere, Mzee Kigo, Mama Ndege, Kibena, Kiduchu, Koba, Baraka na Uncle T.

### 6.2.1. Ngedere

Ngedere ni tumbili mwenye manyoya ya rangi ya kahawia na macho makubwa yanayong’aa, jambo linalomfanya kuwa kivutio kwa watoto. Ni mwenye hekima na

ujasiri, akijiajiri kama mfanyabiashara wa matunda sokoni. Aidha, ana ndoto za kupanua biashara yake na kujikimu zaidi kiuchumi.

Kupitia tabia zake, Ngedere anawakilisha dhamira ya ujasiriamali na uwezeshaji wa kiuchumi. Anaonyesha kuwa hata biashara ya kiwango cha chini inaweza kuwa mwanzo wa mafanikio makubwa. Anaibua masuala ya ubunifu, kujitegemea, na kutafuta suluhisho kwa changamoto za maisha ya kila siku. Kirui (2016) anaeleza kuwa Kenya inakabiliwa na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira, kama ilivyo kwa nchi nyingine zinazoendelea. Vijana ndio wanaathirika zaidi na tatizo hili. Hata hivyo, elimu ina jukumu katika kuamua ikiwa mtu atajiajiri au kuajiriwa kwa mshahara. Kulingana na takwimu za *World Bank Group* (2024), karibu asilimia 75 ya watu chini ya umri wa miaka 35 wanakabiliwa na fursa finyu za ajira nchini Kenya. Ingawa kiwango cha ukosefu wa ajira ni asilimia 5.4, na ukosefu wa ajira kwa vijana ikiwa asilimia 8.4, ajira nyingi zipo katika sekta isiyo rasmi, ambako hakuna uhakika wa ajira wala mshahara mzuri. Pia, kwa kuwa ni asilimia 10 tu ya wafanyakazi walio katika ajira rasmi, watu wengi wako katika kazi zisizo hitaji ujuzi (*World Bank Group*, 2024). Kwa kuwawezesha vijana kwa ujuzi na rasilimali za kuanzisha biashara zao binafsi, taifa linaweza kutoa nafasi ya ajira mpya na kuendeleza uchumi.

Kwa watazamaji, hususan watoto, Ngedere anawatia moyo kuona kazi kama jambo la furaha linaloweza kuchochea ubunifu na fikra za kujiajiri. Kicheko chake huburudisha na kusababisha kuwepo kwa mazingira ya ujifunzaji yenye furaha, akionyesha kwamba kazi ngumu pia inaweza kuwa ya kufurahisha. Kwa maoni ya Sabido (2003), wahusika hushirikisha watazamaji ambao hupata nafasi ya kujifunza masuala yanayowasilishwa kupitia wahusika. Wazo hili linashadidiwa na Njiiri na wenzake (2018) wanaoeleza kuwa wahusika huathiri watazamaji, hasa watoto na kuwafanya kufuata mienendo yao.

### 6.2.2 Mzee Kigo

Mzee Kigo ni mhusika aliyewahi kuishi mjini akifanya kazi za ofisini. Lakini Mzee Kigo hakufurahia uchafuzi, kelele na harakati za maisha ya mjini. Hivyo, alirudi kijijini Kokotoa kuanza kazi ya ukulima. Mzee Kigo anasawiriwa kama mtu mwenye busara, ukarimu na tajriba maishani. Tabia hii humfanya kuwa mshauri kwa watoto.

Aidha, wahusika katika kazi za kifasihi hufundisha masuala nyeti kupitia burudani (Sharma, 2023). Kwenye vipindi vya *Ubongo Kids*, mzee Kigo anasawiriwa kama mwenye ujuzi kuhusu masuala ya mazingira kama vile uchafuzi wa mazingira. Mzee Kigo ana ari ya kubadilisha jamii kwa kuhifadhi mazingira yake. Msimamo wa Mzee Kigo kuhusu uchafuzi wa mazingira inathibitishwa na maelezo ya Kirago na wenzake (2022) wanaosisitiza kuwa uchafuzi wa hewa ndio tatizo kuu la kiafya mazingira duniani kote. Barani Afrika, uchafuzi wa hewa husababisha takribani vifo vya mapema milioni moja kila mwaka, hali inayoufanya kuwa tishio kubwa zaidi kwa afya ya binadamu kuliko magonjwa makuu kama VVU au malaria. Ukuaji wa miji wa haraka na usiopangwa, unaoambatana na ukosefu wa miundombinu na sera madhubuti pia unachangia kuongezeka kwa viwango vya uchafuzi wa hewa katika miji ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Hadithi na maswali ya Mzee Kigo huburudisha huku yakielimisha. Kwa kutoroka maisha ya mjini yaliyojaa uchafuzi na kelele, Mzee Kigo anawasilisha umuhimu wa utunzaji wa mazingira na hatari zinazotokana na uchafuzi usiodhibitiwa. Mzee Kigo alipoamua kurudi kijijini na kulima, anaonyesha kuwa maisha ya kijijini yanawiana na mazingira na huwafundisha watoto umuhimu wa kilimo endelevu, kutunza mazingira, na kula chakula safi. Kama asemavyo Muge (2015), wahusika hutumika kuwasilisha mienendo halisi ya binadamu. Hivyo, mzee Kigo Mzee Kigo anaonyesha madhara ya uchafuzi wa mazingira na kusaidia watoto kuelewa umuhimu wa mazingira safi.

### 6.2.3 Mama Ndege

Mama Ndege amesawiriwa kama ndege mwenye hekima na aliyebobea katika hisabati. Yuko tayari kutoa ushauri kuhusu jambo lolote na ana tabia ya kujitokeza ghafla ili kusaidia panapokuwa na hitaji.

Mama Ndege hupenda nyimbo, densi na kucheka. Mhusika huyu hutumia vipengele hivyo kufundisha watoto somo la hisabati. Pia, Mama Ndege ana ujuzi kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwani anatumiwa na wanaobuni vipindi vya *Ubongo Kids* kuwasilisha suala la wanyama kama vile batabuku kuhama kwenye makao yao na barafu kuyeyuka kutokana na mabadiliko ya tabianchi (Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 5:12- 5:28).

Tabia za Mama Ndege inathibitishwa na mawazo ya Sabido (2003) anayeeleza kuwa wahusika huwashirikisha watazamaji kwa njia ya burudani na kuwaelimisha kuhusu suala katika kipindi teule. Mara nyingi, wahusika hutumiwa kama mawakal wa kuleta mabadiliko yanayokusudidwa. Katika suala la mabadiliko ya tabianchi na haki za watoto, Mama Ndege ni mwakilishi wa kiongozi anayetetea maadili mema na ufahamu kuhusu mazingira. Tajriba yake kuhusiana na masuala ya kimazingira yanajitokeza kila wakati anapoongea kupitia sauti nyororo na ya kupendeza. Anapojitokeza ghafla kusaidia, Mama Ndege huonyesha kwamba jamii inaweza kuwa na watu waaminifu wanaowajibika kusaidia kizazi kipya kutambua changamoto zao na kuzitatua. Anaelezea jinsi uchafuzi unavyoweza kuathiri maisha ya viumbe. Anatumia mfano wa dirisha chafu na safi akielezea jinsi uchafuzi wa mazingira huathiri binadamu (Ubongo Kids Kiswahili 2021c, 48:44- 49:06). Anaeleza kuwa akina Koba hawawezi kuona nyota hata kukiwa hakuna mawingu, kwani uchafu angani inazuia kuonekana kwao. Kukuwa na hewa safi kuona nyota inakuwa rahisi. Vilevile, Mama Ndege anaeleza kuhusu barafu inayoyeyuka na moto mkubwa unaonekana kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Pia, Mama Ndege huelimisha watoto kuhusu vyakula wanavyopaswa kula ili waweze kuwa na afya bora. Kwa mfano, Mama ndege anaimba:

(28). *Ili nikue nifanye nini?*
*Kula chakula mlo kamili,*
*Mlo kamili ni kitu gani?*
*Wanga, mafuta na vitamini*
*Usisahau protini, maji salama…*
(Ubongo Kids Kiswahili, 2019a, 0:28 – 0:41)

Kutokana na wimbo huu katika dondoo la (28), Mama Ndege amesawiriwa kama kiwakilishi cha lishe bora kwa watoto. Ni wazi kuwa ili watoto wakue vizuri, ni muhimu kula mlo kamili kila siku. Mlo kamili unajumuisha vyakula vya aina tofauti kama vile wanga kwa nguvu, protini kwa kujenga mwili, mafuta kwa joto, na vitamini kwa kinga ya mwili. Pia, watazamaji wanapaswa kunywa maji safi na salama ili kudumisha afya njema. Uwasilishaji wa Mama Ndege unaangazia elimu jumuishi kwa kutumia mbinu za kuvutia kama burudani, jambo linalowawezesha watoto kujifunza kwa urahisi.

### 6.2.4 Koba

Koba ana umri wa miaka kumi na moja. Anapenda kubuni filamu na ndiye kaka mkubwa wa Baraka na Mwenda. Ingawa mara nyingi hulalamika kwa marafiki zake, kwa siri hufurahia jukumu la kuwa kaka mkubwa. Pia hujitahidi kutekeleza wajibu kwa jamii kupitia majukumu kama kusambaza umeme shuleni au kumiliki bustani kijijini.

Wamitila (2003) anasema kuwa waandishi wa kazi za fasihi huchota matukio na visa kutoka katika jamii zao na kuviwasilisha kwa njia ya kisanaa katika hadithi. Uwasilishaji huu wa kisanaa unaonyesha kuwa mara nyingi wasanii huibua dhamira zinazochipuka kutokana na mazingira wanamoishi. Koba anaonyesha jinsi watoto wanaweza kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii kupitia ubunifu na uwajibikaji. Kupitia jukumu lake kama kaka mkubwa, anadhihirisha dhana ya elimu ya mtaala wa umilisi kwa vitendo vya kuwajibikia familia yake na jamii pana. Mchango wake wa kusambaza umeme shuleni na kumiliki bustani kijijini unahusiana moja kwa moja na masuala ibuka kama vile mabadiliko ya tabianchi (kupitia bustani ya kijiji inayoweza kukuza lishe bora na kuhifadhi mazingira), lishe bora (kwa kuhakikisha upatikanaji wa mboga safi), na elimu ya teknolojia (kupitia juhudi za kusambaza umeme).

Koba ni mfano wa mtoto anayejifunza kwa matendo, akisisitiza umuhimu wa elimu inayomwezesha mwanafunzi kuwa mshiriki katika utatuzi wa changamoto halisi za maisha. Sabido (2003) anafafanua kuwa wahusika huwasaidia watazamaji kufasiri masuala tata ya kijamii kupitia hadithi zinazoweza kuhusishwa na maisha yao. Hii inadhihirisha kuwa watoto, licha ya umri wao, wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo endelevu ya jamii zao.

### 6.2.5 Kibena

